Alhamisi Agosti 8, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579991
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

ST.JOSEPH UNIVERSITY
In Tanzania
"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"
Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA
SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on 24th August, 2019,
"Entrance is free". For details www.alumni.sjuit.ac.tz
For more information contact:
+255 676 504 147
+255 745 281 505
215359802



## Wananchi na mwekezaji wamweka pabaya DC kukwamisha uwekezaji

UKURASA 3

# Waingia mitini bil.430/- za mikopo elimu ya juu

UKURASA 2



## Mtendaji auawa kikatili kijijini

UKURASA 3

UKURASA 2

Wafanyabiashara wa vinyago na wachoraji, wakichangamkia fursa ya kuuza bidhaa zao kuelekea Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kwa kuzitandaza kando ya Barabara ya Samora, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



## Mkapa kufunguka anayoyajua SADC

MICHEZO AZAM YATUA ETHIOPIA NA MATUMAINI KIBAO UK.31 | MAONI, KATUNI UK.6

# Waingia mitini na bil. 430/- za mikopo ya elimu ya juu

**Na Mary Geofrey**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesema jumla ya wahitimu 145,656 hawajaanza kulipa mikopo yao ya jumla ya Sh. bilioni 432.5.

Kiasi hicho cha fedha ni zaidi ya bajeti ya HESLB kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambao bodi hiyo ilitoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 427 kwa wanafunzi 123,285. Kati yao, wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza walikuwa 40,544 na wanaoendelea na masomo walikuwa 82,741.

Akizungumza na Nipashe kwenye ofisi ya HESLB zilizoko Mwenge jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa bodi hiyo, Omega Ngole, alisema wadaiwa hao ni waliovuka kipindi cha miaka 10 tangu wahitimu, maarufu wadaiwa sugu.

"Jumla ya wahitimu 145, 656 ambao tunawaita sugu, hawajawahi kurejesha mikopo yao hata kidogo, fedha ambazo zinafika Sh. bilioni 432.5. Tuna mikakati mbalimbali ya kuhakikisha tunawapata ili waanze kurejesha," Ngole alisema.

Meneja huyo alitaja mikakati ya bodi hiyo kuhakikisha inawanasa wanufaika hao wa mikopo yake kuwa ni pamoja na kukutana na wadau wa kimkakati kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Chama cha Waajiri (ATE) na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kubadilishana taarifa za kuwabaini.

Ngole pia alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wanufaika na waajiri kuhusu umuhimu wa kurejesha mikopo yao kwa wakati.

Alisema bodi hiyo pia inafanya ziara za ukaguzi kwa waajiri kwa

INAENDELEA UK.26




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitoa heshima za mwisho kwa Natalia Bahati Kilangi, Mke wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi kabla ya mazishi yake yaliyofanyika Luchelele, jijini Mwanza, jana. **PICHA: OWM**

# Mkapa kufunguka anayoyajua SADC

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, anatarajiwa kuongoza mhadhara utakaohusu masuala mbalimbali ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), kwa kueleza historia na uzoefu wake wakati alipokuwa mwenyekiti wa jumuiya hiyo.

Mhadhara huo umepangwa kufanyika Agosti 15, mwaka huu kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na utashirikisha wasomi, wachambuzi na wahadhiri mbalimbali. Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipoeleza ratiba ya matukio ya Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi wa SADC.

"Kupitia kongamano hilo, Rais Mkapa ataelezea uzoefu wake wa uongozi wakati akiwa kiongozi wa SADC, ataelezea kiundani historia nzima ya jumuiya hiyo, si mnafahamu yeye alikuwa ndiyo gwiji wa jumuiya hiyo," Dk. Abbasi alisema.

Kiongozi huyo wa serikali alisema kwenye kongamano hilo kutakuwa na majadiliano yatakayohusu nchi za SADC yakiongozwa na Mkapa.

Dk. Abbasi aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kumsikiliza Rais Mkapa ambaye, akiamini watapata elimu ya kina kuhusu SADC.

"Tanzania imebeba historia kubwa kutokana na mchango wake kama vile kuzisaidia nchi nyingi za kusini kupata uhuru pamoja na kuzisaidia katika kupata maendeleo," Dk. Abbasi alisema.

Awali, Dk. Abbasi alitembelea mabanda ya maonyesho ya viwanda ya SADC yaliyoko katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC).

Aliwaomba wananchi kujitokeza kuona bidhaa nzuri zilizotengenezwa na wajasiriamali wa SADC kwa kuwa maonyesho hayo hayana kiingilio.

Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi za SADC umetanguliwa na maonyesho ya nne ya viwanda ya SADC, yakifunguliwa Agosti 5 na Rais John Magufuli. Mbali na JNICC, maonyesho hayo pia yanafanyika viwanja vya Gymkhana na Karimjee jijini.

Tanzania inatarajia kupokea marais 16 kutoka Nchi za SADC wakifuatana na wageni wengine zaidi ya 1,000 kwa ajili ya kushiriki mkutano huo Agosti 17 na 18. Mara ya mwisho Tanzania kuongoza mkutano huo ilikuwa mwaka 2003, kipindi ambacho nchi ilikuwa chini ya uongozi wa Rais Mkapa.

## Samia ataka vyuo vikuu kubuni vyanzo mbadala

**Idda Mushi na Christina Haule,** MOROGORO

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu, amevitaka vyuo vikuu nchini kubuni vyanzo mbadala vya kuwaingizia mapato ili kujiendesha.

Alivitaka kubuni vyanzo vipya badala ya kusubiri ruzuku kutoka serikali kuu, na kwamba vyanzo visiathiri kwa namna yoyote taaluma inayotolewa.

Samia alisema hayo wakati wa kuweka jiwe la msingi ujenzi wa maabara mtambuka ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), inayojengwa na mkandarasi SUMA JKT, chini ya Mshauri Mwelekezi Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) kwa kushirikiana na Norrplan, ambapo kukamilika kwake kutawezesha kuchukua watu 2,400 kwa wakati mmoja.

Makamu wa Rais licha ya kupongeza kazi nzuri iliyofanyika, aliitaka SUA kuhakikisha utafiti mbalimbali wanaofanya unawafikia wananchi wa vijijini kutokana na changamoto iliyopo sasa ya utafiti kutofika maeneo hayo.

Alisema kukamilika kwa maabara hiyo kubwa kutasaidia kuongeza tija na kukuza uchumi wa nchi kupitia utafiti na mafunzo ya ugani yatakayowafikia wakulima na kutaka maofisa ugani watumike kwa namna mbalimbali kusaidia kusambaza utafiti unaofanywa na wataalam kufika kwa wananchi kwa urahisi.

Makamu wa Rais alisema Serikali imejipanga kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo katika sekta ya kilimo, unaolenga kuhakikisha sekta hiyo inakuwa na tija, kuzalisha bidhaa na kuwa na viwanda vya kuchakata pamoja na kutafuta masoko sambamba na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aliishauri menejimenti ya SUA kuweka katika mitaala yao somo la Uzalendo kwa kuwekewa mkazo ili wataalamu wanaotoka chuoni hapo waweze kufanya kazi na kutumika kwa manufaa ya wakulima, wafugaji na wavuvi kwa manufaa ya taifa.

Aidha alisema Serikali katika kukuza tija kwenye kilimo, imetenga Sh. bilioni 126 kwenda kwa Wakala wa Taifa wa Mbegu za Kilimo (ASA).

Mwenyekiti wa Baraza la SUA, Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Othman Chande, alisema chuo hicho ni tajiri kwenye taaluma, ugani na utafiti, ingawa bado ni masikini kwenye bajeti ya maendeleo na kuomba Serikali iendelee

INAENDELEA UK.26



Mwendesha bodaboda akiwa amepakia tairi na abiria juu, katika barabara ya Mandela, eneo la Tabata, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Ewura washusha bei petroli, dizeli

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) imetangaza kupungua kwa bei ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kuanzia jana.

Hata hivyo, bei mpya ya nishati iliyotangazwa na mamlaka hiyo inatofautiana kutoka kanda moja hadi nyingine kutokana na bandari inakotoka na usafirishaji wake.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa jana kwenye vyombo vya habari, bei ya petroli imepungua kwa Sh. 160 kwa lita ikiwa ni asilimia 6.9.

Vilevile, bei ya mafuta ya dizeli imepungua kwa Sh. 102 kwa lita sawa na asilimia 4.63 na mafuta ya taa Sh. 81 kwa lita, sawa na asilimia 3.75.

Katika tangazo hilo, kwa bidhaa zinazoingizwa kupitia Bandari ya Mtwara kwa ajili ya mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, bei imepungua kwa petroli Sh. 105 kwa lita (asilimia 4.5), dizeli Sh. 124 (asilimia 5.43).

Kwa mwezi uliopita, bei ilikuwa ni petroli Sh. 104.24, sawa na asilimia 4.74 na dizeli Sh. 123.57, sawa na asilimia 5.72.

Mamlaka hiyo ilieleza kuwa punguzo la bei limetokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na mabadiliko ya gharama za usafirishaji.

"Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke kikomo kama ilivyokokotolewa na kanuni iliyopitishwa na Ewura," mamlaka hiyo ilieleza katika tangazo lake hilo.

# Wananchi na mwekezaji waushtaki uongozi wilaya

**Na Mwandishi Wetu,**
MBULU

WANANCHI wa Kijiji cha Eshkeshm, Bonde la Yaedachini wilayani Mbulu mkoani Manyara wamelalamikia kitendo cha baadhi ya viongozi wa wilaya hiyo kuupiga vita uwekezaji wa ranchi ya kisasa ya mifugo.

Mradi huo ulikuwa unatekelezwa na kampuni ya Baragweka Farm Limited ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 10.

Wananchi hao wamesema baadhi ya viongozi hao ngazi ya wilaya wamekuwa wakizusha maneno ya uongo dhidi ya mwekezaji huyo aliyefika kijijini huko miaka tisa iliyopita kwa lengo la kufungua ranchi ya kisasa ya uzalishaji mifugo katika kijiji hicho kwa kudai kuwa eneo analomiliki ni mapito ya wanyama, jambo ambalo halina ukweli.

Pia viongozi hao wanadai kuwa mwekezaji huyo hakufuata taratibu za umiliki wa eneo hilo wakati wananchi wenyewe ndiyo waliamua kumpatia eneo hilo.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliohudhuriwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliyetembelea eneo hilo kusikiliza changamoto za wafugaji na kutembelea miradi ya uwekezaji iliyofanywa na kampuni hiyo, wananchi hao walieleza kushangazwa na mgogoro huo.

Wananchi hao walimweleza Waziri Mpina kuwa walikubaliana kama kijiji kwa nia njema na kuamua kumgawia mwekezaji huyo eneo la hekta 3,903 ili kuanzisha ranchi hiyo, lakini wanashangazwa kuona mwekezaji huyo anazuiliwa na baadhi ya viongozi wa wilaya kutoendeleza eneo hilo na kufikia hatua ya kumchomea maeneo yake ya malisho.

Wafugaji hao, Daniel Gudal na Itamuka Ntaja walisema eneo la malisho ya mifugo Yaedachini lililotengwa halina huduma zozote ikiwamo maji na hivyo kusababisha mifugo yao kusafiri umbali mrefu kutafuta maji na halikuwa na huduma nyingine muhimu za kijamii zikiwamo shule.

Walisema tangu mwekezaji huyo afike kijijini huko, wamenufaika na uwapo wake kwa kuwajengea visima vya maji, majosho, shule na mashine ya kusaga.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, alisema eneo hilo ni mapito ya wanyama na halifai kwa matumizi ya shughuli za ufugaji, jambo lilipingwa wananchi wa kijiji na kumzomea kwa madai kuwa maelezo hayo ni ya uongo na yana lengo la kumkwamisha mwekezaji huyo kwa maslahi binafsi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Baragweka Farm Limited, Gesso Bajuta, alisema mradi huo hadi sasa umegharama ya Sh. bilioni 1.6 ikijumuisha ng'ombe bora 486, mbuzi 270, kondoo 216, ujenzi wa nyumba ya mwalimu, madarasa, ujenzi wa vyoo, josho la mifugo, mradi wa maji, nyumba na mashine ya kusaga.

Alisema kampuni hiyo pia imeziazima kaya 20 madume bora 20 na mitamba 30 kwa lengo la kuboresha koosafu za

INAENDELEA UK.26

# Mtendaji auawa kikatili kijijini

**Na Mohab Dominick,**
KAHAMA

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Nyambula Kata ya Ngogwa wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Khamis Kadelanha, ameuawa kikatili na watu wasiojulikana, huku watu wengine wawili wakiwa wamelazwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyambula, William Mzava, kizungumza jana na wanahabari alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana.

Mzava alisema kuwa Kadilanha akiwa amelala na mkewe, Shija Maziku, walivamiwa na kundi la watu ambao hawakufahamika kisha kuwashambulia kwa kuwakata na kitu chenye ncha kali kichwani na mabegani, na kusababisha kifo chake papo hapo.

Kwa mujibu wa ofisa mtendaji huyo, mtu mmoja ambaye ni mwanafamilia wa marehemu (jina limehifadhiwa), anashikiliwa kwa tuhuma za kuhusika na tukio hilo huku wengine hawajakamatwa.

Aliwataka wanakijiji kushirikiana na serikali ya kijiji katika kuimarisha ulinzi shirikishi ili kuepuka matukio kama hayo kuendelea kujitokeza.

Dalali Kadelanha, kaka wa marehemu, alisema usiku alisikia kelele, lakini alidhani ni za walevi, hivyo kuzipuuzia, ingawa baadaye ndipo walipopata taarifa kuwa ni mdogo wake aliyekuwa akishambuliwa.

Mmoja wa mashuhuda, Katarina Mihayo, alisema alifika haraka katika tukio hilo ndipo alipotoa taarifa katika uongozi wa kijiji ambao nao uliwasiliana na Jeshi la Polisi ambao walifika na kuuchukua mwili pamoja na majeruhi, akiwamo mke wa marehemu ambaye alijeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili.

Richard Abwao, Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwataja wengine waliojeruhiwa ni dada wa marehemu, Shija Kadilanha ambaye alijeruhiwa kwa kukatwa panga katika mkono wake wa kulia na sehemu mbalimbali, na kuwa chanzo cha tukio hilo ni imani za kishirikina.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliyefika kijijini hapo kutoa pole, amewataka wanafamilia pamoja na wanakijiji kuwa wapole na kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika kuwabaini waliohusika na tukio hilo na kwamba yeye kama mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya atahakikisha usalama unaimarika katika kijiji hicho.


**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA AT DAR ES SALAAM**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.46 OF 2017**
**IN THE MATTER OF ADMINISTRATION OF THE ESTATE OF THE LATE THOMAS ANTHONY MASAWE**

**NOTICE TO CREDITORS AND PERSONS WITH CLAIM**

**NOTICE** is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above-named, **THOMAS ANTHONY MASAWE** deceased, who died at Lugalo Hospital, Kinondoni, Dar es Salaam on the 10th day of April, 2017 and probate of whose letters of administration of whose estate was granted to me, **PHILIPO ANTHONY MASAWE** by the High Court on the 16th day of October, 2017 are hereby required to send in their claims to me at the following address within sixty days from the date of the publication of this notice at the expiration of which time I shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims of which I shall then have had notice.

Philipo Anthony Masawe,
P.o BOX 252,
Hai.

115366102

# Nyumba 56 kupigwa mnada

Na Salome Kitomari

NYUMBA 56 na magari matatu katika maeneo mbalimbali nchini, zimetangazwa kupigwa mnada kutokana na wamiliki wake kuchukua mkopo benki na kushindwa kulipa.

Nyumba hizo zipo katika mikoa ya Dares Salaam, Mwanza, Tabora, Mbeya na Iringa.

Tangazo hilo ambalo lilikuwa kwenye moja ya magazeti ya kila siku, lilieleza kuwa benki ya Access imepata kibali cha kuuza mnada wa hadhara mali ambazo ziliwekwa dhamana ya mkopo kwa wahusika na kushindwa kulipa.

“Ifahamike itakapopita muda wa siku 14 kwa dhamana ya nyumba au kiwanja, zitauzwa kwa njia ya mnada kwa siku husika iliyopangwa, mnada utafanyika sehemu nyumba na kiwanja husika vilipo,” tangazo hilo lilieleza.

Aidha, tangazo hilo lilifafanua kuwa mshindi atatakiwa kulipa asilimia 25 ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapotangaza kuwa mshindi na kwamba asilimia 75 lazima ilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada.

“Kiasi cha asilimia 25 kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika

INAENDELEA UK. 8



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa maabara kubwa kwa Afrika ya Sayansi, katika Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA), mkoani Morogoro jana. Makamu wa Rais yupo mkoani humo kwa ziara ya kikazi ya siku tatu. Wanaoshuhudia ni Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako. **PICHA: OMR**

# Mahakama sasa yakubali kuchukua kielelezo cha Aveva

Na Hellen Mwango

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imekubali kupokea maelezo ya onyo ya Rais wa Klabu ya Simba, Evance Aveva kama kielelezo katika kesi ya kughushi na kutakatisha Dola za Marekani 300,000 inayowakabili na makamu wake Godfrey Nyange, maarufu kama Kaburu.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya majibishano ya kisheria ya pande zote mbili kuhusu kupokelewa maelezo hayo.

Awali, upande wa utetezi ulipinga mahakama hiyo kupokea maelezo kwa kuwa shahidi ambaye ni Mchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Frank Mukilanya, hakustahili kuyatoa.

Utetezi ulidai shahidi alichunguza kesi hiyo na wakati huohuo alimhoji mtuhumiwa hivyo hakustahili kufanya kazi mbili kwa wakati mmoja, hakustahili kutoa maelezo hayo.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Leonard Swai, ulipinga pingamizi la utetezi kwa kuwa halikuwa na mashiko ya kisheria.

Swai alidai kuwa mchunguzi kumhoji na kuandika maelezo ya onyo ni sahihi kisheria aliomba mahakama kutupilia mbali pingamizi la utetezi.

Jana, mahakama hiyo ilitupilia mbali pingamizi la utetezi na ilikubali kupokea maelezo ya Aveva kama kielelezo katika kesi hiyo.

Hakimu Simba alisema mahakama yake itaendelea kusikiliza ushahidi wa Jamhuri Agosti 20 na 22, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Shadrack Kimaro, alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016, Aveva na Kaburu walikula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya

INAENDELEA UK. 8

# TBS yaandaa kanuni mpya kuirithi TFDA

Na Mary Geofrey

SHIRIKA la Viwango (TBS) limesema linaendelea kutunga kanuni mpya zitakazoliongoza kutekeleza majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ambayo imefutwa.

Vilevile, shirika hilo limeiomba serikali ilipe kibali cha kuwachukua baadhi ya watumishi waliokuwa TFDA ili walisaidie kuongeza nguvu kusimamia masuala ya chakula na vipodozi yaliyokuwa yanasimamiwa na mamlaka hiyo iliyofutwa.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa TBS, Roida Andusamile, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa chini ya TFDA.

Alisema kwa sasa wako katika kipindi cha mpito cha kuandaa kanuni zitakazotumika katika utekelezaji wa majukumu hayo na wanatarajia zitakuwa tayari katika miezi miwili ijayo.

“Tunatarajia kuanza utekelezaji kwa ukamilifu ifikapo Oktoba Mosi, mwaka huu. Hata hivyo, shirika limeendelea kupokea maombi, kuuhisha vibali vya usajili wa bidhaa mbalimbali na majengo ambayo zilikuwa zinasajiliwa na TFDA hapo awali,” Roida alisema.

Aliongeza kuwa kanuni zinazotumiwa na shirika hilo kwa sasa kushughulikia masuala ya chakula na vipodozi ni za TFDA na wanalazimika

INAENDELEA UK. 8


Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku

215227501



# HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (wa pili kulia), akiangalia mashine itakayotumiwa na Idara ya Uhamiaji ikiwa ni utekelezaji wa mabadiliko ya teknolojia kutoka pasi za zamani za kusafiria kwenda za kielektroniki, alipotembelea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, mjini Zanzibar jana. **PICHA: WMNN**

## UTSS yatiwa moyo ujumbe wa Katibu Mkuu wa SADC

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Under The Same Sun (UTSS) limetiwa moyo na ujumbe uliotolewa na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Dk. Stergomena Lawrence Tax, wakati wa maadhimisho ya mwaka huu ya Siku ya Kimataifa ya watu wenye ualbino (IAAD), inayoadhimishwa kila mwaka Juni 13.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTSS, Berthasia Ladislaus, alisema hayo jana wakati kizungumza na waandishi wa habari jana, Karimjee jijini Dar es Salaam, katika maandalizi ya mkutano wa SADC.

Alisema katika ujumbe wake, Dk. Tax alisema, "Tunatambua watu wenye ualbino wanaendelea kukosa haki zao za kibinadamu kwa njia tofauti ikiwamo unyanyapaa, kukosa huduma ya matibabu na elimu, pia kutengwa kijamii na kisiasa."

Alisema ujumbe huo aliutoa wakati watu wenye ualbino katika nchi za SADC wakiendelea kupambana na changamoto za kukosa haki zao za kibinadamu na kukosa ulinzi.

Alimnukuu Dk. Tax akisema: "Kutokana na sababu hii SADC inaendelea kulaani kwa nguvu aina yoyote ya ukandamizaji na udhalilishaji dhidi ya watu wenye ualbino."

Alisema changamoto wanayokutana nayo watu wenye ualbino inatokana na

INAENDELEA UK. 26

## Nchi za SADC zahimizwa matumizi ya vipimo sahihi

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), zimehimizwa kuzingatia matumizi sahihi ya vipimo katika uzalishaji wa bidhaa kuepuka kuwekewa vikwazo wanapotaka kuuza katika nchi nyingine.

Akizungumza jana katika Maonyesho ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya SADC, Meneja wa Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) katika kitengo cha bandari, Peter Chuwa, alisema jumuiya hiyo inayo miongozo mbalimbali ya vipimo ambayo inapaswa kuzingatiwa na nchi wanachama.

Alisema hata sheria za vipimo nchini zimetungwa kwa kuzingatia miongozo hiyo na kwamba wamekuwa wakitoa elimu kwa wafanyabiashara na wazalishaji viwandani kuizingatia ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

"Tumepata manufaa mengi kuwamo kwenye SADC, tunatunga sheria zetu kulingana na miongozo ya vipimo ya SADC na tunahakikisha hata bidhaa zinazoingia nchini zinakidhi vigezo," alisema Chuwa.

Meneja huyo aliitaja baadhi ya miongozo hiyo kuwa ni ule unaohusu ufungashaji wa bidhaa ambao unalenga kuhakikisha zinakuwa na ulinganisho sahihi.

Hata hivyo, alisema bado kuna changamoto kwa baadhi ya wazalishaji ndani ya SADC kutozingatia miongozo ya kitaalamu ya vipimo na kusababisha bidhaa nyingi kukosa vigezo na kushindwa kufanya vizuri sokoni.

Naye wa WMA, Irene John, alisema wakala huo unahakikisha kuwa vipimo vyote ni sahihi na vinatumika kwa usahihi kulingana na Sheria ya Vipimo Sura 340 mapitio ya mwaka 2002 na maboresho yake ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake.

"Tunawahamasisha wananchi, wafanyabiashara na wenye viwanda waje kutembelea maonyesho haya ili kujifunza mengi kuhusu masuala ya vipimo na miongozo mbalimbali ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na zinazoweza kuuzika katika soko zima la SADC," alisema Irene.

## Tanzania, Uganda kujenga kituo kufua umeme wa maji

**Na Romana Mallya**

SERIKALI ya Tanzania na Uganda zinatekeleza ujenzi wa mradi wa ujenzi wa kituo cha kufua umeme wa maji wa Kikagati-Murongo, uliopo kwenye mto Kagera mpakani mwa nchi hizo utakaozalisha megawatts 14.

Inakadiriwa kuwa kila nchi itapata megawatts saba kati ya hizo 14 zitakazozalishwa mara baada ya mradi huo kukamilika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Geoffrey Mwambe, ametaka maazimio ya mradi wa ujenzi huo ya asilimia 50 kwa 50 yaliyofikiwa na nchi hizo mbili, yazingatiwe.

"Nilitembelea eneo la mradi ambako ujenzi unaendelea na nimetaka maazimio ya ujenzi wa mradi huo ya asilimia 50 kila upande wa nchi hizi, yazingatiwe," alisema.

Alisema mradi huo wa umeme unajengwa na kampuni ya kikandarasi ya PAC ya Italia na unasimamiwa na kampuni binafsi ya Uganda ya Kikagati-Murongo hydropower project.

Alisema ujenzi huo ulianza mwezi Mei mwaka 2018 na unatarajiwa kukamilika Mei 2021 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 90.

Alisema ujenzi huo ni makubaliano ya nchi hizo ili kuwa na matumizi bora ya maji ya Mto Kagera ambao upo mpakani kati ya Tanzania na Uganda.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kupatikana kwa umeme wa uhakika.

Mhandisi Mshauri wa mradi huo, kutoka kampuni ya nguvu za nishati ya geni, mhandisi Juliana Pallangyo, alisema watasimamia ipasavyo ili kuufanikisha mradi huo ili kila nchi iweze kunufaika nao.


## KUMBUKUMBU



**SALUM HERI PUGA**

Siku, wiki, miezi na miaka imepita hatimaye leo tarehe **8/8/2014** unatimiza miaka mitano tangu ulipotutoka na kutuachia majonzi makubwa yasioweza kufutika.

Machozi yametukauka machoni mwetu lakini moyoni bado tunakulilia.

Ukarimu, ucheshi, busara, upendo na upole wako bado vinakumbukwa na wazazi, ndugu na marafiki zako wote uliosoma nao Nur Yakeen Secondary School Temeke.

Hakika tulikupenda Baba Mzazi Heri Puga, Mama Mzazi Mariam Njoroge na Mdogo wako Shaban Heri Puga.

**INA LILAHI WAINA ILAHI RAJIUUNA.**

615365502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nanenane isaidie kukabili mabadiliko ya tabianchi

**KILA** mwaka Agosti 8, ni Maadhimisho ya Nanenane au Siku ya Wakulima ambayo pamoja na wiki nzima ya maonyesho ya Nanenane yanayofanyika kwa kuzunguka kila mkoa, kuna maadhimisho ya kikanda na ya kitaifa.

Tunawapongeza wakulima, wavuvi na wafugaji wanaoshiriki katika siku hiyo kwa moyo mkunjufu tunasema hongera, wakulima wetu wavuvi na wafugaji kwa kuiwezesha Tanzania kuwa na chakula cha kutosha.

Ni wazi kuwa maadhimisho ya Siku ya Nanenane zama hizi yanafanyika katika kipindi ambacho dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi yanayotishia maisha.

Hilo hutokea kutokana na ongezeko la joto duniani, uhaba wa maji, vimbunga, mafuriko na ukame wa muda mrefu nayo pia ni mambo yenye taathira inayojitokeza mara kwa mara kipindi hiki.

Mabadiliko hayo na ongezeko la joto huathiri uzalishaji, ufugaji na uvuvi baharini kwa kuwa maziwa na mito hupungua kina na wakati mwingine vinakauka.

Kila eneo linaathirika. Wavuvi wanalazimika kuwa na mifumo bora ya kuvua na kujenga mabwawa ya kulisha samaki.

Tena uvuvi wa samaki nao unatakiwa kufanywa na usimamizi wa hali ya juu kwa kutumia nyavu na teknolojia rafiki.

Kwenye kilimo hali ni mbaya zaidi, wakulima wanaambulia hasara kutokana na ukame, lakini pia huumizwa na uwekezaji kutokana na kutumia fedha nyingi kununua pembejeo lakini hakuna tija.

Si hivyo tu wafugaji nao hasa wahamaji wanaotembea na mifugo yao huathiriwa na ukame unaosababisha vifo na hata magonjwa ya mifugo.

Mabadiliko ya tabianchi yameleta changamoto nyingi ndiyo maana tunaomba serikali na wadau kuwasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi wetu kujua mbinu mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kutokana na changamoto hizi ni wakati ambao serikali na wadau wana wajibu wa kutumia muda mwingi kuwafunza wahusika namna bora za kutumia mbegu zenye ukinzani na ukame, maradhi na zinazozaa sana kwa upande wa wakulima.

Aidha, kwa wafugaji ni muhimu pia kufunzwa namna bora ya kutunza wanyama na kuwa na wanyama wanaoweza kuhimili madhara yatokanayo na tabia nchi.

Pia kutafiti vyakula ambavyo vina virutubisho kwa wanyama, mchanganyiko ambao silazima mnyama ale kiasi kingi lakini hata akitumia kidogo anapata afya na lishe bora.

Yote hayo ni katika jitihada za kupunguza matumizi ya nyasi nyingi, maji pamoja na maeneo makubwa ya kulishia vitu ambavyo vina athari kwa dunia ya leo kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mafunzo ya mara kwa mara na kuandaa mbinu za kimkakati kukabiliana na matatizo ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi yatawafanya wakulima, wafugaji na wavuvi kupata mbinu na mikakati mipya ya kuboresha shughuli zao.

Wakulima ndiyo walio kwenye hali mbaya zaidi hivyo Nanenane zitumike kuboresha shughuli zao.

Tunaamini kuwa vituo vya utafiti zama hizi pamoja na kuhimiza mabadiliko kiufugaji ni lazima kuangalia mbinu mbadala za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuleta teknolojia nyepesi na nafuu kwenye kilimo hasa mazao ya mkakati ambayo yanatanufaisha taifa na wakulima kimapato.

Shime serikali na wadau Nanenane za wakati huu zisiwe za maonyesho ya kibiashara zaidi bali zijikite kwenye mbinu na teknolojia mpya zitakazosaidia kukuza na kuongeza uwekezaji kwenye sekta za uvuvi, kilimo na ufugaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waathirika dawa za kulevya wanusuriwe kupitia njia hii

Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya wawakilishi wa wananchi bungeni, wamewahi kuibua tuhuma nzito juu ya tabia chafu zinazofanywa na baadhi ya wamiliki wa nyumba za kutibu waathirika na dawa za kulevya, maarufu 'sober house.'

Ilikuwa Aprili mwaka jana mbunge kijana, Halima Bulembo, alipodai baadhi ya wamiliki wa nyumba hizo huwachoma tena sindano za dawa za kulevya, vijana wanaokaribia kupona, ili wasitoke 'sober house.'

Kwa mujibu wa Bulembo, lengo kubwa la kufanya hivyo, ni kutaka kuendelea kuingiza pesa kupitia waathirika na alitaka maelezo kutoka serikalini, kuhusu hatua zinazochukuliwa.

Baada ya tuhuma hizo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), Jenista Mhagama, alikiri kuptia kauli sio mara ya kwanza bungeni na akawaonya wahusika wanaoendekeza nyendo hiyo.

Pamoja na hayo, mjadala bado unaendelea. Kwa maoni yangu, kuna haja ya serikali kutafuta ufumbuzi katika hilo kwa kujenga 'sober house' nyingi nchini na itakayowakusanya waathirika wa dawa za kulevya waishi humo.

Hizo zinapaswa kuwa na maeneo ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji mali, ili waathirika wanapopona, wageuke kuwa wazalishaji mali, zikiwamo za kilimo inayowakwamua kiuchumi.

Nasema hivyo, kutokana na ukweli waathirika walio nje ya 'sober house' wakitokea majumbani kwenda kupata matibabu vituoni kisha wanarudia mazingira yao, wanakumbwa na vishawishi vinavyowafanya warudie 'uteja' hata baadhi hatua mbaya kama vile kupoteza maisha.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa afya, mtu anapotumia methadone (dawa za matibabu) na kurudia dawa za kulevya, ana uwezekano mkubwa wa kupoteza maisha na tena kifo cha ghafla kwa kuzidisha matumizi.

Hivyo, ili kuwanusuru waathirika ni vyema kuwa na sober house nyingi nchini zenye maeneo kwa ajili ya uzalishaji mali na kuwaweka wote huko wakiwa chini ya uangalizi wa hali ya juu.

Ni ukweli usiopingika kwamba matumizi ya dawa za kulevya ni moja ya matatizo makubwa yanayozikumba nchi mbalimbali duniani, ikiwamo Tanzania, vijana wanatajwa kuathirika zaidi kwa dawa hizo.

Madhara ya dawa ya kulevya yako katika nyanja mbalimbali kwani watumiaji wanaweza kushiriki katika vitendo vya kihalifu ikiwamo wizi na ukahaba ili kupata fedha za kununua dawa hizo.

Dawa hizo zinasababisha utegemezi wa kisaikolojia na utegemezi wa kiuchumi. Pia, inafanana na kujichimbia kaburi bila kujua, athari za kiakili na kimwili.

Janga mojawapo la kiafya liko kwa watumiaji, ni kuambukizwa virusi vya Ukimwi (VVU) kwa mtu sindano kutumiwa na mtu zaidi ya mmoja, hali inayokaribisha maambukizi.

Kwa mujibu wa ripoti mpya ya Shirika la Umoja wa Mataifa linalopambana na Ukimwi (UNAIDS), ingawa maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU), duniani kote yamepungua, lakini maambukizi miongoni mwa wanaojidunga sindano za dawa hizo, hayapungui.

Ripoti iliyondoluwa Machi mwaka huu mjini Geneva, Uswisi, ikionyesha asilimia 99 ya watu wanaojidunga dawa za kulevya wanaishi katika nchi ambazo hazitoi huduma ya kupunguza madhara.

Inafafanua zaidi kuwa katika wastani wa watu milioni 10.4 wanaojidunga sindano za dawa za kulevya mwaka 2016, zaidi ya nusu walikuwa wanaishi na maradhi ya homa ya ini (Hepatitis C) na wanane ambao ni wastani wa nusu orodha hiyo, walikutwa na VVU.

Shirika hilo linashauri kuwaweka watu katika vituo vya malezi, wakihakikishiwa wanapata huduma bora za afya za kijamii kwa misingi ya utu, pasipo na ubaguzi dhidi ya dai la makosa yao na kwamba maisha yanaweza kuokolewa na maambukizi mapya ya VVU kupungua.

Pia iko wazi na sahihi kutambua juhudi zinazofanywa na serikali katika kuhakikisha matumizi ya dawa za kulevya yanakoma nchini, lengo kuu ni kuokoa nguvukazi ya taifa, ambayo kimsingi ni kundi la vijana.

Nchini, serikali imeanzisha vituo vingi vya kutoa dawa zinasaidia waraibu kuacha matumizi ya dawa za kulevya, pia kuna nyumba za kuwatibu waathirika wa dawa za kulevya.

Kimsingi, zote ni jitihada za kutaka kuhakikisha watumiaji dawa za kulevya wanaachana nazo na kurejea hali ya kawaida, hatimaye wenye manufaa kwa familia, jamii na taifa lao.

Mtazamo mkubwa niliyo nao kuptia mjadala huu, ni kwamba ushauri ufanyike kitaifa kwa kuanzishwa maeneo ya kutosha ya shughuli za uzalishaji mali, wahusika wapewe faida kwa familia, jamii na taifa lote.

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima (wa pili kulia), akiangalia namna dhahabu inavyochenjuliwa na Mary Matiko Makorere kwa kutumia zebaki katika eneo la wachimbaji wadogo katika wa Mtaa wa Kebaga, Kata ya Kenyamanyori, wilayani Tarime, mkoa wa Mara. **MPIGAPICHA WETU**

# Bodi yalalamikia utitiri wa viwanda mifuko isiyo bora

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Chama cha Ushirika wa Viwanda Vidogo Mkoa wa Dar es Salaam (Dasico), imeliomba Shirika la Viwango Tanzania (TBS), kudhibiti utitiri wa viwanda vinavyotengeneza mifuko ya karatasi isiyo na ubora.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa mwaka wa chama hicho, Mwenyekiti wa Dasico, Mfaume Yusufu, alisema tangu kupigwa marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki, kumeibuka utitiri wa viwanda vinavyotengeneza mifuko ya karatasi kiholela.

Alisema utitiri wa viwanda hivyo unaathiri watumiaji na viwanda ambavyo vimewekeza na kudhibitishwa na mamlaka zinazohusika na udhibiti wa ubora.

"Sasa hivi kumeibuka utengenezaji wa mifuko ya karatasi kiholela ambayo ni ya ajabu. Huko mitaani hivi sasa kila mtu anachukua viroba na kutengeneza mifuko ya karatasi ambayo hata haieleweki na mingine inachanika ovyo, unaweza ukabebea kitu unashangaa unakuchanikia," alisema na kuongeza:

"Kwa hiyo tunawaomba hao wenye mamlaka wakague mifuko inayowekwa kiholela mitaani ili wajue ubora wake ukoje na ninaamini kwamba wakifanya ukaguzi watabaini mifuko mingi mibovu na watapiga marufuku, tunaunga mkono hatua

INAENDELEA UK.26

# Oxfarm yasaidia maelfu wakulima wa mkonge

**Na Happy Severine,** SIMIYU

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali Oxfarm kupitia asasi ya Redeso ya jijini Dar es Salaam limeanzisha kilimo cha mkonge katika wilaya za Kishapu mkoani Shinyanga na Meatu mkoani Simiyu na kuongeza thamani.

Kupitia mradi wake wenye malengo ya kuongezeka thamani mazao, kupunguza umskini vijijini, uwazi na uwajibikaji pamoja na usawa wa kijinsia jumla ya wakulima 3,500 wamefikiwa na kubadilishwa maisha yao.

Akizungumza kwenye Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) kitaifa kwenye viwanja vya Nyakadindi mkoani Simiyu, Meneja mradi kutoka Redeso, Charles Bligea alisema wakulima hao walionufaika ni kutoka kwenye vijiji 10 Meatu na vijiji 30 Kishapu.

Alisema lengo la Oxfarm kupitia Redeso la kuanzisha kilimo cha mkonge kwenye wilaya hizo ni kutokana na kukabiliwa na ukame mkubwa huku wakulima wakibaki maskini kutokana na mazao waliyokuwa wakilima kutohimili hali hiyo.

"Tuliona ili kubadilisha maisha yao tuanzishe zao la mkonge ambalo linahitaji maji kidogo na linaweza kustawi kwenye ukame, mradi ulianza kujikita kwenye zao hilo toka mwaka 2012 na utaisha 2021," alisema Bligea.

Alisema mradi huo ulilenga kuwapa elimu juu ya zao hilo wakulima, kuwatafutia soko la uhakika, kuwapatia teknolojia rahisi za kuongeza thamani na ubora ikiwa pamoja na kuwaunganisha na wadau wengine katika kuboresha zao hilo.

Aliongeza kuwa mradi huo umeonyesha mafanikio makubwa, ambapo awali zao la mkonge kwenye wilaya hiyo lilitumika kama uzio wa mashamba yao na sasa hivi limekuwa zao kubwa la kibiashara.

"Sasa hivi wananchi wengi wameanza kulima zao hili kama mazao mengine, kuna zaidi ya hekari 200 sasa hivi mpya ambazo

INAENDELEA UK. 26

# Waziri Mkuu aongoza mazishi ya mke wa AG

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, jana aliaongoza mazishi ya mke wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, Natalia Bahati Kilangi.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali katika mazishi hayo yaliyofanyika nyumbani kwa Prof. Kilangi eneo la Luchelele jijini Mwanza, Waziri Mkuu alimuomba Prof. Kilangi na familia yake kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu ambapo wamempoteza mama ambaye ni nguzo muhimu ya familia.

Kadhalika, Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuwasilisha salamu za pole kutoka kwa Rais John Magufuli kwa Prof. Kilangi na familia yake kutokana na msiba mzito walioupata.

Katika salamu zake Rais Magufuli alisema Serikali inathamini sana mchango mkubwa na mahili unaotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na anamini kwamba kwa vyovyote vile wakati wa uhai wake, marehemu Natalia alishiriki kwa kiwango kikubwa kuhakikisha kwamba mumewe anaifanya kazi yake vizuri.

Awali, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliwasihi waombolezaji wote wamkumbuke katika sala zao Prof. Kilangi ambaye ana kazi nzito ya kuishauri Serikali na alimtaja kuwa ni kiungo muhimu cha mihimili yote mitatu.

Naye, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza, Renatus Nkwande, alimuomba Profesa Kilangi na familia yake wajipe moyo kwa sababu binadamu anapokuwa hai au anapokufa bado anabaki kuwa mali ya Mwenyezi Mungu.


**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA ANDAN GROUP COMPANY LIMITED,**

Kwa niaba ya **AccessBank Tanzania Limited** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali lifuatalo:

| NAMBA | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MMILIKI DHAMANA | AINA YA DHAMANA | AUCTION COMPANY | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | PAMBA | SHABANI/M,JOHN | MAHOBONYA/SHABANI ,DAKOO | NYUMBA | BOSTON AUCTION MART | BUKABILE-SIMIYU | 21/08/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |
| 2. | PAMBA | SEGESE/Z,PETER | PETER Z. SEGESE | NYUMBA | BOSTON AUCTION MART | KAHANGARA-MWANZA | 22/08/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |
| 3. | PAMBA | NG'WANG'U/K ,DOTTO | DOTTO K. NG'WANG'U | NYUMBA | JOSINA AUCTION MART | MWANCHIMWA-MWANZA | 22/08/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |
| 4. | PAMBA | WANYAMA/M, WANYAMA | WANYAMA MASHEHE WANYAMA | GARI T.728 CPG | JOSINA AUCTION MART | NYAMBITI | 23/08/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |
| 5. | PAMBA | MWAKABONA/E,DEBORA | DEBORA BEN MWAKABONA | KIWANJA | JOSINA AUCTION MART | LUMALA/ MASHARIKI-MWANZA | 23/08/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |
| 6. | PAMBA | RWEGAYULA/E,ROSE | ROSE E. RWEGAYULA | NYUMBA | JOSINA AUCTION MART | ILEMELA-MWANZA | 26/09/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |
| 7. | PAMBA | GILIGWA/I,GERARD | GILIGWA/I,GERARD | NYUMBA | JOSINA AUCTION MART | ILEMELA-MWANZA | 26/09/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |
| 8. | PAMBA | AUGUSTINE/MAJALWA,LEONIDAS | AUGUSTINE/MAJALWA,LEONIDAS | ALTERNAIVE MORTIGAGE | BOSTON AUCTION MART | MAGU | 23/08/2019 | SAA 4 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

**Dhamana zitauzwa mahali zilipo**

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (nyundo itakaposhushwa), salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.

i. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

ii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

Kwa mawasiliano:
Mratibu wa MIKOPO AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu
Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340
Barua pepe: info@accessbank.co.tz
Simu ya Dalali husika: +255768203040 JOSINA AUCTION MART
+255766547732 BOSTON AUCTION MART

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

21536302

HABARI KITAIFA

# Nyumba 56 kupigwa mnada

INATOKA UK. 4

kipindi cha siku ya 14 toka tarehe ya mnada," lilieleza.

Hatua hii ni mwendelezo wa kasi ya mabenki nchini kuuza nyumba na mali nyingine za wateja wanaoshindwa kurejesha mikopo zikiwamo mashamba, magari na viwanja.

Hata hivyo, mamlaka za serikali zimeshatoa angalizo kwa benki na madalali wao kwa kupanga njama huku kuziuza kwa mnada mali zilizowekwa kama dhamana za wanaokwama kurejesha mikopo.

Mara kwa mara, Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amekuwa akiwaonya madalali wanaokula njama na mabenki ili kuuza mali za wakopaji wanyonge kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, mwaka 2016 alipokea malalamiki zaidi ya 80 ya kesi za watu walioonewa na madalali hao na kati ya kesi hizo zaidi ya asilimia 75 ni wanawake.

"Mnakwenda siku ya Jumamosi Sinza mnanadi nyumba kwa Sh. milioni 4 , haiwezekani unauza nyumba chini ya asilimia 25 ya thamani. Ninayo majina ya madalali nitawafuta na kuwatangaza. Fanyeni hii kazi kwa sura ya ubinadamu, leo ya wenzenu maskini kesho ni nyie," alisema.

Waziri huyo alisema baadhi ya watumishi wa benki wanashirikiana na madalali wanawatafauta wanunuzi kwa kisingizio wanataka kulipa mikopo yao huu ni uongo.

Aidha, Waziri huyo aliweka masharti kwamba bei wanayotaka kuuzia nyumba husika mthamini lazima ajue, hatua zilizofikiwa hadi kuuza nyumba ziandikwe na ziwe wazi ili kujua thamani halisi ya nyumba husika kulingana na bei ya soko.

Alisema mthamini wa ardhi atafuatilia kujua bei iliyouzwa kama ndiyo bei ya soko na kama haki imetendeka kabla ya kuhamisha umiliki wa nyumba.

Hivi karibuni, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ilisema kuwa benki zinazouza nyumba za wateja ovyo zinaandaliwa kibano cha kuzidhibiti.

Ofisa wa Dawati la Malalamiko ya wateja wa huduma za Kibenki wa BOT, Ramadhani Myonga, alisema kibano hicho kitaanza hivi karibuni baada ya kumalizika kwa uandaaji wa kanuni za sheria ya sheria ndogondogo za fedha ya mwaka 2018 na kuanza kutumika.

Myonga alisema wamebaini kwamba benki nyingi zimekuwa zikiweka masharti magumu ambayo siyo rafiki kwa wakopaji ambayo pia hayampi ahueni mkopaji kuongeza muda mkopaji huyo kulipa mkopo wake pale anapopata mtikisiko kiuchumi.

Pia alisema wamebaini kwamba baadhi ya benki hizo zimekuwa zikiweka masharti hayo magumu ili kutengeneza mazingira ya mteja kushindwa kulipa deni kwa wakati na hivyo mali zake kupigwa mnada.

Alitoa mfano kuwa unaweza kukuta mteja anayekopa anaambiwa atarejesha kiasi fulani cha fedha kumbe, wakati huo huo rejesho lake halijajumuishwa na fidia ya mkopo wa mwezi, na kwamba mteja anapaswa ajue hata na sehemu ya marejesho, lakini hata zile nyaraka za mikopo yao huwa hawapewi.

Alisema sehemu nyingine ya matatizo ya mikopo ni pale mteja anapotaka kuhama kutoka benki moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta ahueni ya mkopo wake

Kwamba inafika mahalia mkopaji akitaka kuhamia katika benki nyingine kwa ajili ya kutafuta ahueni ya mkopo wake, benki husika ambayo amekopa humuwekea masharti magumu ilimradi tu ashindwe na mwisho wa siku ndiyo kutengeneza mazingira ya kukimbilia kupiga mnada mali zake.

"Mabenki mengi hayatoi fursa kwa wakopaji kurestructure mikopo yao baada ya kuyumba kiuchumi, badala yake yanakimbilia kupiga mnada mali na hiyo pia inachangia na namna ambavyo mikataba imeandikwa, haitoi fursa hiyo," alisema.

Alisema tatizo jingine linalochangia migogoro ya mikopo ni wakopaji wenyewe kukimbilia kusaini mikataba ya mikopo yao bila kusoma vilivyoandikwa katika mikataba hiyo, hivyo mwisho wa siku kujikuta wanaingia katika matatizo hususan wanapobaini kwamba walichokisaini hawawezi kukitelekeza

Tatizo jingine ambalo alisema linachangia migogoro ya mikopo katika mabenki mengi ni lugha inayotumika katika kuandika mikataba ya mikopo, kutokuwa na elimu ya mikopo kwa wakopaji na maandishi madogo yanayoandikwa katika mikataba hiyo

"Kwa hiyo BOT imetengeneza sheria mpya ya 2018 ambayo inasubiri kanuni ambazo wakati wowote zitakamilika na kuanza kufanya kazi, hizi zitakuwa suluhisho la kumlinda mteja na huduma za kibenki," alisema Myonga

Alisema pia itatoa fursa kwa mkopaji kuwa na nafasi ya kujiridhisha na kile kilichoandikwa kwenye mkataba wa mkopo kwa muda wa saa 24 hadi siku tatu na kufanya uamuzi wa kukubali au kukataa

"Pia kutakuwa na mfumo wa kurestructure mkopo kwa ajili ya kumsaidia mkopaji anapopata mtikisiko wa kiuchumi," alisema

Pia alisema sheria hiyo itatoa fursa kwa BoT kutembelea taasisi za fedha kuangalia au kukagua na kujiridhisha kama zinatekeleza kanuni za kuwalinda wateja na muongozo wa BOT.

Baada ya kauli ya BoT, Umoja wa Mabenki nchini ulisema umepokea jambo hilo kwa kuwa utakwenda kusaidia pande zote.






## Mahakama sasa yakubali kuchukua kielelezo cha Aveva

INATOKA UK. 4

ya ofisi.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016 jijini Dar es Salaam, Aveva na Kaburu, walifanya matumizi mabaya ya madaraka kwa kuandaa hati ya kuhamisha Dola za Marekani 300,000 kutoka akaunti ya Klabu ya Simba benki ya CRDB tawi la Azikiwe kwenda akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays, tawi la Uhio.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa shtaka la tatu, Machi 15, mwaka 2016 Aveva na Kaburu, wote kwa pamoja walighushi fomu ya kuhamisha fedha ya tarehe hiyo wakionyesha kwamba Klabu ya Simba inalipa deni la Dola za Marekani 300,000 kwa Rais wake Aveva.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa Machi 15, mwaka 2016 katika benki ya CRDB, tawi la Azikiwe lililopo Ilala, jijini Dar es Salaam, Aveva aliwasilisha fomu ya kuhamisha fedha zilizoghushiwa ya terehe hiyo akionyesha kwamba Klabu ya Simba imeomba kuhamisha Dola za Marekani 300,000 huku akijua sio kweli.

Katika shtaka la tano, ilidaiwa kuwa kati ya Machi 10, 2016 jijini Dar es Salaam, Aveva alijilipa na kutakatisha Dola za Marekani 187,817 kutoka benki ya Barclays tawi la Uhio, huku akijua zimetokana na kughushi.

Kimaro alidai katika shtaka la sita, kati ya Machi 10 na 16, 2016 Kaburu alitakatisha fedha baada mshtakiwa huyo wa pili kumsaidia Aveva kupata Dola za Marekani 187,817.

Katika shtaka la saba, kati ya Machi 10 na Mei 30, 2016, jijini Dar es Salaam, Aveva, Kaburu na Zakaria Hans Poppe, walighushi hati ya malipo wakidai wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577, huku wakijua si kweli.

## TBS yaandaa kanuni mpya

INATOKA UK. 4

kufanya hivyo ili kutokwamisha shughuli za serikali.

"Hakuna kilichosimama, bali kanuni za TBS ndiyo zinafanyiwa kazi kwa wakati huu ambao tuko katika mpito, tunatumia zile za TFDA," Roida alisema.

Roida alibainisha kuwa wameomba kibali serikalini kuwachukua baadhi ya watumishi waliokuwa wa TFDA wakishughulikia masuala ya chakula na vipodozi kwenda kuongeza nguvu ya utendaji kazi.

Juni 26, mwaka huu, serikali ilipendekeza kwa Bunge kufanya marekebisho ya Sheria ya Viwango Sura 130 ili kuhamishia majukumu ya kusimamia masuala ya chakula na vipodozi kwa TBS kutoka TFDA.

Kutokana na kubadilishwa kwa majukumu hayo, ilipendekezwa kuwa badala ya kuitwa TFDA, iitwe Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Kufuatia pendekezo hili, TBS itachukua jukumu la kuunganisha utaratibu wa usajili wa majengo, bidhaa, udhibiti wa bidhaa na udhibiti wa bidhaa kutoka nje.

Mapendekezo hayo ndiyo yalisababisha kurekebishwa kwa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura ya 219 ili kuiondolea TFDA jukumu la kusimamia chakula na vipodozi.

HABARI KITAIFA

# EPZA yawataka Watanzania kuchangamkia fursa za SADC

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji Nchini (EPZA) imesema Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) inazo fursa za uwekezaji na soko kubwa ambavyo kwa pamoja ni vitu muhimu katika maendeleo ya viwanda na juhudi za kuondoa umaskini.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Kanali mstaafu Joseph Simbakalia, wakati akiwasilisha mada katika Maonyesho ya Nne ya Viwanda ya SADC yanayofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

"SADC imejaa fursa lukuki za uwekezaji zikiambatana na mtaji mkubwa wenye nguvu kazi ya vijana ambayo ni nguzo muhimu sana katika ujenzi wa uchumi wa viwanda," alisema.

Maonyesho ya Nne ya SADC ya Viwanda yalifunguliwa rasmi Jumatatu na Rais John Magufuli ambaye katika kilele ya mkutano wa jumuiya ya SADC atachukua kiti cha uenyekiti.

Aliongeza kusema kuwa vijana katika eneo la SADC ni vema wakapewa maelekezo sahihi ili waweze kuwa madhubuti katika kushiriki kwenye maendeleo ya nchi zao na eneo lote la SADC badala ya kujiingiza katika siasa za vurugu.

Alisema uimara na uthabiti wa kisiasa ni nguzo muhimu sana katika kujenga kujiamini na kuvutia uwekezaji wa miradi ya muda mfupi na muda mrefu ambayo ni muhimu sana katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alisema eneo la SADC lipo thabiti na imara kisiasa iliyojengwa wakati wa juhudi za ukombozi na kupigania uhuru wa nchi hizi.

"Hali hii imejenga umoja na ushirikiano katika nchi hizi ikiwa ni kigezo muhimu sana katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

"Jumuiya ya SADC imetengeneza mpango mkakati wa maendeleo wenye lengo la kusukuma mbele maendeleo ya viwanda ili yaweze kuchangia zaidi katika ujenzi wa uchumi wa nchi hizi," alisema Simbakalia.

Aliongeza kuwa SADC inatakiwa itumie fursa ya uhusiano na China katika kujenga mikakati imara zaidi yenye lengo la kuleta maendeleo endelevu katika ukanda huu. Alisema ni vema SADC kuelekeza nguvu katika uzalishaji wa bidhaa mpya na mitambo inayotumika sehemu mbalimbali za uzalishaji kwa kutumia aina mbalimbali za madini yanayopatikana katika nchi hizi.



Mkuu wa Mauzo wa Tigo, Kadambara Maita, akimkaribisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika banda la Tigo, lililopo katika Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) unaoendelea jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji kuchanja ng'ombe dhidi ugonjwa wa mapafu

**Na Edward Kondela**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imewataka wafugaji kuchanja ng'ombe wao dhidi ya ugonjwa wa mapafu ya ng'ombe (CBPP) ambao husababisha vifo.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambaye pia ni Mganga Mkuu wa Mifugo nchini, Dk. Hezron Nonga, akizungumza katika Maonyesho ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi (Nanenane), kwenye viwanja vya Nyakabindi katika Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, alisema chanjo hiyo iliyoanza kutumika nchini Julai, mwaka huu inapatikana kwa Sh. 200 hadi 250 pekee.

"Ugonjwa wa mapafu ya ng'ombe unasababisha kifo usipomkinga ng'ombe wako kwa kutumia chanjo hii utaingia gharama kubwa kwa kuwa ng'ombe huyo atakufa pia utatumia gharama kubwa kuwalinda ng'ombe wengine ulionao," alisema Dk. Nonga.

Akizungumzia chanjo hiyo, Dk. Nonga, alisema, tayari ipo sokoni nchi nzima na kwamba vipo vituo 11 kila kanda na kuwataka wafugaji kuhakikisha ng'ombe wanachanjwa dhidi ya ugonjwa huo.

Vile vile, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Kituo cha Kuzalisha Chanjo Kibaha (TVI) kilichopo mkoani Pwani inatarajia katika kipindi cha mwaka mmoja hadi miwili kuanza kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa ambazo kwa sasa zinanunuliwa kutoka nchi za nje.

Kutokana na watu wengi kuwa na utaratibu wa kumiliki mbwa katika makazi yao katika kipindi cha siku za hivi karibuni, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Nonga, aliwataka watu wanaomiliki mbwa kuhakikisha wanyama hao wanachanjwa kwa kuwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa hauna tiba endapo binadamu atang'atwa.

Alifafanua kuwa kwa kawaida chanjo hiyo hupatiwa mbwa mara moja kwa mwaka na kwa sasa inapatikana kwa Sh. 1,000 pekee ili kuhakikisha wamiliki wa mbwa na wananchi wanakuwa salama.

# Maelfu vijiji viwili wakosa majisafi

**Na Daniel Limbe,** KYERWA

WAKAZI zaidi ya 6,400 wa vitongoji saba na vijiji viwili vya Kibimba na Makazi wilayani Kyerwa mkoani Kagera hawana huduma ya majisafi na salama.

Hali hiyo imesababisha wananchi hao kutumia maji yasiyo salama kwa afya ya binadamu ambayo hupatikana kwenye chanzo cha Tungula katika Kitongoji cha Kibimba 'B', huku wakichangia na mifugo.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kibimba 'B', Thobias Theobard, ameliambia Nipashe kuwa wananchi wake wanalazimika kutumia maji hayo kutokana na kukosekana huduma mbadala ya majisafi na salama, na kwamba wanalazimika kutumia chanzo hicho hasa kipindi cha kiangazi.

Licha ya kwamba maji hayo hayafai kwa afya za binadamu, bado hutumika kupikia, kufua, kunywa na kufulia nguo.

Gazeti hili likiwa katika eneo la tukio lilizungumza na Mwenyekiti wa kijiji hicho, Ibrahimu Paschala ambaye alisema kuwa chanzo hicho cha maji kinatumiwa na vijiji viwili, na kwamba kinapokauka hasa kipindi cha kiangazi wananchi hulazimika kutembea umbali wa kilomita 11 kutafuta huduma hiyo kwenye kijiji jirani cha Mabila Chemigela.

Kutokana na hali hiyo, Shirika lisilo la Kiserikali la Kuhudumia Wakulima wilayani Karagwe na Kyerwa la Mavuno, limeamua kupanda miti zaidi ya 3,000 kwenye chanzo hicho cha maji ili kunusuru kukauka kutokana na uharibifu wa mazingira.

Mkurugenzi wa Shirika la Mavuno, Charles Bahati, alisema shirika hilo kwa kushirikiana na wananchi wa kijiji cha Kibimba, wameamua kuendelea kukitunza chanzo hicho cha maji kwa kupanda miti ili kukinusuru, kwa kuwa bado ndiyo chanzo pekee kinachotegemewa na wananchi zaidi ya 6,400.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Denis Ndagara, amekiri wananchi hao kutumia maji yasiyofaa kwa matumizi ya binadamu, na kwamba baadhi ya wananchi wasiotambua umuhimu wa kutunza mazingira wamekuwa wakichafua kwa kujisaidia ovyo, hali inayosababisha wananchi kuugua magonjwa ya kuhara.

## Wanahabari wasaidia shule

**Gideon Mwakanosya,** SONGEA.

UMOJA wa Vilabu vya Habari Tanzania [UTPC], umetoa msaada wa mifuko 20 ya saruji yenye thamani ya Sh, 380,000 kwaajili ya kusaidia ujenzi wa shule ya msingi ya Ulamboni katika Kata ya Kizuka na shule ya Sekondari ya Kata ya Litapwasi zilizopo katika Halmashuri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Akikabidhi saruji hiyo jana mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari mkoani Ruvuma, Thomas Makwaya, kwa niaba ya Mkurugenzi wa UTPC, Abubakar Karsan, alisema saruji hiyo imetolewa msaada kwenye shule hizo ili kusaidia ujenzi wa madarasa unaoendelea kwenye shule hizo .

Makwaya alisema msaada huo uliotolewa na UTPC ni kutokana na uongozi wa muungano huo kufanya ziara ya siku tatu mkoani Ruvuma ambapo katika ziara hiyo walitembelea maeneo mbalimbali yakiwamo Shule ya Msingi ya Ulamboni pamoja na kijiji cha Lyangweni Kata ya Litapwasi chenye shule ya sekondari ya kata.

Mratibu huyo alisema uongozi wa UTPC ulioongonzwa na Karsan walipokuwa katika maeneo hayo na kutambua shughuli zinazofanywa na wakazi wa vijiji hivyo, ikiwamo jitihada za kuboresha shule hizo kwa kujenga madarasa, waliamua nao kuchangia ujenzi huo kwa msaada wa mifuko 20 ya saruji.

Kwa upande wake Afisa manunuzi wa Halmashauri ya Songea, Noel Lyanga akipokea saruji hiyo, alisema uongozi wa Halmashuri hiyo unaushukuru uongozi wa UTPC kwa msaada huo ambao utasaidia kuleta chachu kwa wananchi na wadau mbalimbali kuona umuhimu wa kujitolea katika suala la maendeleo.

"Kitendo hiki kilichofanywa na UTPC kimetufanya tufumbue macho, kutambua kuwa kumbe kazi za maendeleo zinafanywa na wanachi zimekuwa zikitambuliwa na taasisi mbalimbali zikiwamo za waandishi wa habari," alisema Lyanga.



Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Magharabi, Sospeter Magesse, akimkabidhi tikitimaji, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) kitaifa mkoani Simiyu. NMB ni wadhamini wa maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waeleza fedha za ruzuku ya Tasaf zilivyowaendeleza

**Na Restuta Damian,** MULEBA

BAADHI ya wananchi walioopo katika mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF lll) katika vijiji vya Kyamyorwa Kata ya Kasharunga na Kyamunyagi Kata ya Magata wilayani Muleba mkoani Kagera, wameeleza jinsi walivyoweza kuendeleza elimu ya watoto wao pamoja na kuwa na makazi bora. Wamesema kuwa wamepata mafanikio hayo kutokana na kuwahishiwa fedha za ruzuku kutoka serikalini.

Wameeleza kuwa mpango huo umesaidia kubadili maisha ya familia na kaya zao kwa kutumia vizuri maelekezo yaliyokuwq yakitolewa na wataalamu baada ya kupokea fedha zinazotolewa na serikali yenye lengo la kubadili maisha ya wananchi wasiojiweza katika kimapato. Rosemary Peter, alisema mafanikio aliyonayo kwa muda wa miaka mitatu sasa ni kutokana na fedha za ruzuku ya Tasaf lll alizopata, hivyo kumsaidia kusomesha mtoto hadi kufikia taaluma ya udaktari wa binadamu.

Alisema baada ya kuingia katika mpango huo, alianzisha ufugaji wa kuku na kilimo cha mboga kwa kufanya ujasiriamali, na kumwezesha kuongezea fedha anayoipata kiasi cha Sh. 40,000 kuongeza malipo ya mwanafunzi. "Baada ya kupata fedha niliona kama haitoshi mimi na familia ya watoto sita nikaanzisha ufugaji na kulima bustani," alisema na kuongeza: "Kile nilichopata nilipeleka magulioni nia yangu nipate pesa zaidi kupitia ninayopewa na serikali, na nyingine natumia kwa matumizi ya familia."

Alisema awali aliishi katika mazingira magumu kutokana na kukosa chakula cha uhakika pamoja na makazi duni, na kuwa alikuwa na nyumba ya majani.

Nadhali Ramadhan, mnufaika kutoka Kijiji cha Ktamunyangi Kata ya Magata, alisema kwa kipindo kirefu aliishi kwenye familia ya mzee wake, huku akitegenea ardhi na chakula kutokana na kulima vibarua vya malipo na kupewa chakula. Alisema baada ya kuingizwa katika mpango wa kaya maskini, alipata nuru iliyomvusha kutoka hali duni na kuanza kutumia fedha kwa kuwekeza kwenye kilimo cha mazao ya muda mfupi na ufugaji. "Nilipoingia tu katika mpango huu niliona nuru kubwa imeingia ndani ya familia, nilianza kulima matunda kwani fedha niliyopata nilinunulia mbegu na mbolea ya kukuzia nyingine nikaanza ufugaji wa kuku, bata na mbuzi kama akiba ya elimu kwa watoto wangu," alielezea Ramadhan.

Mtendaji wa Kijiji Kyamworwa, Mariam Kibelenge, alisema tangu mradi huo uingie kijijini hapo wenye wakazi 7,222, wanaume 4782 na wanawake2440, huku nguvu kazi ikiwa 3,482.

Alisema kuwa, walengwa walioopo katika mpango ni 201 kiasi kilichotolewa kwa sehemu ya kwanza ni zaidi ya Sh. milioni 164 ambacho kiliwanufaisha kuwa na elimu, mahudhurio ya kliniki, kilimo, na ufugaji.

"Manufaa ya mradi huo kwa walengwa waliweza kuwa na makazi ambapo nyumba 56 zilijengwa, ufugaji wa kuku 76 mbuzi 25 hiyo ni jumla ya kijiji kizima kilivyoonyesha nia na mafanikio," alisema Kibelenge.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, alisema lengo la serikali ni kupata matokeo chanya katika mpango wa Tasaf kwa kuona mafanikio.

Dk. Mwanjelwa alisema kwa kuona juhudi na kiu ya kuwa na uwezo wa kuishi maisha yenye kujihudumia, kaya hizo zitakuwa mabalozi wa kusaidia wengine ambao waingizwa sehemu ya pili waweze kupata mahitaji na kuboresha maisha yao.

# Waziri awataka wafugaji, wavuvi kujiunga NSSF

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAFUGAJI na wavuvi Kanda ya Kusini inayounganisha mikoa ya Lindi na Mtwara, wamesisitizwa kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii {NSSF} kwa kuwa ni miongoni mwa wadau wakubwa kwenye sekta ya isiyo rasmi.

Msisitizo huo umetolewa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alipokuwa akizungumza na wanahabari kwenye viwanja vya Maonyesho ya Wakulima Nanenane Kanda ya Kusini katika Manispaa ya Lindi.

Naibu Ulega alisema kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii mwaka 2018, NSSF ndiyo iliyopewa jukumu la kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na ile isiyo rasmi wakiwamo wafugaji na wavuvi, hivyo wanao wajibu wa kutumia fursa hiyo kujiandikisha.

Ulega alisema idadi kubwa ya wadau wake wapo wafugaji na wavuvi, wakiwamo wadogo.

Ulega alisema wavuvi, wafugaji na wananchi wengine watakapojiunga na mfuko huo, watanufaika na huduma mbalimbali, ikiwamo mafao ya uzeeni, matibabu pamoja na mikopo itakayowawezesha kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali.

Alisema wafugaji na wavuvi wamepata mahali salama pa hifadhi kwa watakaojiunga na NSSF. Naye Meneja wa NSSF mkoani Lindi, Robert Cosmas, akipokea maelekezo hayo, alimhakikishia Ulega kuwa wamejipanga vizuri kuhakikisha wananchi wote walioopo sekta binafsi na zile zisizo rasmi wanasajiliwa ili kunufaika na mafao yanayotolewa na mfuko huo.

# Serikali yaonya mangariba Simanjiro

**Novatus Makunga,**
SIMANJIRO

SERIKALI imewataka mangariba wanaofanya shughuli ya ukeketaji wa watoto wa kike wilayani Simanjiro mkoani Manyara, kuacha mara moja shughuli hiyo kwa kuwa ni haramu na badala yake wajitumbukize katika ujasiriamali.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula, wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Loswaki, kilichopo katika Kata ya Terrat wilayani humo.

Mhandisi Chaula alisema ukeketaji ni biashara haramu ambayo haitakiwi katika wilaya hiyo na kuwataka mangariba kujitumbukiza katika shughuli nyingine za ujasiriamali.

Alisema kuwa mikakati ya kuwasaidia kujiingiza katika ujasiriamali imeanza na mwezi uliopita, shirika lisilokuwa la kiserikali la Nafgem limewapatia mashine ya kukoboa nafaka, waliokuwa mangariba.

Mhandisi Chaula alisema pia kuna fursa ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, kupitia fedha asilimia kumi zinazotengwa kutoka mapato ya ndani ya halmashauri hiyo kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Alisema mwezi uliopita walitoa mikopo ya jumla ya Sh. milioni 230 kwa vikundi cha ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Ni mpango wa Rais John Magufuli wa kuwasaidia wanyonge kwa kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba, hivyo ni vyema kinamama wakachangamkia fursa hiyo ya kujikwamua kiuchumi," alisema.

Aliwahakikishia wananchi wa kijiji hicho na vijiji vingine vya Kata ya Terrat kwamba watapata umeme kabla ya kufikia mwaka 2021.

Alisema mpaka sasa hivi katika wilaya hiyo vijiji 31 vimeshapata umeme kati ya vyote 57 na kazi ya usambazaji inaendelea kupitia mradi wa umeme vijijini (Rea).

"Serikali inasambaza umeme kwa gharama nafuu ya Sh. 27,000 hivyo msiwe na wasiwasi, ninachowasihi msikubali kurubuniwa na kuwatumia vishoka, nendeni ofisi ya Tanesco mtahudumiwa vizuri," alisema.

Pia mkuu huyo wa wilaya aliwaahidi wananchi hao kwamba wilaya hiyo ipo katika mpango wa kukarabati barabara zilizoharibiwa na mvua za masika na kuwataka kuvuta subira.

Alisema katika vikao mbalimbali vya mkoa walishauri bajeti ya Wakala wa Usimamizi wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura) kuongezwa kutoka asilimia 30 ya sasa huku Tanroads wakitengewa asilimia 70.

Katika hatua nyingine Mhandisi Chaula alipiga marufuku uchezaji wa michezo mbalimbali wakati wa kazi ikiwamo ya kubahatisha pamoja na pool table.

Aliwaagiza viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya vijiji mpaka katika halmashauri ya wilaya kushirikiana na vyombo vya usalama kudhibiti michezo hiyo na kuhakikisha kila mtu hususani vijana wanafanyakazi.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Terrat, Jackson Materi, alimwomba mkuu huyo wa wilaya kusukuma utekelezaji wa ukarabati wa barabara zinazohudumia vijiji vya kata hiyo kwa kuwa Julai 20, walikuwa na mkutano na maofisa wa Tarura.

Vile vile, Diwani Materi alizungumzia suala la usambazaji umeme na kusema kasi imekuwa ndogo pamoja na kwamba nguzo zimeshafika jirani katika kijiji cha Losinyai.



Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Chelestino Mofuga (katikati), akiwa na viongozi wengine waliotembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika eneo la Tropiki (TPRI) kwenye maonyesho ya Nanenane Kanda ya Kaskazini jijini Arusha, wakimsikiliza Ofisa Mwandamizi wa taasisi hiyo, Justine Ringo, akielezea njia sahihi ya unyunyiziaji viuatilifu jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi wahimizwa kufuga samaki

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SERIKALI imewaomba wananchi nchini waanze ufugaji wa mazao ya samaki kutokana na uhitaji mkubwa nchini na duniani.

Hayo yameelezwa jijini hapa na Mtaalamu wa Mifugo na Uvuvi wa wizara hiyo, Fredrick Francesis, katika viwanja vya Themi, jijini Arusha wakati wa maonyesho ya Wakulima (Nanenane) kwa Kanda ya Kaskazini.

Alisema hadi sasa Tanzania ipo asilimia 50 kati ya 100 katika kufikia lengo la ufugaji samaki na mazao yake ambayo yana faida kubwa kiafya na biashara.

Fredrick alisema serikali imekuwa ikipokea maombi mengi kutoka nchi mbalimbali duniani ya mazao ya uvuvi, hasa vyakula vinavyotokana na mazao ya bahari.

"Lakini hatujaweza kukidhi maombi hayo kutokana na kiwango chetu cha uzalishaji ni kidogo kuliko mahitaji na hivyo nawaomba Watanzania kuchangamkia fursa hiyo," alisema.

Alisema mazao ya uvuvi yana soko kubwa duniani kuliko biashara nyingine ambazo baadhi ya watu wanalazimisha kufanya, japokuwa ni haramu na kosa kwa mujibu wa sheria za nchi, hivyo hawana budi kugeukia kuzalisha kwa wingi ili kwenda sambamba na ukubwa wa soko.

Kwa mujibu wa Fredrick, kwa kuzingatia ukweli huo, wananchi wanatakiwa kupata elimu ya ufugaji wa mazao hayo, itakayowasaidia waweze kujikwamua kiuchumi na wachangie pato la taifa kupitia katika sekta ya uvuvi.

"Watu wanalalamika umaskini, lakini kuna fursa nyingi, sisi watumishi wa serikali tunawajibu wa kuwaonyesha wananchi fursa hizo, ikiwamo hii ya mazao ya samaki kuwa ya biashara kubwa duniani," alisema Ulega.

Pia mtaalamu huyo wa wizara yenye dhamana ya uvuvi na mifugo alisisitiza kwamba mkakati wa serikali ni kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa viwanda ili kufikia mkakati huo malighafi zinahitajika, hususani katika viwanda vya kuchakata mazao hayo.

Naye Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Mwanga, alisema baada ya kufanikiwa kutokomeza tatizo la uvuvi haramu kwa asilimia 90, kwa hivi sasa ni muda wa kusimamia utoaji elimu kwa wananchi kuhusu ufugaji Ili wananchi watumie fursa hiyo.

Alisema, uvuvi haramu unaharibu mazingira ya mazalia ya samaki hivyo kuwaomba wafanyabiashara nchini kuona umuhimu wa kushirikiana kuondoa tatizo la uvuvi haramu kwa kutonunua samaki ambao hawapo kisheria.

# Wafugaji walalamikia umbali mrefu kufuata maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAFUGAJI wa Kijiji cha Irkujit, Kata ya Edonyongijape wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wamelalamikia changamoto ya ukosefu wa maji kwa kuwa inawalazimu kutembelea umbali wa kilomita 30 kwenda Orkesumet kufuata maji na kurudi nyumbani.

Wakizungumza juzi wafugaji hao walidai kuwa inawawia vigumu kufanya shughuli mbalimbali za kijamii na za maendeleo kutokana na ukosefu wa huduma ya maji kwenye eneo la karibu.

Mmoja kati ya wafugaji hao, Parasoi Kurdun, alisema suala la maji limekuwa tatizo kubwa kwao hasa wakati huu wa kiangazi kwa kuwa mifugo na wanyama wanapata shida mno.

"Tunaiomba serikali iangalie suala hili kwa jicho la huruma haiwezekani sisi tulie juu ya maji na kusababisha mifugo na jamii kwa ujumla iteseke kwa muda mrefu," alisema Kurdun.

Mfugaji Yohana Ngalai, alisema japokuwa hivi sasa nguzo za umeme zinasimikwa kwenye kijiji chao ili wapatiwe nishati ya umeme, lakini suala la maji bado ni changamoto kubwa kwao.

"Sera ya maji na ilani ya uchaguzi wa CCM imeelezea kuwa lengo ni kumtua mama ndoo kichwani na umbali wa kuchota maji isiwe zaidi ya mita 200 au 400, lakini sasa inakuwa tofauti kwetu, tunatembea zaidi ya kilomita 30 kwenda na kurudi," alisema Ngalai.

Rehema Kivai, alisema watoto na wanawake ndiyo huteseka zaidi kwa kuwa hutumia punda kufuata huduma ya maji kwenye mji mdogo wa Orkesumet na sasa hivi kuna ukame.

"Tuna wakati mgumu sana, tunakabiliwa na changamoto kubwa mno ukiwa na maji kidogo unachagua uoge, unywe, ufue, uwape mifugo, upikie chakula au umwagilie mti," alisema Kivai.

Hata hivyo, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James Ole Millya, alisema kero hiyo ya maji itafikia ukingoni wakati wowote mradi mkubwa wa maji wa Mto Ruvu upo mbioni kukamilika.

Ole Millya, alisema mradi huo wa maji unaotoka katika kata ya Ruvu Remit hadi mji mdogo wa Orkesumet ukikamilika Mei mwakani kata jirani za Edonyongijape na Langai nazo zitanufaika.

Alisema wanamshukuru Rais John Magufuli kwa kufanikisha mradi huo mkubwa wa maji ambao utakuwa faida kwao wafugaji na vizazi vijavyo.

Alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 41.5 pindi ukikamilishwa na kuwa suluhisho la tatizo la maji kwa mifugo na binadamu.

## Mbatia aomba barabara ya lami Kiborloni

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MBUNGE wa Vunjo (NCCR-Mageuzi) na Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), James Mbatia, amemwomba Rais John Magufuli kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kiborloni/ Kidia hadi Hospitali ya Mtakatifu Monica yenye urefu wa kilomita 14.

Mbatia ameeleza kuwa iwapo serikali itaona umuhimu wa kuijenga barabara hiyo, itarahisisha ufikishwaji wa wagonjwa katika hospitali hiyo na kufungua fursa za utalii. Alikuwa akizungumza jana katika Kata ya Kirua Vunjo Magharibi, wakati wa hafla ya uzinduzi wa Hospitali ya Mtakatifu Monica, inayomilikiwa na Mfuko wa Kusaidia Watoto, Kata ya Kirua (KCCF). Alisema barabara hiyo ambayo kwa sasa imeishia katika eneo maarufu la Kwa Msaki, imeshajengwa kwa kilomita 2.5 pekee kati ya kilomita 14 zilizopo.

Kwa mujibu wa Mbatia, tayari ameshaijengea hoja kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Prof. Makame Mbarawa na serikali imewaahidi kuendelea kuijenga kadiri fedha inapopatikana.

"Tunaomba ikiipendeza serikali, iunganishe barabara hiyo hadi eneo la Maua ili iitwe barabara ya utalii, kwa kuwa itasaidia kupitisha watalii kwenda Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro kwa nyakati zote hasa za misimu ya mvua," alisema Mbatia.

Vile vile, alizishukuru taasisi za dini kwa kuwekeza huduma za afya katika jimbo hilo na kuwa kunarahisisha upatikanaji wa matibabu tofauti na ilivyokuwa kwa kutembea umbali mrefu hasa nyakati za mvua na usiku ikilinganishwa na mazingira ya milimani. "Maeneo ya huku ni milimani na iliwalazimu wananchi kutembea umbali mrefu hasa nyakati za usiku na za mvua hasa kinamama, watoto pamoja wazee mara wanapopewa rufani," alisema Mbatia.

Katika hatua nyingine, Mbunge huyo ameeleza kuwa Vunjo ndiyo jimbo pekee la uchaguzi mkoani Kilimanjaro ambalo linaongoza kwa kuwa na taasisi nyingi za elimu na afya.

"Maendeleo kama haya mnayoyaona hivi sasa hayana itikadi zozote zile tunatakiwa tuweke nguvu kwa pamoja ili tuhakikishe manufaa yanakuwapo katika jamii kutokana na uwekezaji wa namna hii ambao unasaidia watu wa kada zote zile," alisisitiza Mbatia. Awali, Mwenyekiti wa Mfuko wa Kusaidia Watoto wa Kata ya Kirua (KCCF), Padri Amedeus Macha, alisema kuwa hospitali hiyo iliyozinduliwa inalenga hasa kutoa matibabu kwa wazee na watoto waliokuwa wakitembea umbali kupata matibabu.

# Mweka yagundua nyuki mpya asiyepatikana nchi zingine

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WATAALAMU wa nyuki kutoka Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania (Mweka), wamedai kugundua aina mpya ya nyuki ambaye hapatikani mahali popote duniani, zaidi ya kuwapo katika ukanda wa Mlima Meru uliopo chini ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

Akizungumza jana na Nipashe kuhusu ugunduzi huo, mtaalamu wa nyuki kutoka Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania, Julius Laswai, alisema nyuki huyo ambaye amegunduliwa katika eneo hilo ana rangi ya bluu.

"Hata hivyo, kunahitajika jitihada zaidi za kumlinda asihame kwenda mbali, lakini pia kama taifa, hivi sasa Tanzania inapaswa kuhakikisha inakuwa na takwimu sahihi za nyuki waliopo, ingawa kuna taarifa kwamba wataalamu wanaendelea na kazi ya kupata takwimu sahihi," ameeleza mtaalamu huyo.

Kwa mujibu wa Laswai, kwa sasa nchi za Afrika Mashariki zinatajwa kuwa na aina za nyuki 1,200.

Pamoja na mambo mengine, mtaalamu huyo ametahadharisha kuwa kwa Tanzania, nyuki wachavushaji wako hatarini kupotea kutokana na kushamiri kwa tatizo la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

"Hali hiyo kama haitadhibitiwa haraka kwa mamlaka husika kuchukua hatua, kuna hatari ya kukumbwa na baa la njaa kutokana na umuhimu wa nyuki hao kwa wakulima," ameeleza Laswai.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wataalamu wa kilimo waliozungumza na Nipashe kuhusu hatari hiyo, akiwamo Lasioglosomu Merurupter, amewashauri wakulima wa Tanzania kuhakikisha wanazingatia kanuni bora za kilimo ili kuhakikisha mimea inakutana na nyuki wachavushaji.

Mabadiliko ya tabianchi, yanatajwa na wataalamu hao kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, jambo ambalo hu-



Huu ndio mwonekano wa baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam ambayo yanatumiwa na wafanyabiashara wadogo ambao bado hawajatengewa maeneo ya kufanyia shughuli zao kama hawa wa Mbezi Mwisho. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wafanyabiashara wafunguka uuzaji mazao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BAADHI ya wafanyabiashara wa mazao katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha wamefunguka kuhusu angalizo lililotolewa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, la kuwataka watendaji wa wizara yake pamoja na wakuu wa wilaya nchini kutowazuia wakulima kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi kwa kuhofia kutokea baa la njaa.

Kilimo ni njia kuu ya uchumi wa Tanzania, ikiajiri zaidi ya asilimia 70 ya wananchi.

Kwa nyakati tofauti jana, wafanyabiashara hao wakizungumza katika maonyesho ya Nanenane, wameeleza kuwa iko haja kwa serikali kusimamia maagizo hayo kutekelezwa kwa vitendo ili kumaliza sintofahamu inayojitokeza wakati mwingine.

Mfanyabiashara wa mahindi kutoka mkoani Kilimanjaro, Nicholaus Mashauri, alisema uamuzi wa serikali wa kuondoa zuio hilo la wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi ni la kiungwana na linalenga kuwasaidia wakulima na wafanyabiashara kunufaika na jasho lao.

"Wafanyabiashara walio wengi wa mazao hasa mahindi na maharage tunajua kero na changamoto tunazokutana nazo katika uendeshaji wa shughuli zetu zinavyovuruga uchumi wetu, lakini pia zuio hilo lilikuwa likisababisha serikali yetu ikose mapato yake yanayotokana na fedha za kigeni," alisema Gideria Samson, mfanyabiashara wa maharage.

Naye Fidelia Allan, mkazi wa Arusha na mfanyabiashara wa mazao alisema kuondolewa kwa kizuizi hicho kilichokuwa kimewekwa na serikali tangu Juni mwaka 2017, kunatoa fursa kwa soko na mapato kwa wakulima kuchanua na hivyo kuwawezesha kuchangia pato la taifa.

Juzi Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliwataka watendaji wa wizara yake pamoja na wakuu wa wilaya nchini kutowazuia wakulima kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi kwa kuhofia kutokea baa la njaa.

Bashe alitoa angalizo hilo, wakati akifungua maonyesho ya kilimo na sherehe za wakulima (Nanenane), Kanda ya Ziwa Magharibi ambayo inajumuisha mikoa ya Kagera, Geita na Mwanza.

Mwaka 2017, serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ilitangaza ingeyataifisha mahindi yote pamoja na malori yanayovusha chakula kwa njia ya magendo kwenda nje ya nchi.

Serikali iliweka mkazo zaidi kuhusu zuio hilo, ikisema mtu yeyote atakayekamatwa anasafirisha mahindi kwenda nje ya nchi, yatataifishwa na yatapelekwa kwenye ghala la taifa la chakula na gari litataifishwa na litaishia Jeshi Polisi.

# ama

ALHAMISI AGOSTI 8, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 18

## Mapinduzi kilimo yanavyoteketeza hali ya hewa duniani



Ukurasa 17

## Wajue wabunge wenye ulemavu walioweka rekodi



Ukurasa 14

## UN yalia kufikwa joto la kihistoria, watafiti watahadharisha balaa



# Ummy Mwalimu alipotoa darasa 'kila kitu' ndani ya unyonyeshaji

Ukurasa 19

# Maradhi ya figo kugundulika kupitia simu

**LONDON, Uingereza**

MAPINDUZI mapya ya teknolojia yanayobaini maradhi ya figo yanaelezwa kuleta mageuzi makubwa hospitalini, majibu ya vipimo yanapelekwa moja kwa moja katika simu za mkononi.

Ni hatua inayomwagiwa sifa na wengi kuokoa muda, ikizingatiwa sehemu kubwa ya watu wanasumbuliwa na maradhi hayo. Kila mwaka inasababisha vifo kwa wastani watu 100,000. Katika majaribio yaliyofanyika katika hospitali moja ya jijini hapa, kunatajwa mageuzi makubwa majibu kupatikana kwenye simu ndani ya dakika 14, kinyume na zamani ilivyochukua saa nyingi.

Mary Emerson, Muuguzi Mwandamizi katika hospitali iliyofanyiwa majaribio, katika maoni yake anakiri kushuhudia mageuzi makubwa ya nafuu ya kikazi.

Anafafanua: "Ni mageuzi makubwa unapata ishara kuhusu mgonjwa popote ulipo hospitalini. Huduma za afya zinahama na za muda sahihi. Hiki kifaa kinachonisaidia kuona majibu kwa muda sahihi niliko."

Mshauri wa Kitaalamu kuhusu masuala ya figo, Dk. Sally Hamour, kutoka hospitali husika ya Royal Free, anakitaja kifaa hicho kuwa na maana kubwa katika kuokoa afya ya wagonjwa.



Wagonjwa wa figo wakionyeshana majibu yao kwenye simu. **PICHA: MTANDAO.**

## MAZINGIRA

### JULAI YA KIPEKEE...

# UN yalia kufikwa joto la kihistoria, watafiti watahadharisha balaa laja

- Ulaya hakushikiki; Japan 5000 waenda hospitali
- India walia shida maji; Ubelgiji, Ujerumani...



Pilika ya Wajapani kutokana na adha ya joto, Julai mwaka jana. Mwaka huu mwezi huo baadhi ya watu walifikishwa kutibiwa hospitalini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI inatimia wiki moja sasa tangu kuanza mwezi mpya, watafiti wa masuala ya hali ya hewa na sayansi duniani, wamekuja na matokeo ya kipekee duniani kuhusu hali ya hewa isiyoridhisha.

Katika mtazamo wao wanautaja mwezi uliopita, Julai ndio ulikuwa na joto zaidi katika kipindi cha miaka 40 iliyopita.

Kwa kurejea takwimu ya siku 29, rekodi inaonyesha mwezi huo ulifikisha kiwango kinachopiku rekodi inayofanana na hiyo, mwaka 2016.

Watafiti kutoka Umoja wa Ulaya (EU), walidhihirisha hayo siku kadhaa zilizopita wakisema kuna viashiria vya joto kuongezeka kwa kiasi kikubwa duniani, katika rekodi inayobadilika katika namna tofauti.

> "Tunahitaji kwenda kwa kasi na kuweka sawa sera zetu, zinazotambulika bungeni kwamba hali ya hewa ni ya dharura kwetu.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, rekodi hizo zimethibitishwa na zingine kutoka vituo mbalimbali vya hali ya hewa duniani.

Wakati ikieleza joto hilo bado halijaonyesha uhusiano wa moja kwa moja na mabadiliko ya hali ya hewa duniani, bado ukweli unasimama kwamba joto la mwezi uliopita liko katika hatua mbaya.

Watafiti wananena kwamba, huenda mabadiliko hayo yana uhusiano na kiwango kikubwa cha gesi ya ukaa (carbon dioxide) inayotolewa, kutokana na ziada ya shughuli za kibinadamu imeongeza kwa ziada ya joto, iliyofikisha rekodi ya mwezi uliopita.

"Mwezi huu umekuwa na joto zaidi. Lakini kwangu mimi hiyo siyo hoja. Mtazamo mkuu kwangu si mwezi huu umekuwa na joto zaidi. Miezi yote kwa mwaka 2019 imekuwa na joto zaidi ikilinganishwa na miaka mingine," anasema mtaalamu, Dk. Freja Vamborg.

"Pia, mwenendo huu unaonekana hauna dalili za kukoma, vinginevyo tuchukue hatua fulani kusimamisha," anaongeza.

**TAHADHARI DUNIANI**

Wakati imekuwa utamaduni kila mwezi Julai kuwa na kiwango cha juu zaidi cha joto, lakini mwaka huu unaonekana kuwapo upekee wa joto hilo bara za Ulaya, Marekani na iliko Arctic.

Hapo kunatajwa nchi zilizoshuhudia nyuzi joto 40 katika mataifa ya Ubelgiji, Uholanzi na Ujerumani, ilhali Uingereza ilifikia nyuzi joto 38.7. Vyote ni ziada na joto lisilozoeleka.

Nchini Marekani kunaelezwa kwamba, mamilioni ya wakazi wao waliathirika mno, wakati katika jimbo la Alaska, mashamba yaliathirika, vivyo hivyo Kaskazini mwa nchini Russia.

Upande mwingine wa nchini India, joto jingi lilileta athari za kijamii, zinajumuisha shida ya maji; wakati nchini Japan kulikuwapo wastani wa watu 5,000 waliogua kutokana na athari za joto na wakalazimka kwende hospitali kusaka matibabu.

"Huu ni ushahidi zaidi kwamba tunalekea katika dunia yenye joto jingi, iwapo tutaruhusu kuendelea kutolewa kwa hewa ya ukaa," anasema Dk. Katherine Kramer, kutoka asasi iitwayo Christian Aid.

"Kwa watu wengi kutoka dunia inayoendelea, kumekuwapo ukweli kwa kipindi kirefu sasa, sasa mfumuko wa joto unakamata sehemu nyingi za nchi zilizoendelea kama vile Uingereza.

"Kama Waziri Mkuu anahitaji ukumbusho, asipuuzie mabadiliko hali ya hewa. Julai hii imenyesha Uingereza haiwezi kuikimbia safari inayopata joto.

"Tunahitaji kwenda kwa kasi na kuweka sawa sera zetu, zinazotambulika bungeni kwamba hali ya hewa ni ya dharura kwetu," anafafanua.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Umoja wa Mataifa kinachoshughulikia Bahari na hali ya Hewa (NOAA), mwezi wa Julai mwaka 2016, ilikuwa rekodi ya juu iliyopiku cha mwaka 1880.

NOAA inasema asilimia 90 ya joto la miezi Julai, imeshuhudiwa katika karne ya 21, ikimanaisha kuanzia mwaka 2000.

Asasi ya hali ya hewa ya Marekani (NASA), ina mtazamo tofauti kwamba, ikirejewa kiwango kikubwa cha joto cha mwaka 2016 kiko juu kuliko cha mwaka 2017.

Takwimu za mwezi Julai mwaka huu, NASA inasema zitatolewa kati ya wiki moja na mbili ijayo.

**MAONI UN**

Shirika la Hali ya Hewa Duniani, nalo linaungana na hilo kwamba mwezi uliopita, ikiutaja kwamba wastani wa joto duniani kwa siku 29 kuanzia Julai Mosi, kuna rekodi 'isiyoshikika.'

Katibu Mkuu wa Umoja wa

AFYA

# UN yalia kufikwa joto la kihistoria, watafiti watahadharisha balaa laja



Wakazi wa Uingereza waliofurika ufukweni, kutokana na joto kali, Julai 25. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Mataifa, António Guteress , alitamka Alhamisi iliyoipita, kwamba inapiku rekodi ya Julai 2016, akirejea mfano wa joto la bahari ya Pacific, lenye kawaida ya kuathiri hali ya hewa Kusini mwa Bara Amerika.

Katika mifano yake, anagusia jiji la Paris, kwamba joto lake lilifikia nyuzi joto sentigredi 42.6. Anafafanua Guteress: "Tuko katika mfululizo wa miaka mitano yenye joto lililopitiliza kutoka mwaka 2015 hadi 2019. Kama hatutachukua hatua katika mabadiliko ya hali ya hewa."

Anatoa mfano wa barafu kupotea katika ukanda wa Greenland akitaja ni mamilioni ya tani za barafu yanayeyuka kila kukicha.

Guteress anaielezea ripoti ya Umoja wa Mataifa mwaka jana, inayotathmini maamuzi ya serikali duniani kuingia katika mkakati wa kupunguza joto la nchi dunia ya tatu, kwa kiwango nyuzi joto sentigredi 1.5 kila mwaka.

Hivyo katibu mkuu analinganisha kuwa sawa na kuweka rehani uhai wa mamilioni ya watu duniani, kupitia janga la hali ya hewa, njaa na ukame.

Hadi sasa wanadamu katika nchi za dunia ya tatu wanaelezwa kuongeza joto kiwango cha sentigredi moja na kwa kasi ya mwenendo ulioko, kuna shaka kufikia nyuzi joto 2.7 ifikapo mwaka 2030, jambo linalopaswa kuchukuliwa hatua.

Akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Hali ya Hewa ya Umoja wa Afrika (AU), jijini Malabo, Equatorial Guineas, ambayo Rais Jakaya Kikwete alikuwa Mwenyekiti wake mwaka 2014, aliyekuwa Katibu

> **"Tuko katika mfululizo wa miaka mitano yenye joto lililopitiliza kutoka mwaka 2015 hadi 2019. Kama hatutachukua hatua katika mabadiliko ya hali ya hewa.**



Wakazi wa jiji la Paris, Ufaransa wakitafuta nafuu kutokana na joto kali, Julai 23 iliyopita.

Mkuu Ban Ki -moon, alikuwa na ushawishi kama wa sasa kuhusu kutetea hali ya hewa.

Katika safari ya kuzishawishi nchi za dunia ya tatu, kuridhia maoni ya mchakato wa awali kufikia Mkataba wa Paris wa Mazingira, Ban alizitaka nchi za Afrika zilizoko daraja la dunia ya tatu, kukubali kwani zingenufaika zaidi dhidi ya madhara ya hali ya hewa.

Ban Ki - moon, alitoa mifano kwamba nchi zenye viwanda vikubwa ndio zinaharibu zaidi mazingira kwa mbadala wa kunufaika kiuchumi na nchi za dunia ya tatu zinanufaika kidogo na viwanda hivyo, huku athari ya mazingira kwa watu wake zikiwa juu zaidi.

Katibu Mkuu huyo aliiomba Afrika kupitia AU, kuridhia maoni iliyoyapokea kwa mikono miwili kupitia kamati yake, ambayo yalipelekwa katika kikao cha kwanza nchini Marekani, kabla ya maazimio kupitia ngazi nyingine, hadi kufikiwa Paris.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa mbalimbali***

AFYA

# Kahama waamka katika ubia na NGO kukabili madhara ukatili kwa watoto



Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali Huheso Foundation, Juma Mwesigwa, akizungumza na wadau wa mashirika yasiyokuwa ya serikali muda mfupi kabla ya kuzinduliwa.

**Na Shaban Njia,** Kahama

UKATILI wa kijinsia kwa watoto unatajwa kuchangia ongezeko la watoto mitaani na kukwamisha kutimiza ndoto au malengo waliojiwekea tangu zama za usomi wao.

Hilo ni zao la sintofahamu kwenye familia, baba kumnyanysa mama, kushindwa kutimiza wajibu wake kwenye familia au mama kuwanyanyasa watoto na watoto wanaoishia kushindwa kuhimili na wanatoweka nyumbani, wanaishia kuanza maisha wangali wadogo.

Kutokana na ongezeko la ukatili dhidi ya watoto katika nchi nyingi, Tanzania ikiwamo mahitaji yake hayaishii suala hilo si la serikali pekee, bali hata asasi binafsi zimeamua kuingilia kati kukabili udhalilishaji watoto.

Mkoa wa Shinyanga uko katika orodha ya muda mrefu, kukishuhudiwa kuongoza ndoa za utotoni, ukatili wa kijinsia na mauaji, kwa imani za kishirikina.

Ni hali inayochangia maendeleo kuwa duni kwa wakazi wake, kupitia ngazi zote za ukoo, familia, kijiji na kata, huku jinsia ya kinamama nayo ikiangukia janga la kudhalilishwa.

Serikali katika hatua yake, imeandaa Mpango wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, lengo ni kuipunguza kwa kiwango cha asilimia 50 ifikapo mwaka 2022. Hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia 2005; Sera ya Maendeleo ya Mtoto 2008; na Sheria ya Makosa ya Kujamiana ya Mwaka 1998.

> **Hizi ni taarifa ambazo huwa zinaripotiwa pale tatizo linapokuwa kubwa, ila kwenye familia zetu ukatili bado upo kwa kiwango kikubwa sana.**



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, ambaye pia ni Ofisa Maendeleo ya Jamii katika halmashauri hiyo, Mary Chima, alipofungua mradi wa 'mwanamke amka.' **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

### HUHESO FOUNDATION

Wilberth Wanga, ni Mratibu wa Mradi wa 'Mwanamke Amka' kutoka katika shirika lisilo la kiserikali la Huheso Foundation.

Anasema, mkakati wao wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake, ni sehemu ya Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Watoto na Wanawake (MTAKUWWA).

Wamanga anasema katika lengo la kupunguza ukatili wa kijinsia ambao ni tatizo kwenye jamii., mpango wao unalenga kutekelezwa kwenye kata tano zilizopo katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, akizitaja kata hizo kuwa; ni Kilago, Kinaga, Mondo, Zongomela na Ngongwa na lengo

Anaeleza walivyolenga ni pamoja na kuwafikia hata wasiowahi kuwafikia ambao bado hawajafanyiwa ukatili wa kijinsia na kuwapatia misaada ya kiafya, ikiwamo wasichana hasa walioko katika mazingira hatarishi dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Wanga anaahidi kufikia wajumbe 120 na kuwajengea uwezo wa namna ya kupambana na ukatili wa kijinsia, sambamba na kujenga vilabu 10 mahsusi kupinga ukatili huo katika kata zinazofikiwa na mradi.

Ni mradi unaojitanua kuwanufaisha kupitia mafunzo walimu shule za msingi na sekondari, kuhusu namna ya kusimamia na kuratibu masuala ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi, kupitia uanzishaji klabu katika shule hizo.

### DAWATI LA JINSI

Ofisa wa Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia, wilayani Kahama, Koplo Iyogelo Njile, anashiriki katika kutokomeza ukatili wa jinsia kwa watoto na kinamama, akianza na kutoa elimu kwa jamii akidai asilimia kubwa ya wananchi wanashindwa kutoa taarifa, wakihofu watatengwa na jamii zao.

Anasema wengi wanaofanyiwa ukatili huo ni yatima waliokosa ama mzazi mmoja au wazazi wote na ajira za utotoni ni nyingi majumbani, wengi wanatokoa mkoani Kigoma na hata kwenye kambi za wakimbizi.

Koplo Njile anasema ukatili wilayani Kahama bado uko juu, licha ya kuwa mbali na taarifa zinazotolewa na baadhi ya wananchi, kwamba ni vitendo ambavyo vimekuwa vikiripotiwa mara nyingi Polisi.

Anasema mwanzo waliojitokeza kulalamika walikuwa wanawake na watoto wadogo, lakini sasa hata wanaume wanajitokeza baada ya kupatiwa elimu na kujitambua kuwa na haki ya kuripoti na kusaidiwa.

Njile anaendelea kusema kuwa, kesi nyingi za ukatili wa kijinsia zinaharibika, kutokana na walalamikaji hawatojitokezi mahakamani na zinaishia kufutwa, kwa sababu ya kukosa ushahidi au vielelezo.

### OFISA USTAWI WA JAMII

Abduharman Nuru, ni Ofisa Ustawi wa Jamii katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, anasema zaidi ya mashauri 908 ya ukatili wa kijinsia yanayowahusu watoto na wanawake, yameripotiwa na kutafutiwa ufumbuzi, asilimia kubwa yakiwagusa watoto.

Anasema kuwa, kwa kipindi cha kuanzia mwezi januari hadi juni mwaka huu wa 2019 zaidi ya mashauri 908 yameripotiwa na kutafutiwa ufumbuzi, huku ukatili dhidi ya watoto ukiwa 585, wa kike 222 na wanaume 351; Kutoka jumla yao, watu wazima wako 323.

"Ukatili wa kijinsia ndugu zangu kwa wilaya ya Kahama bado uko juu sana, ukilinganisha na halmashauri nyingine zilizopo mkoani kwetu," anasema Nuru akiongeza:

"Hizi ni taarifa ambazo huwa zinaripotiwa pale tatizo linapokuwa kubwa, ila kwenye familia zetu ukatili bado upo kwa kiwango kikubwa sana."

Lingine analolifanya ni kuhakikisha watokomezaji ukatili huo wameanzisha mabaraza ya watoto 98 kila kata, inayotoa mikopo kwa kinamama, vijana na walemavu.

Kuna fedha zaidi ya Sh. milioni 743 zimekwishatolewa, kwa kuanzisha vilabu 11 vya kupinga ukatili wa kijinsia shuleni.

Anasema kuwa, ukatili dhidi ya watu wazima walikuwa 323 huku wanawake wakiwa 281 na wanaume wakiwa 42 nakuongeza asilimia kubwa ya wanaofanyiwa vitendo hivyo ni wanawake na watoto wadogo.

Anasema ukatili wa kisakolojia watoto walikuwa 57, watoto wakike walikuwa 41 na watoto wakiume walikuwa 16 huku kwa watu wazima walikuwa 154, wanaume walikuwa 34 na wanawake walikuwa 120.

Nuru anasema, watoto waliofanyiwa ukatili wa kingono walikuwa 50, wavulana 19 na mabinti 31. Pia, kuna wanawake 14 waliofanyiwa ukatili wa kingono, walikuwa wote wanawake na ukatili wa kutupa watotoni zikiwa taarifa mbili ziliripotiwa.

### MKURUGENZI HALMASHAURI

Mary Chima, ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, anayesema mradi wa 'Mwanamke Amka' katika mji huo uko katika muafaka, kwani wataalamu wa halmashauri hawakufanikiwa.

> **Kuna fedha zaidi ya Sh. milioni 743 zimekwishatolewa, kwa kuanzisha vilabu 11 vya kupinga ukatili wa kijinsia shuleni.**

Anakiri kuwa, serikali pekee haiwezi kutokomeza ukatili wa kijinsia, pasipo kuwashirikisha wadau wengine binafsi, kwani mila potofu zimekuwa zikichangia uozeshwaji watoto wenye umri mdogo.

Mkurugenzi anataja tiba ya kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake, ni kutoa elimu kwa jamii kupitia kubadilisha mtazamo.

Pia, anahimiza kwamba, kinyume na mabadiliko ya elimu inaishia vifungo na kujazana magerezani, pasipo kutatua msingi mkuu wa tatizo kwenye jamii.

Ikumbukwe, Shinyanga imekuwa mkoa unaotajwa kuongoza kwa ukatili wa kijinsia kitaifa na wilaya ya Kahama, ambako kumeanzishwa mapambano kumekuwa kinara wa mkoa.

---

## Wabunge wenye ulemavu walioweka rekodi



Waandishi wa habari wakizungumza na  Eiko Kimura. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Tokyo,** Japan

NCHINI Japan kumefanyika mageuzi ya aina yake ya kidemokrasia, watu wenye ulemavu wa kipekee nchini humo katika fursa hiyo ya kuwa wenye mamlaka ya kutunga sheria.

Hao ni Yasuhiko Funago na Mama Eiko Kimura. Wote ulemavu wao uko katika hatua isiyo nzuri hata kidogo, kufikia kiwango cha kihistoria katika wabunge walemavu wa aina hiyo.

Pia, katika tafsiri ya demokrasia ndani ya bunge la Japan, napo kunaelezwa kuna mafanikio makubwa ya kihisitoria. Wote walianza kutumikia Alhamsi iliyopita, wakipokewa kwa shangwe kubwa bungeni.

Yasuhiko Funago, mwenye umri wa miaka 61 misuli yake imeathrika kwa kiasi kikubwa hata mfumo wake wa mawasiliano kwa kutumia kompyuta.

Ni hali ya maradhi yake yaliyofikia hatua mbaya zaidi katika mwaka 2000, hapo alipoteza uwezo mkubwa wa kimwili, ikiwamo kutembea.

"Nimetawaliwa na hisia ambazo wakati wake umefika," anasema Funago na kuongeza kuhusu msimamo wake kwamba:"Ninaweza kuonekana ni dhaifu, lakini nina uthubutu kuliko wengine (wabunge), kwani ni suala la kufa na kupona kwangu."



Yasuhiko Funago, akizungumza kwa kusaidiwa.

Eiko Kimura, mwili wake umetwaliwa na kupooza upande wa kulia, kuanzia usawa wa shingo yake, hali ambayo amekuwa nayo tangu akiwa na umri wa miezi minane.

Lakini, wasifu wake uko bayana kuwa ndani ya ulemavu huo, yu mpambanaji mkubwa na ana ujasiri wa 'kujichangaya' katika jamii kuyatafuta mafaniko yaliko.

Katika harakati zake hizo mpya za kisiasa, anapeperusha bendera ya chama pinzani chenye itikadi ya siasa za kushoto (ujamaa).

Ni chama ambacho muasisi wake awali alikuwa  muigizaji tamthilia, lakini baadaye akajitosa katika siasa na kufanikiwa kuutwaa ubunge na nafasi zingine mbili zinazofanya chama kuwa na wabunge watatu, ndizo zimetwaliwa na walemavu hao.

Nafasi hizo maalum walizozipata walemavu hao ni fursa maalum za kisheria zinazotolewa, kushirikisha pia wazazi wasio na waume au wake, kama vile wajane na wasio na ajira za kudumu.

Kutokana na uwapo wa wabunge hao wenye ulemavu mkubwa, kuna maboresho ya kimiundombinu yamefanyika kuwawezesha watumikie wajibu wao huo mpya kwa uhuru zaidi.

***Kwa mujibu wa taarifa za mtandao.**

MAZINGIRA

CHANGAMOTO SAFARI YA DUNIA

# Mapinduzi kilimo yanavyoteketeza hali ya hewa duniani na mazingira

• China, India zatoa ishara zao



Sehemu ya bidhaa za mizizi, viazi na karoti zinazotajwa kuathiri mazingira. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

RIPOTIYA "Matarajio ya Idadi ya Watu duniani 2019" iliyotolewa na Kitengo cha Masuala ya Idadi ya Watu katika Idara ya Masuala ya Uchumi na Jamii (DESA) ya Umoja wa Mataifa, inasema idadi ya watu duniani inatarajiwa kuongezeka kutoka bilioni 7.7 ya sasa, hadi bilioni 9.7 mwaka 2050.

Ongezeko hilo linatarajiwa kutokea katika nchi za: India, Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Pakistan, Ethiopia, Tanzania, Marekani, Uganda na Indonesia.

Pia, wastani wa ukuaji idadi ya watu dunaini, inaonekana kuwa kubwa zaidi katika nchi za kipato cha chini na kati, huku katika nchi zilizoendelea, wastani wake ukishuka.

Ripoti inafafanua kwamba, mapato husika yanatarajiwa kuongezeka kwa kasi kubwa katika nchi nyingi zenye kipato cha chini na cha kati, hususan India na Uchina, ambazo kwa pamoja zinaunda asilimia 37 ya idadi ya sasa ya watu duniani.

Kuna mtazamo kwamba bidhaa kutoka nchi hizo, zinaweza kutawala soko la dunia.

Ikiwa mapato hayo yataongezeka barani Afrika na watu wengine bilioni 1.3, maana yake ni kwamba, itakaribia nusu ya wakazi duniani.

Kwa kuzingatia mifumo ya ukuaji katika siku zijazo, Afrika na Asia

> **"Teknolojia nazo zinazoruhusu uzalishaji mzuri zaidi, hivyo ripoti inashauri umuhimu ni lengo kuu la utafiti wa kilimo, ikitoa mfano kutoka Chuo Kikuu cha Guelph, kilichopo nchini Canada.**



zitashikilia zaidi ya nusu ya watu duniani.

Ukuaji huo wa mapato, unaelezwa kusababisha kuongezeka mahitaji ya baadhi ya vyakula kama vilde nyama, maziwa, matunda na mboga mpya.

**VIZUIZI**

Pia, kingine kinachoguswa na ripoti husika ni kwamba, chakula kilichopo sasa hakiwezi kushughulikia ongezeko la mahitaji kwa jumla.

Hapo kunatajwa mambo mawili makuu; kwanza ni hitaji la kuzalisha chakula zaidi katika mfumo wa sasa, ambao ngazi ya sasa haukidhi mahitaji.

Pili, ni kwamba kilimo na uzalishaji chakula ni mfumo wa ziada, ni una athari katika mazingira. Hivyo, jamii inahitaji kutafakari tena kuhusu chakula, mapishi yake na inavyotumiwa.

Tatu, inagusa athari itokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa tayari zinaonekana, zaidi ni kwa nchi maskini zaidi duniani.

Ripoti inadokeza mtazamo kwamba, kuna jambo lisilozungumziwa kikamilifu kutoka kwenye mabadiliko ya hali ya hewa na inaweza kuwa na athari kutoka kwenye mbolea, pale inapozalisha nafaka kubwa, matunda au mboga.

Walakini huo, pia unaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa virutubishi cha vyakula vilovyopo.

Uzalishaji wa chakula ni ishara mojawapo katika mazingira. Hapo ndipo inapodokezwa tahadhari kama za haja ya kula nyama kidogo.

Kuna kundi linaloeleza kwamba, ulaji kiasi kidogo cha nyama unaweza kuifanya kuwa endelevu.

Katika badaji ya maendeo, nchi kama vile kunaelezwa kwamba, New Zealand na Australia, watu wanalisha ng'ombe na kondoo kwa sababu wana ardhi ya kutosha inayofaa uzalishaji na wanyama hao hawaathiri. Katika mifugo hiyo, uzalishaji wa kukua unazidi maradufu nyama za ng'ombe kwa kiasi kikubwa, mshindani wa karibu ikitajwa nchi kama vile Marekani.

Mazao shambani yanatajwa kuwa na uharibifu mkubwa na zinahitaji kupingwa kabisa kwa mfumo wa ikolojia uliopo, iwe nyasi na

Wakulima huendesha kilimo cha kuondoa sehemu yenye virutubishi zaidi ya mmea na mbegu zake kwa mazao kama vile ngano, mahindi, shayiri na matunda.

Hapo kuna mtindo wa kuondoa mmea mzima ua mzizi wake kama ilivyo kwa karoti na viazi. Hiyo inapoendelea mwaka mmoja, hadi mwingine, aina ya uchimbaji unaofanya udongo wa ardhi kuwa dhaifu .

Kitaalamu inatajwa, wastani wa theluthi moja ya chakula kimataifa kinaharibiwa. Katika mataifa tajiri, kunaelezwa kuwapo mazoea ya kununua chakula zaidi kuliko kinachoweza kuliwa.

Katika mataifa masikini, zaidi wanaishia katika shamba ambalo watu wanakosa vifaa vya kuhifadhi chakula na hawajaunganishwa vizuri katika masoko, kuweza kuuza kabla ya uharibifu wa vyakula.

Ni mustabali unaoifanya jamii kuongeza uzalishaji wa chakula bila ya ardhi kuwa na ardhi ya ziada, zaidi ya kutosha na mchanga bora.

Teknolojia nazo zinazoruhusu uzalishaji mzuri zaidi, hivyo ripoti inashauri umuhimu ni lengo kuu la utafiti wa kilimo, ikitoa mfano kutoka Chuo Kikuu cha Guelph, kilichopo nchini Canada.

**VYAKULA VIPI?**

Hiyo ina maana kwamba, ili kulisha watu wengine bilioni tatu duniani, pamoja na kuwapo shinikizo la hali ya hewa na uharibifu wa mazingira wa rasilimali kuu inayohitajika kutokeza chakula, mambo yanayoweza kubadilika.

Wanasayansi wanaendelea kujitahidi kubuni uzalishaji wa aina ya mazao yanayostahimili ukame na kuhimili mafuriko.

***Makala hii imeandaliwa na Mwandishi wa Mazingira, Jenifer Julius, kwa msaada wa taarifa mbalimbali za kimataifa.***

AFYA

# Ummy Mwalimu alipotoa darasa ‘kila kitu’ ndani ya unyonyeshaji

Na Yasmine Protace

## • Awanyooshea mkono wanaokaidi sheria



Waziri Ummy Mwalimu, akizungumza katika Wiki ya Unyonyeshaji ya mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

BADO nyayo za Wiki ya Unyonyeshaji kitaifa hazijatoweka. Hapo kuna kujiuliza chimbuko lake nini? Marejeo ni Azimio la Innocenti la Mwaka 1991, nchini Italia linalolenga kuwawezesha wanawake maziwa yao pekee kwa ‘vichanga’ vyao miezi sita tangu kujifungua.

Ni matunda ya kilichoafikiwa katika mji wa Innocenti nchini Italia, wawakilishi wa nchi mbalimbali zikiwamo Tanzania, wadau na vyombo vya Umoja wa Mataifa, zikiwamo Shirika la Afya(WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), waliridhia.

Hiyo ilifanyika kwa utiaji saini kulinda, kuendeleza na kusaidia unyonyeshaji maziwa ya mama, kama njia pekee bora zaidi ya kuwapatia watoto mlo bora.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alitamka hivi karibuni katika maadhimisho hayo jamii inapata jukwaa la kukumbushana umuhimu wa maziwa ya mama na yanavyosaidia kuboresha afya ya watoto wachanga, kuimarisha kinga na ukuaji wa mwili na akili ya watoto.

### MALENGO UNYONYESHAJI

Ummy anaainisha malengo ya Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama mwaka huu, ni kuinua uelewa wa jamii kuhusu usawa wa kijinsia, sheria na kanuni, zinavyolinda, kuendeleza na kusaidia unyonyeshaji maziwa ya mama na ubora wa lishe ya watoto.

Anasema, katika hilo washirikisha taasisi na watu binafsi kuchangia ulinzi, kuendeleza na kusaidia unyonyeshaji maziwa ya mama, hivyo inaboresha lishe ya jamii.

Waziri anasema, katika utekelezaji uliopo wanahimiza kuimarisha usawa wa kijinsia, usimamizi na utekelezaji wa sheria na kanuni zinazosaidia malengo tajwa .

Anasema Wiki ya Unyonyeshaji Duniani mwaka huu ina kaulimbiu: “Wawezeshe wazazi kufanikisha unyonyeshaji” inayobeba ujumbe wanawake na wenza wao kusaidiwa watekeleze kwa ufanisi jukumu la kuwanyonyesha watoto wao.

Kaulimbiu hiyo, pia inahimiza uwajibikaji wa pamoja wa wadau ikiwamo watumishi wa serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi, vyombo vya habari na jamii kwa ujumla katika kulinda, kuendeleza na kusaidia unyonyeshaji maziwa ya mama, hivyo kuboresha lishe ya jamii. .

### PICHA INAYOTAWALA

Waziri Ummy anataja takwimu za ulishaji watoto nchini kwa mujibu wa utafiti wa lishe nchini mwaka 2018, zinaonyesha wastani wa asilimia 97 ya watoto wenye umri chini ya miaka miwili wananyonyeshwa maziwa ya mama.

“Takwimu hii inaonyesha kuwa hali ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama imepungua, ikilinganishwa na takwimu ya mwaka 2015/2016 ambayo ilikuwa asilimia 98,” anasema.

Pia, Ummy anasema, idadi ya watoto wanaoanzishiwa kunyonyeshwa maziwa ya mama kwa wakati sahihi, ambayo ni saa moja baada ya kuzaliwa ni asilimia 53, ikilinganishwa na asilimia 51 ya mwaka 2015/2016.

Anasema kuwa idadi ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila ya kupewa maji, vinywaji na vyakula vingine katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58, ikilinganishwa na asilimia 59 ya mwaka 2015/2016.

Ummy analifafanua hilo kuwa idadi ya watoto wenye umri wa miezi sita hadi 23 wanaolishwa chakula kinachokidhi vigezo bora vya lishe ni asilimia 35, akitaja kuwa ni kiwango kilichoongezeka, ikilinganishwa na asilimia 10 kwa mwaka huo wa awali.

Anataja vigezo vinavyotumika kuwa ni idadi sahihi ya milo anayopewa mtoto kwa siku kulingana na umri wake, anauainisha kuwa na mchanganyiko wa vyakula kutoka makundi yasiyopungua manne, yakiendana na huduma za kunyonyesha maziwa ya mama au mengineyo.

Ummy anaongeza kuwa, ili kuboresha viwango vya unyonyeshaji na ulishaji watoto vyakula vya nyongeza, kila mtu ana wajibu nao ikiongozwa na Azimio la Innocenti, 1991.

> **Ukimzoesha mtoto wako ni wa kiume wewe unampa midori au kioo ajiangalie atafikiri maisha yake yake yote vitu hivyo vinafaa kutumiwa naye.**

### VYOMBO VYA LISHE

Hivi sasa kuna mchakato wa kuanzishwa vyombo vya kuratibu na kusimamia unyonyeshaji kitaifa, kukidhamiriwa kuwapo kamati ya unyonyeshaji kitaifa inayojumuisha; serikali, asasi za kiraia na wanataaluma.

Waziri anasema, masuala ya lishe yanaratibiwa na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania na katika Mpango Jumuishi wa Lishe wa Taifa imeanzishwa Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu wa Lishe ya Wanawake, Watoto na Vijana waliopoevuka.

Anasema kuhakikisha kuwa kila kituo kinachotoa huduma ya afya hususani huduma za kujifungua kwa wanawake zinatekeleza hatua kumi za kufanikisha unyonyeshaji maziwa ya mama.

Hatua zake zinatajwa kuwa ni kuwafundisha wanawake wanaohudhuria kliniki ya wajawazito faida za unyonyeshaji, kuwasaidia kinamama unyonyeshaji ndani ya saa moja baada ya kujifungua, jinsi ya kukamua maziwa ya mama na unyonyeshaji maziwa ya mama pekee kabla mzazi hajaruhusiwa kwenda nyumbani, baada ya kujifungua.

Huku akirejea vigezo kimataifa, Waziri Ummy anasema Tanzania ina kanuni ya kitaifa inayosimamia taratibu za uuzaji, usambazaji maziwa na vyakula vya watoto wachanga na wadogo, chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

### SHERIA KAZINI

Waziri Ummy anafafanua kuwa: “Suala hili limezingatiwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004 inayotumika nchini Tanzania. “

“Kupitia sheria hii, wanawake waliojifungua wanayo haki ya kupewa likizo ya uzazi yenye malipo ya siku 84. Endapo mwanamke atajifungua watoto mapacha anastahili likizo ya uzazi ya siku 100,” anasema.

Pia, anachambua kanuni za sheria hiyo ya mwaka 2017, kinachompa fursa mwanamke arudipo kazini baada ya likizo yake ya uzazi, haki ya ruhusa saa mbili kwa siku kumnyonyesha mtoto ambayo mnyonyeshaji atakubaliana na mwajiri.

Ni aina ya ruhusa kisheria inayomfungulia mlango baba wa mtoto likizo ya siku tano, ndani ya wiki moja mke anapojifungua.

Ummy anataja faida zinazoendana na unyoyeshaji kwa jamii, familia, jamii na taifa kwa ujumla ni zifuatazo:

- Watoto wachanga watakuwa na hali nzuri ya lishe itakayoboresha ukuaji na maendeleo yao kimwili na kiakili.
- Kasi ya watoto kupata magonjwa hatari ya kuambukizwa itapungua na hivyo kupunguza vifo vya watoto nchini.
- Hali ya lishe na afya ya wanawake itaboreka kwa kupunguza uwezekano wa kupata saratani ya matiti na via vya uzazi; pamoja na kuepuka kupata mimba nyingine katika kipindi cha miezi michache baada ya kujifungua.
- Gharama za matibabu zitapungua kutokana na kuimarika kwa kinga ya mwili kwa watoto hali itakayosababisha kupungua kwa kasi ya watoto kuugua mara

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Ummy Mwalimu alipotoa darasa 'kila kitu' ndani ya unyonyeshaji

INATOKA UK.19

kwa mara.

• Tija katika shughuli za uzalishaji mali itaongezeka kutokana na wazazi kutumia muda mwingi katika kufanya kazi za kuongeza pato la familia badala ya kutumia muda huo kuuguza watoto.

• Wanawake wanaonyonyesha watazidi kujiamini kuwa wanaweza kuwanyonyesha watoto wao vizuri kutokana na kutambua kuwa jamii ipo tayari kuwasaidia ili waweze kufanikisha unyonyeshaji inavyopaswa.

**UTAPIAMLO**

Ummy anazungumzia athari za lishe duni, kwamba kuna kiwango kikubwa cha utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano na utafiti wa lishe nchini mwaka jana, unaonyesha asilimia 31 wamedumaa, ikilinganishwa na asilimia 34 ya mwaka 2015/2016. .

Anataja sababu kubwa ya utapiamlo huo, ni lishe duni inayochangiwa na majukumu mengi yanayomkabili mama, hivyo wanakosa muda wa kuwatunza watoto.

Waziri Ummy anasema, ujumbe wa Wiki ya Unyonyeshaji mwaka huu unaikumbusha jamii wajibu wa kuwawezesha wanawake wazazi kunyonyesha watoto wao maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo.

Wadau ambao ni baba wa mtoto, familia yake, jamii, waajiri na sekta binafsi, wanakumbushwa wajibu wa kumsaidia mwanamke fursa ya kumnyonyesha mtoto maziwa yake pekee katika miezi sita inayoridhiwa kiafya na kuendelezwa na milo mingine katika miaka miwili.

Ummy anataja sehemu ya uwezeshaji huo, ni kutoa elimu na taarifa sahihi zinazohusu faida za unyonyeshaji Anaongeza: "Utamaduni wa ulishaji watoto kwa kutumia chupa unaanza kujitokeza sasa."

"Jambo hili linahitaji juhudi za makusudi za uelimishaji jamii, kuwajengea wanawake hali ya kujiamini kuwa kunyonyesha watoto maziwa ya mama ndiyo njia bora zaidi kuliko zote ya ulishaji watoto.

"Jamii inapaswa kumwondolea mwanamke vikwazo vinamfanya ashindwe kunyonyesha mtoto wake ipasavyo, pamoja na ushawishi wa kibiashara kutoka kwa wauzaji wa vyakula mbadala vya watoto na hisia au imani na mitazamo isiyo sahihi katika jamii dhidi ya unyonyeshaji na ulishaji watoto kwa ujumla ," anasema.

Waziri anaongeza kwamba yanahitaji ulinzi wa kisheria unaosaidia kujenga mazingira wezeshi kwa wanawake kazini waweze kunyonyesha watoto wao.



Jukumu la unyoyeshaji likiendelea. **PICHA: MTANDAO.**

**HATUA KWA WAAJIRI**

Waziri Ummy anasema, serikali kupitia wizara yake imetangaza kuwachukulia hatua waajiri wote wanaokaidi sheria kwa kukwepa kutoa likizo kwa kinamama wazazi.

"Haki ya mwanamke kuzaa na kupata likizo ya uzazi ni ya asili, haitakiwi kuwekewa vikwazo au changamoto yoyote, kwa hiyo nitoe wito kwa wanawake ambao wanafanya kazi, ni haki yako kupata likizo," anasema na kuongeza:

"Asije mtu anakwambia anaijaza kazi yako kwa kuwa umetoka likizo ya kujifungua. Tuambie sisi, tutachukua hatua na huyo mwajiri tutamtangaza kuwa ni adui wa wanawake na watoto wa Tanzania, "anasema.

Waziri Ummy anaeleza kuwa serikali ipo katika mpango wa kuanzisha dawati la malalamiko litaloshughulikia kupigania na kutetea haki za wanawake kupata likizo ya uzazi, jambo litalosaidia kudhibiti waajiri wanaowakandamiza katika haki hiyo.

**KUTOKA UNICEF**

Mwakilishi wa UNICEF, James Gitau, anasema unyonyeshaji ni moja ya njia muhimu inayohakikisha afya bora kwa mtoto na wito wake kwa

wanahabari kuhakikisha wanaivusha elimu hiyo mbali, hususan kwa kinamama.

Gitau anaiomba serikali kuongeza nguvu katika uhamasishaji wa kupatikana haki ya watoto kunyonyeshwa, jambo analoamini litasaidia kuokoa watoto dhidi ya magonjwa yatokanayo na kukosa virutubisho kutoka kwenye maziwa ya mama.

## ...TGNP waibukia vyumba vya kunyonyesha

**Na Yasmine Protace**

WAKATI Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akitoa ufafanuzi wa kina kuhusu nafasi ya unyoyeshaji, asasi ya

TGNP Mtandao imemuunga mkono kwa kuanzisha chumba maalamu kwa ajili ya wanawake kunyonyesha watoto wao.

Deograthias Temba, ni Ofisa Programu Mwandamizi wa TGNP Mtandao, anayesema ofisi yao inaunga mkono serikali kuamua kutenga vyumba kwa ajili ya kinamama kunyonyesha.

"Kutengwa kwa vyumba jicho ni pongezi kubwa kwa Waziri Ummy Mwalimu, kwa kuangalia umuhimu wa wakina mama katika kunyonyesha," anasema .

Temba anafafanua kwamba, kinamama wakitengewa sehemu ya kunyonyesha, inawasaidia kutanua wigo wa uchumi kutokana na muda ambao angeupoteza kwenda nyumbani kunyonyesha, sasa anautumia alipo kazini.

Temba anasema, baadhi ya kampuni zimekuwa zikiuza haki hiyo na haiwajali wanawake wanaonyonyesha na wengine wamejikuta wakipoteza ajira, baada ya kujifungua, jambo ambalo Waziri Ummy ameshalikemea.

Anasema katika kuwajali wanawake, TGNP Mtandao, imetenga vyumba maalumu vya kunyonyeshea watoto katika ofisi yao, ambako kuna wanawake wanafika mikutanoni au kufuata baadhi ya shughuli za kiofisi, watoto wao wananyonya pasipo bugudha.

Pia, ofisa huyo mwanaharakati wa haki za kijinsia, anasema kuwapo chumba maalumu cha kunyonyesha watoto, njia mojawapo ya kumezesha mama mwenye mtoto kunyonyesha pasipo shaka yoyote

.Anasema, mwaka jana waliandika barua kwa mawaziri wa Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kuomba sauti hiyo bunge, juu ya kuwapo na vyumba vya kunyonyeshea watoto mahali pa kazi.

Kupitia mwitikio huo, Temba anaeleza kushukuru barua zao zilijibiwa na sasa wizara imetenga chumba maalumu kwa ajili ya kina mama kunyonyesha watoto.

"TGNP Mtandao tunampongeza Waziri Ummy kwa kuandaa chumba maalumu kwa ajili ya kunyonyesha," anasema.

Anaongeza kuwa, mwaka jana alianzisha programu ya kuwapo na 'vilinge' sehemu za kazi zinazowawezesha wanawake kuzitumia kunyonyeshea watoto wao na kuisaida hata msukumo wa uchumi kupanda, kwa kujenga ufanisi katika utendaji wao.



# Pinda mgeni rasmi Nanenane Nyanda za Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI Mkuu mstaafu wa awamu ya nne, Mizengo Pinda, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayofanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye ndiye mwenyeji wa maonyesho hayo wakati kikao cha majumuisho ya maonyesho hayo na kuwataka wakulima kujiandaa kumpokea mkulima mwenzao.

Alisema maandalizi ya kilele hicho yamekamilika ikiwamo kuandaa maeneo atakayotembelea kiongozi huyo pamoja na utaratibu wa wakulima kuonyesha teknolojia wanazozitumia kwenye uzalishaji.

Aliwataka wenye mabanda ya maonyesho kuwahi ili mgeni huyo maarufu 'Mtoto wa Mkulima' atakapokuwa anatembelea awakute wataalamu na wampe maelezo kuhusu teknolojia zao.

"Maonyesho yetu yalifunguliwa rasmi na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na tunatarajia yatafungwa na mzee wetu Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, hivyo tujiandae kumpokea," alisema Chalamila.

Aliwasisitiza wataalamu wa halmashauri kuweka utaratibu mzuri wa kuzifikisha teknolojia za kilimo zinazoonyeshwa kwenye maonyesho hayo kwa wakulima ili kuyafanya kuwa na uhalisia tofauti na ilivyo sasa.

Alisema kuwa taarifa za utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi zinazotolewa na wataalamu zinaonyesha ukanda huo ni rafiki kwa uzalishaji, lakini wananchi wanashindwa kuzitumia teknolojia hizo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, aliitaka sekretarieti ya maandalizi ya maonyesho hayo kuwa na kanzi data ya wananchi wanaojitokeza kwenye maonyesho hayo pamoja na waonyeshaji. Alisema utaratibu huo utawasaidia katika kufanya tathmini ya maonyesho hayo na kujua kama yanawasaidia wananchi ama la pamoja na kutafuta mbinu za kuboresha.

"Wananchi wanakuja na kuondoka, lakini hatujui ni wangapi wanakuja kujifunza, hii haitatusaidia hivyo wataalamu wetu lazima mtusaidie kuandaa taarifa za watu na kuwe na ufuatiliaji wa kile wanachojifunza hapa ili tujue kama kinawasaidia," alisema Mtatiro.

Baadhi ya wananchi waliotembelea maonyesho hayo walisema wanavutiwa na baadhi ya mbegu za mazao yakiwamo maharage ambayo yanazalishwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Kituo cha Uyole.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Mwambungu, alisema kituo hicho kina mbegu za maharage ambazo zina madini ya chuma na zinki, madini ambayo ni muhimu kwa afya za wananchi.

Alisema wataalamu hao wanafundisha namna ya kulima na pamoja na soko lake lilivyo na hivyo akawashauri wananchi wengine kutembelea ili kujifunza na kuanza kuzitumia.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akikagua ajali baada ya bodaboda kugongwa na gari katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la Tangi Mbovu, jijini Dar es Salaam jana. Dereva wa bodaboda alitambulika kuwa ni mfanyakazi wa kampuni ya Mwananchi Communications Ltd, Athumani Omari. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wafugaji waendeleza migogoro waonywa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya imewatahadharisha wafugaji wanaoendeleza migogoro ya ardhi na wakulima kwa kuchungia mifugo kwenye mazao ya wakulima kuwa itawachukulia hatua kali za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

Vile vile, baadhi ya wafugaji hao wanadaiwa kutumia nguvu kuingiza mifugo kwenye mazao ya wakulima kwa kuwacharaza bakora wakulima hasa wanawake wanaowazuia kuingiza mifugo hiyo kwenye mashamba hali ambayo inazua uhasama miongoni mwa makundi hayo.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Mhandisi Maryprisca Mahundi, wakati alipokuwa anafungua mkutano wa mradi wa uboreshaji na usimamizi wa rasilimali za umma na uwajibikaji katika sekta ya kilimo na mifugo katika Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Alisema wafugaji wamekuwa wakifanya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake wakiwa mashambani kwa lengo la kuwalazimisha kuingiza mifugo yao kwenye mashamba bila kujali kuwa kwenye mashamba hayo kuna mazao ambayo bado hayajavunwa.

Mahundi alisema serikali haiwezi kuendelea kuvumilia vitendo vya aina hiyo viendelee kwenye jamii na kwamba ndio maana iliamua kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji ili kuepuka kuingiliana kwenye shughuli zao za uzalishaji mali na hivyo akawataka kuacha mara moja vitendo hivyo.

Alisema vitendo hivyo ni kinyume na maagizo ya serikali ya kuhakikisha migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji inakomeshwa ili kudumisha amani na mshikamano miongoni mwa jamii.

Alilitaka jukwaa la wakulima na wafugaji linaloundwa wilayani humo kuhakikisha linatumika kwa ajili ya kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji na kwamba endapo litashindwa kutakuwa hakuna maana ya kuendelea kuwapo.

"Katika kuhakikisha tunamaliza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji tuliamua kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya wafugaji ili kuepuka kuingiliana, lakini pia tulifanya hivyo ili kuweka utaratibu mzuri wa matumizi ya ardhi, sasa ombeni jukwaa hili litakaloundwa likawe msaada kwenye utatuzi wa migogoro hii," alisema Mahundi.

Alizitaja kata zenye wafugaji wengi wasiotaka kufuata sheria pamoja na kufanya vitendo vya ukatili dhidi ya wafugaji kuwa ni Upendo, Mamba na Lualaje na kwamba kwenye maeneo hayo vimekuwa vikiripotiwa visa vingi vya ukatili vinavyofanywa na wafugaji hao.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Mtandao wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali mkoani Mbeya (Mbengonet), ambayo yanajishughulisha na kukuza utawala bora na uwajibikaji wa jamii, Paulo Kitta, alisema lengo la mradi huo ni kuongeza ushiriki wa wananchi katika kuchangia miradi ya maendeleo kwa sekta ya kilimo na mifugo ili kukuza umiliki na uendelevu wa miradi.

Akizungumzia suala la wafugaji kuwavamia na kuwapiga wakulima, Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ni Chunya, James Kidayi, alisema uongozi wa wafugaji haujawahi kupata malalamiko kutoka kwa wakulima kuhusu kupigwa na wafugaji na kwamba endapo wangekuwa wamepata taarifa hizo wangekuwa wameshalishughulikia.

Aliwataka wakulima kutoa ushirikiano kwa viongozi wa wafugaji ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za uonezi wanazofanyiwa ili hatua zichukuliwe mapema na kumaliza migogoro ambayo sio ya lazima miongoni mwao.

"Sisi tuna maeneo yetu ya kuchungia mifugo na kwa bahati mbaya sana hatujawahi kupata malalamiko hayo kutoka kwa wakulima, lakini hatuwezi kukataa kuwa vitendo hivyo havipo maana watu tunatofautiana akili zetu, tunaomba wenzetu wakulima wawe wanatuletea taarifa hizo.

# Vijana wasisitizwa kujiunga JKT kujiajiri

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

VIJANA katika Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameshauriwa kujitokeza kwenye mafunzo ya uzalishaji mali yanayotolewa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili wapate mafunzo yatakayowasaidia kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mwakilishi wa Mkuu wa JKT, Kanali Julius Kadawi, kwenye Maonyesho ya Wakulima (Nanenane ) Kanda ya Nyanda za Juu kusini.

Alisema jeshi hilo linatoa mafunzo yanayohusu shughuli za kijamii na uzalishaji mali.

Alitoa ushauri huo baada ya kutembelea mifugo pamoja na vipando mbalimbali ambavyo vimeandaliwa na jeshi hilo kupitia vijana wa kujitolea.

Kanali Kadawi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Utumishi wa JKT, alisema vijana wasiwe waoga wa kujiunga na nafasi za kujitolea kwa kuwa yanasaidia kujua kazi mbalimbali ambazo yanasaidia baada ya kumaliza mafunzo.

Alisema jeshi hilo limekuwa likitumia vijana katika kazi mbalimbali na kupata elimu ikiwa ni sehemu ya kujifunza na hatimaye kujiajiri baada ya kumaliza mafunzo hayo.

"Pia tumekuwa tukitoa elimu kwa wananchi wanaozunguka kambi zetu za jeshi ili waweze kujifunza shughuli za uzalishaji mali wakiwa kwenye makazi yao, tunatumia mashamba darasa kufikisha elimu hiyo," alisema Kanali Kadawi.

Baadhi ya vijana wanaotumiwa na Kambi ya JKT 844 KJ Itende ya jijini Mbeya, walisema mafunzo wanayoyapata ni mazuri na yatawasaidia kujiajiri watakaporudi nyumbani.

Mmoja wa vijana hao, Jackson Mgonyo, ambaye anafanya kazi kwa kujitolea, aliwataka vijana wanaojiunga na JKT kuondoa dhana ya kuajiriwa na badala yake wajenge imani ya kujiajiri kwa kutumia elimu hiyo.





# Serikali yasisitiza mafunzo usindikaji

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAJASIRIAMALI wataweza kufanya kazi kwa ubora zaidi iwapo wataalamu wa usindikaji watawafundisha vijana njia bora za kuongezea thamani mazao yao.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Stella Manyanya, alisema hayo wakati akitembelea mabanda mbalimbali kwenye Maonyesho ya 26 ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Aliwataka wataalamu wa kilimo kuwafundisha wajasiriamali vijana jinsi ya kusindika bidhaa wanazozalisha ili waziongezee thamani tofauti na ilivyo sasa.

Manyanya alikumbusha kuwa kwa Dodoma ni makao makuu na vijana wengi wanahamia kwa hiyo ni vema wataalamu wakatoa elimu ya usindikaji ili kuwawezesha vijana kuwekeza katika kilimo na ufugaji.

Naibu waziri huyo alisema, viwanda bila wakulima na wafugaji haviwezi kusonga mbele kwa hiyo wataalamu kutoka wizara hiyo na ile ya kilimo wanapaswa kushirikiana kuhakikisha mnatoa elimu juu ya usindikaji wa bidhaa ili kuongeza thamani jambo ambalo litawapa faida wajasiriamali na taifa kwa ujumla.

"Mkiwapa elimu ya usindikaji itasaidia kuzuia upotevu wa bidhaa mashambani kama ilivyo sasa kwa sababu watakuwa wakizisindika," alisema Manyanya.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni wataalamu kutumia fursa ya maonyesho haya kuwasisitiza wakulima kusindika bidhaa ili ziweze kuwa bora na kuingia katika soko la ushindani la kimataifa.

Alisema pamoja na kuwa kuna changamoto ya soko la bidhaa hiyo ya usindikaji itawasaidia kuongeza upatikanaji wa masoko ya bidhaa ambazo wanalima na kutengeneza.

"Viwanda haviwezi kufanya vizuri bila wakulima na wafugaji kwa hiyo naomba muwasisitize juu ya suala zima la usindikaji bidhaa zao," alisema Manyanya.

Alisema lengo la serikali ni kuona wakulima na wafugaji wanapiga hatua katika kilimo na ufugaji wanaofanya katika maeneo mbalimbali wanayotoka. Katika hatua nyingine amewataka wakulima na wafugaji kupeleka fedha zao benki ili ziweze kuzaa faida katika mzunguko wa shughuli nyingine za kibenki ambazo zinaleta faida badala ya kuzihifadhi nyumbani kwenye magunia na chini ya magodoro ambapo usalama wake ni mdogo.

Naibu Waziri alisema hivi sasa Benki Kuu (BoT), imetoa fursa ya kuhifadhi fedha ikiwamo kutoa mitaji kwa wajasiriamali kupitia dhamana.

Alisema hilo ni jambo jema ambalo litawasaidia kuongeza ufanisi katika biashara wanazofanya.

"Nawapongeza benki kwa kuanzisha utaratibu huo kwa sababu utawasaidia sana wajasiriamali katika kuendeleza mitaji yao," alisema Manyanya.

Aliwataka kuchangamkia fursa ili waweze kupiga hatua kwa kile wanachokifanya.

Akizungumzia maonyesho hayo kwa ujumla alisema mwaka huu yamekuwa bora zaidi tofauti na miaka ya nyuma kutokana na kwamba wananchi wanazidi kuonyesha mwamko kadri siku zinavyokwenda.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, akiangalia nyanya zilizostawishwa kwenye bustani ya kampuni ya East African Seed (T) LTD inayojihusisha na utengenezaji wa dawa za mbegu za mimea mbalimbali alipotembelea kwenye banda hilo lililopo Halmashauri ya Chamwino viwanja vya Nzuguni Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC: TBS jengeni maabara Dodoma

Na Peter Mkwavila, DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amelitaka Shirika la Viwango la Taifa (TBS) kujenga maabara mkoani Dodoma ili kufanya ukaguzi na uchunguzi mapema ili kuwezesha wawekezaji kupata vibali vya kufanya kazi kwa haraka.

Dk. Mahenge alitoa ushauri huo alipotembelea kiwanda kipya cha kisasa cha kukamua mafuta ya alizeti cha Pyxus Agriculture Tanzania, kilichopo Kizota jijini hapa.

Aidha, alisema kuwa kumekuwapo na malalamiko kwa baadhi ya wawekezaji kucheleweshwa kupata vibali na kuwataka TBS kuondoa kasoro hiyo.

Alisema kutokana na uhitaji huo analishauri shirika la viwango, kutumia kila mbinu kujenga maabara ili kuwasaidia wawekezaji hao kupata vibali kwa wakati.

Aidha, alikipongeza kiwanda hicho kuja na utaratibu wa kutoa mikataba kwa wakulima wa mazao ili kuwasaidia kupata soko la uhakika.

Halikadhalika, alisema kwa upande wa serikali itandelea kushirikiana na wakulima kwa kuwatafutia masoko ya uhakika, ikiwamo mbegu za kisasa kwa lengo la kuwakwamua kiuchumi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Malcom McGrath, alisema kuwa wanatarajia kuanza kazi mara baada ya shirika la viwango, kuwathibitisha bidhaa zao.

Alieleza kuwa kiwanda hicho pamoja na kuhakikisha mazao yatakayoletwa yanakaguliwa kwa mashine ya kisasa, itatumia utaalamu huo kutambua kama mbegu za mafuta na nafaka nyingine zimechanganywa pamoja na alizeti.

# Askofu ahimiza kuchagua waadilifu

Na Peter Mkwavila, MPWAPWA

WAPIGAKURA wamekumbushwa kuwa kuchagua viongozi ni jukumu lao na kuonywa wasifanye makosa katika uchaguzi wa serikali za mitaa na vijijini unaofanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Aidha, wamekumbushwa kuwachagua viongozi wanaopigana na umaskini na wenye juhudi za maendeleo tena wanaounga mkono kazi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Askofu mstaafu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAM) Kanda ya Mashariki, Everest Mkomekwa, alipokuwa akizungumza na wanahabari.

Aidha, aliwashauri wagombea wenye sifa ya uongozi kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi ambao utafanyika mwaka huu nchini kote.

Askofu huyo aliwataka Watanzania kwenye uchaguzi huo wasifanye makosa ambayo ni hasara kwa taifa na watu wake kwa kuwachagua viongozi wasiokuwa waadilifu, mafisadi na wenye sifa ya wapinga maendeleo.

Aidha, walishauriwa kutokubali kuwachagua viongozi wanaopingana na maendeleo yanayofanywa na serikali ya awamu ya tano.

Kadhalika, askofu huyo aliwataka wapigakura kuhakikisha wale wote wenye sifa ya uongozi wasihofie kuchukua fomu na kugombea.

Aliwaambia hakuna sababu ya kuhofia kujitokeza kwenye uchaguzi huo kugombea nafasi hizo kwa kuwa ni haki yao ya msingi.

Alisema kuwa ili uchaguzi huo uweze kufanikiwa wanatakiwa kujitokeza kwa wingi badala ya kukaa majumbani na kusubiri watu wengine wawachagulie viongozi wa kuongoza vijiji, mitaa na vitongoji hivyo ni vizuri wakatumia nafasi hiyo kujitokeza kwa wingi ili waweze kufanya maamuzi yatakayoweza kuwapata viongozi wenye uchungu kwa ajili ya taifa na rasilimali zake.

Askofu huyo alisema kuwa Tanzania inahitaji kuwa na viongozi wenye uadilifu, wachapa kazi ambao pia wataunga mkono juhudi zinazofanywa na Rais Magufuli.

Mwangalizi wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAM) lililopo Bonde la Mtera Aswile Mwandambo, aliwataka Watanzania wajitokeze kushiriki uchaguzi huo muhimu kwa ngazi ya serikali ya mitaa.



## Waraka wasukwa kutatua kero viwanja vya ndege

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, amesema Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na vyombo vya usalama vinatarajia kutengeneza waraka na kuwasilisha serikalini ili kutafuta njia bora ya kufanya kazi kwa ushirikiano.

Akizungumza katika mwendelezo wa ziara yake visiwani Zanzibar, Masauni alisema hatua hiyo inalenga kukuza ushirikiano katika kufanya kazi za kuwahudumia wageni na wananchi kwa ujumla.

Alisema kutokana na umuhimu wa viwanja vya ndege, kunahitajika ushirikiano ili kuondoa usumbufu ikiwamo foleni katika kuwahudumia wageni.

Masauni pia aliipongeza mamlaka hiyo, Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji kwa kubuni njia za kuharakisha utendaji kazi ikiwamo kuajiri vijana wenye taaluma za kazi na kuimarisha mifumo ya mawasiliano na ulinzi.

"Kitu ambacho kinahitajika kufanyika ni kuona ule upungufu ambao umejitokeza hususani katika vyombo vyetu hivi viwili, unaboreshwa ili kazi ziendelee kufanyika vizuri," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Rajab Ali Mussa, alisema wanatarajia kufunga mitambo mipya ya vipoza hewa na vifaa vya kufanyia upekuzi ili kupunguza muda wa kufanya kazi hiyo.

"Kwa sasa, tupo vizuri kwani ile hali ya usumbufu katika ukaguzi itapungua kwa kiasi kikubwa," alisema.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akipata maelekezo alipotembelea Kiwanda cha nguo cha Cotex, ambacho kinatarajiwa kufufuliwa baada ya kutofanya kazi kwa muda mrefu huko Chumbuni Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yapata kampuni mpya kufufua kiwanda cha Cotex

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeamua kuipa kampuni ya uwekezaji ya Basra Textile Milles jukumu la kufufua kiwanda cha nguo cha Cotex kilichoko Mtaa wa Chumbuni ikiwa ni sehemu ya uimarisha sekta ya viwanda nchini.

Uamuzi huo umechukuliwa kutokana na kiwanda hicho kusitisha uzalishaji kwa miaka 25 na kusababisha watu wengi kupoteza ajira.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, aliyasema hayo alipofanya ziara ya kuangalia eneo la kiwanda hicho ambalo limekuwa na magofu.

Balozi Iddi alisema zipo taratibu za uwekezaji zilizowekwa sahihi na serikali kupitia taasisi zake ambazo kampuni au mwekezaji analazimika kuzifuata. Aliuagiza uongozi wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar kuhakikisha mali za mwekezaji aliyeshindwa kukiendeleza kiwanda hicho, zinaondoshwa ili kumpisha mwekezaji aliyekuwa tayari kufanya kazi hiyo.

Alisema kiwanda hicho ni miongoni mwa maeneo yanayoweza kusaidia kupata nafasi nyingi za ajira, hivyo kutimiza nia ya serikali kuimarisha viwanda ili kuongeza mapato na kustawisha maisha ya wananchi wake.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar, Ali Khamis Juma, alimweleza Balozi Iddi kuwa mwekezaji alipewa agizo la kuondoka na kuhamisha mali zake baada ya kushindwa kukiendeleza kiwanda cha Cotex kwa miaka mingi.

Alisema wizara kwa kushirikiana na vyombo vya dola imelazimika kuchukua hatua ya kumwondoa kwa nguvu kutokana na ukaidi wake. Alisema wizara hiyo pia imeshawasiliana na Mamlaka ya Mapato (TRA) kufanya ukaguzi wa magari matano ya thamani kubwa yaliyomo ndani ya kiwanda hicho ambayo hayana namba za usajili.

# Tume: Sheria nyingi Z'bar zinapaswa kurekebishwa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

TUME ya Kurekebisha Sheria imesema Zanzibar zipo sheria nyingi za zamani ambazo zinapaswa kufanyiwa marekebisho ili ziendane na mabadiliko ya wakati.

Katibu wa tume hiyo, Kubingwa Mashaka Simba, aliyasema hayo alipozungumza na wadau mbalimbali wa sheria kisiwani Pemba kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ardhi.

Alisema Sheria ya Umiliki wa Ardhi Na.1 ya mwaka 1992 na iliyoanzisha Mahakama ya Ardhi ya mwaka ya 1994 ni miongoni mwa sheria zinazopaswa kufanyiwa marekebisho.

Alisema sheria hiyo inahitaji kufanyiwa marekebisho ili iweze kufanya kazi na kuondoa malalamiko ya migogoro ya ardhi ambayo ni changamoto kubwa kwa sasa.

"Tunakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi ambayo njia pekee ya kuipatia ufumbuzi wake ni kuwa na sheria zinazokwenda na wakati wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi," alisema.

Mrajisi wa Ardhi Zanzibar, Abdinasir Hikmany, alisema marekebisho ya Sheria za Ardhi na umiliki wake yanalenga kutatua migogoro na kubainisha matumizi sahihi ya ardhi nchini.

Alisema kwa sasa ardhi ya kilimo imevamiwa na kutumika kwa ujenzi wa nyumba za kudumu, hivyo kuhatarisha maendeleo ya sekta hiyo kwa vizazi vijavyo.

"Marekebisho ya Sheria ya Ardhi lengo lake kubwa ni kudhibiti matumizi mabaya ambayo yamepelekea uvamizi wa ardhi ikiwamo ile ya kilimo kutumika kwa makazi ya ujenzi wa nyumba za kudumu," alisema.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akikagua bidhaa ya mafuta ambayo yametengenezwa na wajasiriamali waliowezeshwa na Benki ya NBC, alipotembelea maonyesho ya Nanenane kitaifa, viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu juzi. Kulia ni Mkoa wa Mara, Adamu Malima. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Serikali yatoa maelezo kukaimu nafasi katika utumishi wa umma

**Na Restuta Damian,** BIHARAMULO

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, amewata watumishi kufuata sheria na taratibu za kazi kwa kutekeleza miongozo inayotolewa na serikali.

Amesema hayo akiwa wilayani Biharamulo mkoani Kagera baada ya kupokea taarifa ya utumishi na utawala iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Saada Malunde, na kueleza baadhi ya idara kukaimiwa kwa kipindi kinachozidi miezi sita. Dk. Mwanjelwa alisema katika utumishi suala la sababu binafsi kupeana madaraka ya kukaimu nafasi ambayo haina mhusika ni kuwavunja moyo watumishi wengine. Alisema kuwa serikali imetoa waraka wake tangu mwaka 2018 ambao unatamka juu ya nafasi ambazo hazina wakuu wa idara kukaimu ni miezi sita endapo kuna sababu ya kuendelea itolewe taarifa.

"Waraka ulishatolewa tayari wenye kusema kwamba nafasi zote zisiwe zaidi ya miezi sita endapo mnaona kuna sababu toleeni taarifa, acheni kupendeleana, fanyeni uwajibikaji," alisema Mwanjelwa.

Aidha, alisema kuwa taarifa ya Wilaya Biharamulo ambayo imeonyesha kuna watumishi wamekaimu nafasi zaidi ya mwaka mmoja kwenye Idara ya Ardhi, Fedha, Maendeleo ya Jamii na Afya bila kufanya maanuzi yoyote.

Aliongeza kuwa, ukaimu wa muda mrefu unafanya mhusika wa nafasi hiyo kushindwa kuona ufanisi wa kazi yake kutokana na kukaimishwa nafasi ambayo amepangiwa na mwajiri wake. Alisema kuwa, kufanya hivyo kunatokana na mazoea ya kazi bila kutambua uwajibikaji, hali ambayo ni kunyimana haki na kufanya upendeleo.

# DCB, manispaa kutekeleza miradi ya kimkakati

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya DCB imesema itaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi na manispaa mbalimbali nchini, na kwa sasa itaanzisha mpango maalumu kuwezesha manispaa hizo kupata fedha.

Mpango huo kupitia huduma maalumu (municipal bonds) utaziwezesha manispaa hizo kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati.

Akizungumza jijini Mwanza Mkurugenzi Mtendaji wa DCB, Godfrey Ndalahwa, alisema mpango huo utakaosaidia upatikanaji wa fedha kuendesha miradi ya kimkakati, una masharti wezeshi kwa mkopaji na tayari wameshaanza mazungumzo na manispaa na wadau wengine muhimu katika mchakato huo.

"Mchakato wa uanzishwaji wa huduma hii unaendelea tutakachofanya ni kuongeza manispaa na halmashauri nyingine ambazo pia zina miradi ya kimkakati kuweza kujumuishwa kwenye mpango huu.

"Ombi langu ni kwamba najua vyanzo viko vingi, lakini hii inaweza ikawa chanzo kizuri cha kutafuta pesa, na vilevile ni chanzo kizuri kwa ajili ya kusaidia umma wa wawekezaji wakubwa na wadogo kupata fursa ya kuwekeza kwenye miradi yetu," aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji huyo wa DCB alizungumzia udhamini na ushiriki wao katika mikutano mbalimbali na shughuli za kijamii ikiwamo Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT) uliofanyika mjini Mwanza hivi karibuni, alisema hiyo imetokana na azma ya kuanzishwa kwa benki hiyo ikiwa na kuwahudumia wananchi na wajasiriamali wadogo wadogo hasa wanawake na vijana na kufanikiwa kwa azma hiyo kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na ushirikiano kutoka katika manispaa na halmashari za Jiji la Dar es Salaam ilikoanzishwa.

"Tumekuwa tukishirikiana kwa karibu sana na Manispaa na halmashauri zote za Jiji la Dar es Salaam katika kutoa mikopo ya wanawake na vijana na mafanikio ni makubwa mpaka sasa hivi ukiangalia hiyo pesa iliyotoka na wanufaika wamenufaika mara tatu na hii ni kwa sababu ya weledi na uzoefu tulionao," alisema.

Akizungumza mafanikio ya zoezi la uuzaji hisa lililofanyika hivi karibuni, Ndalahwa alisema lilifanikiwa kwa asilimia 108 na hiyo imechangiwa sana na historia yao na mahusiano yao ya karibu na manispaa na halmashauri kwa maana wao ndiyo waanzilishi.

Alisema wigo wa kufanya biashara umeongezeka kutoka Dar es Salaam pekee na sasa wameruhusiwa kuendesha biashara nchi nzima wakiwa na matawi manane likiwamo la Dodoma pamoja na mawakala 1,000 nchi nzima, huku wakipatikana kwenye mtandao, hivyo huduma zao kupatikana nchi nzima.

# Wananchi walia meli kuwakwaza

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya wakazi wa vijiji vya mwambao wa ziwa Tanganyika mkoani Rukwa, wamelalamika kuwa wapo hatarini kupoteza maisha kutokana na kukosekana kwa usafiri wa uhakika baada ya meli ya Mv Liemba kusimama kufanya safari kwa zaidi ya mwaka mmoja hivi sasa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na gazeti hili, walisema kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja na nusu meli hiyo imesimama kwa madai inafanyiwa ukarabati hali inayowalazimu kusafiri kwa kutumia maboti na mitumbwi.

Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Samazi kilichopo mwambao wa ziwa hilo wilayani Kalambo, Pierre Sikazwe, alisema tangu meli hiyo iliposimama kufanya safari zake kati ya bandari ya Kasnga na Kigoma wamejikuta katika wakati mgumu.

Alisema hivi sasa wanalazimika kufanya safari zao kwa kutumia maboti pamoja na mitumbwi, hali ambayo ni hatari hasa katika kipindi cha pepo kari kwani vyombo hivyo vinashindwa kukabili mawimbi ya maji katika ziwa hilo.

"Kwakeli tupo katika wakati mgumu sana,na hatuna namna hapa tulipo tunajiona kama nusu wafu kutokana na kukosa usafiri wa uhakika kwa kipindi kirefu na sisi watu wa mwambao tumekuwa tukiitegemea meli ya Mv Liemba,imesimama kwa muda mrefu kwa madai kuwa inafanyiwa ukarabati," alisema.

Monica Nachula mkazi wa Kasanga, alisema daima safari zao zimekuwa roho mkononi kutokana na kukosa usafiri wa uhakika,na hawawezi kukaa bila kusafiri kwakuwa wanatafuta maisha na kusalimia ndugu zao,kitendo ambacho wanahisi kama serikali imewatelekeza.

Alisema kumekuwa na ajali za majini mara kwa mara hali ambayo ni tishio kwa maisha yao na hawaoni jitihada za kumaliza ukarabati huo haraka kana kwamba hakuna wananchi wanaoteseka kwa kukosekana kwa meli hiyo kongwe kuliko zote duniani.

Philipo Siulapwa mkazi wa kijiji cha Kasanga, alisema amegundua kuwa meli hivyo imekuwa hailipi kwakuwa baadhi ya abiria wanakwenda mjini Sumbawanga na kutumia usafiri wa mabasi ambao ni wamuda mfupi.

Alisema kwa kawaida kusafiri kutoka bandari ya Kasanga iliyopo mkoani Rukwa hadi bandari ya Kigoma mkoani Kigoma meli hiyo inatumia siku tatu, lakini ukipanda basi saa 12;00 asubuhi Sumbawanga mjini mko Rukwa unafika Kigoma mjini saa 12;00 jioni, hivyo abilia wengi waliamua kuacha kusafiri kwa kutumia meli hiyo.

Hivi karibuni Mbunge wa Nkasi Kusini, Ally Kessy, alimwambia Mkuu wa mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, kuwa serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuikarabati meli hiyo ambayo imesimama kwa kipindi kirefu na kuleta adha kubwa kwa wananchi.

Wangabo aliiomba serikali kufanya hivyo haraka kwani wakazi wa vijiji vya mwambao wanakabiliwa na hali ngumu kwakuwa usafiri wanaotumia hivi sasa ni wa maboti na mitumbwi ambao si salama kwa maisha yao.

HABARI KIMATAIFA

## Rwanda, Congo zaweka ulinzi mkali mipakani kisa ebola

**KIGALI,** Rwanda

NCHI za Rwanda na Jamhuri ya Demokrasia na Congo (DRC) zimeanza kuzuwia usafiri kuvuka kuingia katika mipaka yao wakati maofisa wakipambana kudhibiti kusambaa kwa virusi vya ugonjwa wa ebola.

Vikwazo vya kusafiri ni sehemu ya hatua zinazochukuliwa na maofisa wa nchi hizo waliokutana nchini Rwanda siku ya Jumanne.

Kulingana na taarifa iliyotolewa mwishoni mwa mkutano huo, watu wanaosafiri nje ya mipaka hiyo kwa sababu zisizo muhimu kama vile kuhudhuria warsha na mikutano ya kidini watahitaji vibali kutoka serikali zote mbili.

Mlipuko wa ugonjwa wa ebola mashariki mwa Congo umesababisha vifo vya zaidi ya watu 1,800.**DW**

## Wine: Tutaendelea kutetea haki za wanyonge

**KAMPALA,** Uganda

MBUNGE wa upinzani na mwanamuziki nchini Uganda, Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, amesema ataendelea kutetea haki za wanyonge licha ya kuandamwa na serikali ya Rais Yoweri Museveni.

Mahakama nchini humo imemfungulia mashtaka mbunge huyo na watu wengine zaidi ya 20 kwa kumkasirisha Rais Museveni.

Mbunge huyo aliyetangaza nia ya kuwania urais mwaka 2021, aliongezewa shtaka hilo, baada ya kuanza kwa kesi hiyo mwanzoni mwa wiki jijini Kampala, kutokana na mashtaka mengine yanayomkabili ya kurushia mawe msafara wa Rais Museveni mwaka uliopita.

"Mashtaka mengi ya kipumbavu yanaendelea kuwasilishwa dhidi yetu, napenda kuiambia dunia kuwa, hii haitutishi kwa njia yoyote ile," alisema Wine. **RFI**

# Waliotekwa na Al Shabaab walazimishwa kubadili dini

**NAIROBI,** Kenya

VYANZO vya kiintelijensia nchini Kenya vimeeleza kuwa madaktari wawili raia wa Cuba waliotekwa mjini Mandera Kaskazini Mashariki mwa Kenya Aprili, mwaka huu wamelazimishwa na wanamgambo wa Al-Shabaab kujiunga na dini ya Kiislamu.

Mtandao wa gazeti la Daily Nation umenukuu ripoti ya kiusalama ya hivi karibuni na kueleza kuwa madaktari hao wamehamishiwa katika msitu wa Halaanqo karibu na mji wa Barawe Kusini Magharibi mwa Somalia ambako wanadaiwa kuwasilimisha kwa lazima.

**Kazi yetu kama polisi inaishia mpakani... sipo katika nafasi ya kuelezea hatima ya madaktari wa Cuba waliotekwa lakini maofisa wangu wanashughuliki.**

Mkuu wa Jeshi la Polisi Kenya, Hilary Mutyambai, alieleza kuwa operesheni ya ukombozi wa madaktari hao raia wa Cuba inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kupata idhini ya kuvuka mpaka wa Kenya na Somalia.

"Kazi yetu kama polisi inaishia mpakani... sipo katika nafasi ya kuelezea hatima ya madaktari wa Cuba waliotekwa lakini maofisa wangu wanashughulikia," alisema Mutyabai wakati akielezea changamoto inayowakabili maofisa wake.

Hata hivyo, Mutyambai alieleza kuwa wanawazuia baadhi ya washukiwa ambao wanasaidia katika shughuli ya uchunguzi.

Watu waliokuwa wamejihami kwa bunduki waliwateka madaktari Assel Herera Corea na Landy Rodriguez, Aprili katika uvamizi mkali ambapo mmoja wa ofisa wawili wa polisi waliokuwa wakiwasindikiza madaktari hao katika kituo chao cha kazi alipigwa risasi na kuuawa.

Watekaji hao walioshukiwa kuwa wanamgambo wa kundi la kigaidi la Al-Shabaab, baadaye walitaka kupewa dola 150,000 ili kuwaachia madaktari hao, kwa mujibu wa wazee wa kijamii walioenda kijiji kimoja kushiriki katika mazungumzo ya kushinikiza kuachiliwa kwao katika eneo la Jubbaland, Somalia.

Hatima ya madaktari hao wa kigeni haijulikani kufikia sasa

Inaarifiwa madaktari hao wanaishi karibu na makazi ya Gavana wa eneo hilo ambayo ni kilomita takriban nne kutoka eneo la mpaka na Somalia.

Haijulikani ni washambuliaji wangapi waliokuwa ndani ya magari aina ya Probox ambayo kwa mujibu wa duru yalikuwa yameegeshwa karibu na makazi hayo. **BBC**




Mwanamuziki na Mbunge wa Upinzani nchini Uganda, Bobi Wine (aliyenyoosha mkono), akiwa mbele ya mahakama Aprili mwaka huu. **PICHA: AFP**

# Korea Kaskazini yatumia mabilioni kutengeneza makombora

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

RIPOTI ya Umoja wa Mataifa (UN) imeeleza kuwa Korea Kaskazini 'imeiba' dola bilioni mbili kufadhili mpango wake wa silaha kupitia uvamizi wa kimtandao.

Ripoti hiyo ambayo ilikuwa ya siri imeeleza kuwa Pyongyang inalenga mabenki na ubadilishanaji wa sarafu ya crypto-currency kukusanya pesa.

Vyanzo vya habari vimethibitishia kwamba UN ilikuwa ikichunguza mashambulio 35 ya kimtandao na kwamba Korea Kaskazini ilifyatua makombora mawili juzi ikiwa ni mara ya nne katika kipindi cha chini ya wiki mbili.

Rais wa nchi hiyo, Kim Jong-un alisema hatua hiyo ni onyo dhidi ya mazoezi ya pamoja ya kijeshi yanayofanywa na Marekani na Korea Kusini.

Pyongyang imeelezea kuwa mazoezi hayo yanakiuka mkataba wa amani.

Ripoti hiyo ilitumwa kwa kamati ya vikwazo vya Korea Kaskazini katika Baraza Kuu la Usalama la UN, inasema: "Pyongyang ilitumia uhalifu wa hali ya juu wa kimtandao kuiba pesa kutoka kwa taasisi za kifedha na ubadilishanaji wa sarafu ya crypto-kukusanya mapato yake".

Wataalamu pia wanachunguza shughuli za kimtandao zinazolenga malipo kupitia fedha za kigeni.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa shambulio la Korea Kaskazini dhidi ya sarafu ya crypto- imeisaidia kukusanya fedha kwa njia ambazo ni vigumu kutambuliwa na ikilinganishwa na ukaguzi wa kawaida unaofanywa na sekta ya benki.

Pia imeeleza kuwa Korea Kaskazini imekiuka vikwazo vya UN kwa kutumia njia haramu ya kubadilishana fedha pamoja na kupata vifaa vya kutengeneza silaha ya maangamizi.

Tangu mwaka 2006, Baraza Kuu la UN iliiwekea Korea Kaskazini vikwazo vya kuuza nje ya nchi hiyo bidhaa kama vile mkaa wa mawe, vyuma na vyakula vya baharini.

Pia iliiwekea kiwango cha uagizaji kutoka nje mafuta na bidhaa zake.

Taarifa ya kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Korea Kaskazini inaeleza kuwa ushirikiano wa kijeshi baina ya Kusini na Marekani unawalazimu kuendelea kufanya ugunduzi na majaribio ya silaha mpya.

"Tunalazimika kuendelea, kujaribu na kutumia makombora mazito ambayo ni muhimu kwa kujilinda," ilieleza taarifa iliyotolewa na Korea Kaskazini.

Taarifa hiyo pia imeeleza kuwa kinachoendelea baina ya Marekani na Korea ya Kusini ni uvunjwaji wa mazungumzo ya hivi karibuni baina ya Marekani na Korea Kaskazini (DPRK).

"Tumeshaonya mara kadhaa kuwa mazoezi ya kivita yatadhoretesha mahusiano baina ya Marekani na Korea Kaskazini na mahusiano ya Korea zote mbili kwa ujumla na kutufanya tufikirie kurejea tena hatua zetu za awali," ilieleza taarifa iliyotolewa na Korea Kaskazini.

Kwa mujibu wa Jeshi la Korea Kusini, makombora yaliyorushwa mwanzoni mwa wiki ni ya masafa mafupi yanayoenda mpaka kilomita 450.

Ndani ya wiki mbili zilizopita, Korea Kaskazini imekuwa ikirusha aina mpya ya makombora ya masafa mafupi.

Wiki iliyopita Korea Kaskanini ilirusha makombora mawili yaliyoangukia kwenye bahari ya Japani.

Kim Jong- Un mwaka jana wakati wa mkutano wake na Rais wa Marekani, Donald Trump nchini Singapore alikubali kuwa atakomesha vitendo vya majaribio silaha za nyuklia.

Kim pia alisema Korea Kaskazini haitarusha tena makombora ya masafa marefu. **BBC**

# Waingia mitini na bil. 430/-

INATOKA UK.2

kupitia orodha ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi wao.

Ngole alibainisha kuwa tangu mwaka 1994 serikali ilipoanza kutoa mikopo hiyo, Watanzania 479,779 wamenufaika kwa kupewa mikopo yenye jumla ya Sh. trilioni 3.889.

**RIPOTI ZA CAG**

Katika ripoti yake ya mwaka wa fedha 2017/18 aliyoiwasilisha bungeni Aprili 10, mwaka huu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad (pichani), alisema amebaini HESLB imeshindwa kufahamu waliko wakopaji wa mikopo ya elimu ya juu yenye thamani ya Sh. trilioni 1.46.

"Kiasi hiki cha fedha ni kikubwa sana ikizingatiwa kuwa Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya HESLB kinaitaka bodi kutengeneza mtandao na kushirikiana na taasisi na mashirika mbalimbali ili kuwatambua wadaiwa na kuwezesha kupata marejesho ya mikopo hiyo," alisema.

Prof. Assad alisema HESLB inapaswa kushirikiana na taasisi na vyanzo vingine vya taarifa ili kuiongezea nguvu kwenye kanzidata yake kuwatambua wakopaji ambao hawajulikani waliko.

Vilevile, katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2016/17, CAG Assad alisema amebaini HESLB imewafikisha mahakamani wadaiwa sugu wawili tu katika kipindi cha miaka miwili ilhali taarifa zinaonyesha kuna wadaiwa sugu 163,394 wanaopaswa kuchukuliwa hatua hizo za kisheria.



Alisema amebaini kuna udhaifu katika uchukuaji wa hatua dhidi ya wadaiwa sugu wa madeni ya mikopo, akieleza kuwa wakati wa ukaguzi, bodi hiyo ilikuwa na wadaiwa sugu 163,394, lakini kumbukumbu za bodi zilizowasilishwa kwa wakaguzi zilionyesha kulikuwa na wadaiwa sugu 18.

Alisema pia amebaini urejeshaji wa mikopo na ukusanyaji wa madeni kwa kipindi cha kuanzia 2012/13 hadi 2016/17 ni chini ya asilimia 50 ya mikopo iliyoiva.

Prof. Assad alishauri bodi hiyo kutambua na kuchukua hatua za kisheria mara kwa mara dhidi ya wadaiwa sugu na wanufaika wanaokiuka masharti ya ulipaji mikopo ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadhamini na waajiri wao.

"Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapaswa kujitathmini kama ina uwezo wa kuendelea kusimamia utendaji wa moja kwa moja wa HESLB katika kushughulikia urejeshaji wa mikop na ukusanyaji wa madeni ya mikopo ama kuipa kazi taasisi nyingine ya serikali kama vile Wizara ya Fedha na Mipango yenye ujuzi na uzoefu wa masuala hayo," CAG Assad alishauri.

## Wananchi na mwekezaji waushtaki uongozi wilaya

INATOKA UK. 3

mifugo yao na kupata mavuno makubwa kwa kuwa na ng'ombe wenye uzito mkubwa na kuongeza uzalishaji wa maziwa.

Bajuta alisema katika kipindi chote alichosumbuliwa na baadhi ya viongozi wa wilaya hiyo, amepata hasara ya Sh. bilioni 2.5 na kama uwekezaji huo ungeendelea kwa kipindi chote cha miaka tisa, angezalisha jumla ya ng'ombe 1,458, mbuzi 1,080 kondoo 864 na kufanikiwa kuwasaidia wafugaji wa asili madume na kuleta faida kwao na taifa kwa ujumla.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Waziri Mpina alisema serikali ya awamu ya tano inayoalika wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi, kamwe haiwezi kukubali kuwa kikwazo kwa wawekezaji ambao tayari wameshaonyesha nia njema kuwekeza kwenye sekta hiyo na kusisitiza iko tayari kumtafutia ardhi eneo lolote mwekezaji wa aina hiyo.

Waziri Mpina alisema kabla kufika kijijini huko, alituma timu ya maofisa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenda kukagua mradi huo na walikuta miundombinu ya mifugo ikiwa kwenye hali nzuri na kutoa huduma na walikuta zaidi ya ng'ombe 400 aina ya Sahiwal na mbuzi na kondoo zaidi ya 400.

Mpina alisema baada ya kutembelea miradi ya mwekezaji huyo, amekuta ng'ombe na madume bora aina ya Sahiwal ambayo yamekuwa yakitumika kama shamba darasa kwa wafugaji wa eneo na kunufaika na uboreshaji wa koosafu za mifugo.

Alisema kwa sasa uhitaji wa mbegu za madume bora ni mkubwa, hali inayowafanya wafugaji wengi kuagiza madume hayo kutoka nje ya nchi kutokana na taifa kutokuwa na madume ya kutosha.

Alisema kitendo cha mwekezaji huyo kwenda kuwasaidia wafugaji hao ni jambo la kuungwa mkono kwa kuwa ni dhamira ya serikali kuboresha koosafu za mifugo yake.

Mpina alimtaka mwekezaji huyo wakati anasubiri utaratibu utakaotolewa na viongozi wa juu kuhusu suala hilo la ardhi, aendelee kuwahudumia wafugaji hao ili mifugo yao isidhoofike kwa kukosa huduma muhimu.

# Oxfarm yasaidia wakulima maelfu

INATOKA UK. 7

zimepandwa zao hili, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 0 hadi 40," alisema Bligea.

Aliongeza kuwa mradi huo ulianza na mshine 20 za kutumika kama mafunzo ambazo zinaongeza thamani zao hilo, ambapo wakulima baada ya kujifunza na kuona manufaa yake wameanza wenyewe kununua na zimefika zaidi ya 50.

"Katika kuongeza mnyororo wa thamani zao hili limetoa ajira zaidi ya watu 3,000 na wengi wakiwa wanawake na vijana, mkulima wa chini anapata kilo 100 hadi 200 kutoka kilo 10 hadi 20 walipokuwa wanatumia kisu katika kusindika," alisema Bligea.

Alisema Oxfarm kupitia Redeso wamefanikiwa kuwasaidia soko wakulima wa zao hilo na wengi wameanza kubadilika kutoka kulima mazao mengine na kuanza kulima mkonge kwa kasi kubwa.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo kutoka Kishapu, Tabu Hashimu, alisema awali hawakujua kama mkonge unaweza kubadilisha maisha yao kutokana na kuliona kama siyo zao lenye tija kubwa kwao.

"Tulikuwa tumezoa mazao yetu ya mahindi na pamba, na hali ya hewa ikiwa mbaya tunapata hasara, lakini sasa tunawashukuru Redeso na Oxfarm kwa kutuletea mkombozi, sasa hivi nazalisha kilo 5,000 hadi tani moja na mapato yangu kwa mwaka ni Sh. milioni tano hadi sita," alisema Hashimu.

Naye Meneja Kampeini wa Oxfarm, Jovitha Mlay, alisema shirika hilo linajivunia kuona maisha ya wakulima wa wilaya hizo yameanza kubadilisha kwa kiwango kikubwa kama malengo yake yalivyokuwa yamepangwa.

Alisema shirika hilo linawasaidia wakulima wa mazao mengine kama alizeti na mpunga, lengo likiwa kuwasaidia wakulima kuongeza thamani mazao hayo ili kufikia uchumi wa viwanda.

## Bodi yalalamikia utitiri viwanda

INATOKA UK. 7

ya serikali kupiga marufuku mifuko ya plastiki na hatutaki kurudi huko tena hivyo tuhakikishe kwa sasa hakuna kitu kibovu kinachoingizwa sokoni," alisema.

Akizungumzia vyama vya ushirika, Mfaume aliiomba serikali iweke usimamizi imara katika vyama hivyo ili virudishe ari na nguvu iliyokuwapo awali.

Alisema ari na nguvu ya vyama hivyo imedorora na haifanani na ile ya vyama vya ushirika vya miaka 10 au 15 iliyopita.

"Ari na nguvu ya vyama vya ushirika kwa kweli imefifia, amsha amsha ya vyama hivi si kama ya miaka iliyopita, nguvu imepungua kidogo, kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee kuna zaidi ya vyama 200, lakini naona havina msaada," alisema Mfaume.

Aliongeza: "Kama ambavyo tunaona inafanyika katika maeneo mengine, tunaamini kila mara viongozi wakuu wangekuwa wanavitembelea na kuvipa maelekezo mazuri na amsha amsha ya kuvisimamia ingesaidia vifanye vizuri kama zamani," alisema.

## Samia ataka vyuo vikuu

INATOKA UK. 2

kuwatupia macho ili wafanikiwe.

Naye Mkamu Mkuu wa chuo hicho Prof. Rafael Chibunda, akamshuruku Rais John Magufuli kwa kuwajengea maabara hiyo kubwa na ya kisasa kwa Afrika Mashariki, kwa kutoa Sh. bil 10.5 zikiwamo bilioni 9.1 za ujenzi huo, baada ya miaka minne mfululizo kukosa ruzuku serikalini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof Joyce Ndalichako, alisema Serikali imeendelea kutumia fedha nyingi kufanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya elimu ya juu ikiwamo kujenga na kuboresha miundombinu katika vyuo na ofisi.

Mkuu wa Chuo hicho, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Jaji Joseph Warioba, aliyebainisha kuwa licha ya taifa kufanikiwa kwenye kuondoa ujinga na maradhi kwa kuboresha sekta za elimu na afya, bado kuna changamoto kubwa ya umaskini hasa kwa wakulima wadogo vijijini ambao ni wengi.

Jaji Warioba alisema kwa sasa nchi unaweza kusema inajitosheleza kwa chakula, lakini kama wakulima wadogo ambao ndio wazalishaji wakubwa hawatawezeshwa kupiga vita umaskini, itakuwa kazi kubwa.

Makamu Mkuu wa ARU, Prof Idrissa Mshoro, alisema ujenzi wa maabara hiyo hadi kukamilika itatumia Sh. 11,452,390,954, na kwamba hadi sasa asilimia 87 ya ujenzi huo imefikiwa na amekwishalipwa Sh. bilioni 4.78.

## UTSS yatiwa moyo ujumbe

INATOKA UK. 5

jamii ya nchi za SADC kutokuwa na uelewa na kusababisha watu hao kushambuliwa, kunyanyaswa na kutengwa na jamii.

Katika maadhimisho hayo ya Siku ya Kimataifa ya watu wenye ualbino, Dk. Tax, alitoa ujumbe kwa kuiomba jamii kuendelea kutoa elimu kuhusu masuala yanayowaathiri watu wenye ualbino na kutaka ari ya kisiasa kutumika kuelimisha tatizo hilo.

Berthasia alisema wakati wakuu wa nchi za SADC na serikali wakikutana Tanzania katika Mkutano Mkuu wa nchi hizo, UTSS imewaomba viongozi hao kuweka mkazo wa kupambana na changamoto zinazowakuta watu wenye ualbino na kupata suluhisho.

"Tunawaomba viongozi wanachama wa SADC kuchukua hatua kwa kila mwanachama kuweka sera na mabadiliko ya kisheria ili kuweka ulinzi wa kutosha kwa watu wenye ualbino," alisema.

Alisema nchi za SADC lazima zitekeleze kwa vitendo kampeni za kutokomeza mtazamo hasi kwa watu wenye ualbino na imani za kishirikina zinazosababisha kupoteza uhai wao.

Kadhalika alisema Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano wa SADC ni heshima kubwa kwa wananchi na taifa kwa ujumla, mara ya mwisho ilikuwa mwenyeji wa mkutano huo miaka 16 iliyopita (2003).

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**ANAHITAJIKA MHASIBU SIFA:** MWANAMKE ELIMU: DIPLOMA MAWASILIANO: 0715 885533 / 0752 610700.

## MCHANGANYIKO

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

**VIWANJA VINAUZWA KISEMVULE:** malipo awamu mbili muda wa mwezi mmoja, urefu futi 50 kwa upana futi 40, bei Sh.1,700,000/= tu simu 0623528465/0752737534.

**WACHIMBAJI VISIMA-** Master Drilling:Tunachimba Visima virefu / vifupi mikoa ya Dodoma/Singida/ Arusha/Manyara tunatumia mashine kubwa za kisasa simu:0788767141.

**Wachimbaji Visima visima** Tanzania tunachimba Visima virefu na vifupi kwa gharama nafuu na ofa ya pampu ya bure, simu:0623528465/0713256904.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHAURI LA ARDHI NA. 32/2017**

**INNOCENT FRANK CHAMI............................MDAI**
**DHIDI YA**
1. CRDB BANK PLC
2. KIMBEMBE AUCTIONMARTIN LTD...............................WADAIWA

KWA: KIMBEMBE AUCTION MARTIN LTD
POPOTE PALE WALIPO

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 32/2017 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA; shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu ya Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya MHE.JAJI. MLACHA, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00)kamili asubuhi siku ya ijumaa tarehe 9/8/2019.
HIVYO unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
NA ENDAPO hutafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili itashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

IMETOLEWA kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 2/8/2019.

215365702

---

**KADI YA GARI IMEPOTEA**

**KAJUBI DIOCLES MUKAJANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.861 DLR** aina ya gari **TOYOTA PORTE.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

TAARIFA POLISI: **TAN/RB/1089/2019.**

215365602

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 47 YA MWAKA 2017**
**ABDULMALIK ISSA SHABAN................MDAI**
**DHIDI YA**
**FREDY SAMWEL KAULASA.................MDAIWA**
**HAPPYHERMAN LYIMO..................................MDAIWA**
**ACCESS BANK TANZANIA LIMITED........................MDAIWA**

**KWA**
**FREDY SAMWEL KAULASA**
**HAPPY HERMAN LYIMO**
**POPOTE MLIPO**

**KUITWA SHAURI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 22/08/2019 kujakusikiliza shauri la madai yaliyofunguliwa na mdai dhidi yenu.
Mnatahadharishwa kuwa endapo hamtafika siku hiyoshauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uhamuzi.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 29/07/2019.

215366702

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**CIVIL APPEAL/MISC CR.APPEAL CASE/CR.APPLICATION**
**CASE NO:.... 27......... 2019**
**NEEMA JOSEPH MNYENYELWA...................PLAINTIFF/PETITICIVER**
**VERSUS**
**EMMANUEL BORUZA BARIDI..................DEFENDANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/Hearing on 19th....Day of AUGUST...2019 at 09:00am Before Hon E.J.NYEMBEZE.........................S.RM

**YOU ARE** required to appear before this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support your case.

Given Under my Hand and the seal of the Court this ....1st...Day of AUGUST ...2019.

215366202

---

**KUPOTEA KWA KADI**

**Thobius Ngonyani Lyander** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba ya usajili **MC 553 AUS** aina ya TVS yenye chasis namba MO6M14PK3E4140857, engine namba OK4AFA187830.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/OST/RB/189248/2019**

115365902

---


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# D.C. UNITED WAMTAKA OZIL




**LONDON,** England

KLABU ya D.C. United itafanya mazungumzo wiki hii na wawakilishi wa kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil, kwa mujibu wa ESPN FC.

Gazeti la Washington Post limeripoti kwamba D.C. imeonyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo wa zamani wa timu ya taifa ya Ujerumani.

Habari za D.C. United kuamua kumfuata Ozil ni kwa ajili ya kuziba pengo la Wayne Rooney ambaye anamalizia msimu wa Ligi Kuu ya Marekani, MLS, na atajiunga na timu ya daraja la kwanza ya England Derby County akiwa kocha mchezaji Januari mwakani.

Ozil amekuwa kwenye wakati mgumu wa kupata namba ya kucheza katika kikosi cha kwanza chini ya kocha, Unai Emery pale Arsenal.

Mchezaji huyo msimu uliopita alicheza dakika 1,741 tu kwenye Ligi Kuu, zikiwa chache zaidi tangu msimu wa 2007-08 wakati alipopata nafasi ya kucheza Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, pale Werder Bremen.

Tangu alipojiunga na washikabunduki hao mwaka 2013, Ozil amecheza mechi 231, akifunga mabao 43 huku akishinda mataji matatu ya Kombe la FA na lile la Ngao ya Jamii.

Ozil alianza kucheza soka ya kulipwa mwaka 2006 akiwa na Schalke kabla ya kujiunga na Bremen, Real Madrid na halafu Arsenal.

Alikuwa sehemu ya kikosi cha Real Madrid kilichoshinda taji la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, msimu wa 2011-12 pamoja na kombe la Copa del Rey.

Katika mechi za kimataifa, Ozil alicheza mechi 92 akiwa na Ujerumani akifunga mabao 23, alikuwa sehemu ya kikosi cha Kombe la Dunia kilichotwaa kombe hilo mwaka 2014.

Alistaafu kuichezea Ujerumani Julai 2018 akiwa na umri wa miaka 29 kwa madai ya ubaguzi wa rangi.

# Rooney: Familia imenirudisha England

**LONDON,** England

WAYNE Rooney amesema kwamba elimu ya watoto wake ndio ilikuwa kigezo kikubwa zaidi kwa yeye kuamua kuondoka nchini Marekani na kurudi nchini England na kujiunga na klabu ya Derby County.

Akizungumza kwenye mkutano wake na waandishi wa habari Jumanne baada ya kutangazwa kujiunga na klabu hiyo, Rooney alibainisha kwamba familia ndiyo ilikuwa kigezo kikubwa cha kuamua kujiunga na timu hiyo.


"Ni kitu nilichokiangalia kwa makini, nikiwa na watoto wa kiume wanne na kwa ajili ya kijana wangu mkubwa (Kai) ni muda wa shule na ningependa wasome huku," alisema Rooney.

"Jambo la muhimu kwangu ilikuwa ni familia yangu. Na vitu vingine vichache vilinifanya niamue kurudi hapa."

Pia amesema sababu nyingine ilikuwa ni kufuata nyayo za wachezaji wenzake wa zamani wa England kwenye kazi ya ukocha, Steven Gerrard na Frank Lampard.

Rooney amejiunga na timu hiyo akiwa kocha mchezaji, huku Lampard aliondoka Derby na kuwa kocha wa Chelsea, huku Gerrard ameanza msimu wa pili akiwa kocha wa Rangers.

Rooney atarudi nchini Marekani kumalizia msimu wake akiwa na DC United na atajiunga rasmi na Derby Januari mwakani.







# *Newcastle United yafikia makubaliano kumsajili Krafth*

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle United imefikia makubaliano na Amiens kumsajili beki wa kulia, Emil Krafth.

Wiki iliyopita Newcastle ilitoa ofa ya pauni milioni 4.5 kumsajili beki huyo, lakini klabu hiyo ya nchini Ufaransa iliikataa.

Lakini sasa Newcastle imetuma ofa ya pili kwa Krafth ya pauni milioni 6 ambayo imekubaliwa na Amiens.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 raia wa Sweden alitumia miaka minne kucheza nchini Italia akiwa na Bologna na baadaye akajiunga na Amiens.

Kocha mpya wa Steve Bruce tayari amesajili wachezaji kama Joelinton, Jetro Willems na Allan Saint-Maximin,

Magpies hao wataanza kampeni ya Ligi Kuu kwa kucheza na Arsenal Jumapili.

## HABARI MICHEZO



# PIQUE: NEYMAR TAMKA WAZI KAMA UNATAKA KURUDI BARCA

**MIAMI,** Marekani

GERARD Pique amesema Neymar anatakiwa kuzungumza wazi kama anataka kusukuma uhamisho wake wa "utata" kurudi Barcelona kutoka Paris Saint-Germain kipindi hiki cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa ESPN FC, Barca inaangalia dili hilo la kumsajili Neymar, huku Mkurugenzi wa soka wa PSG, Leonardo amethibitisha kwamba klabu hiyo inaweza kumuuza nyota huyo wa Brazil kwa kiasi kama klabu itafikia kiasi wanachokitaka.

Neymar mwenye umri wa miaka 27, aliondoka Barca kwenda PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 miaka miwili iliyopita na kwa namna alivyolazimisha uhamisho wake aliwakasirisha baadhi ya mashabiki wa klabu hiyo ya pale Katalyunya.

Hata hivyo, Pique amesema atajisikia vizuri kumkaribisha tena hapo kwenye dimba la Camp Nou, lakini akasema haitakuwa kazi rahisi kwa mabingwa hao wa Ufaransa kumwachia.

"Nafikiri Neymar ni mchezaji mkubwa ambaye anajua vizuri vyumba vya kubadilishia nguo, jiji pamoja na klabu yetu," alisema beki huyo katika mkutano wake na waandishi wa habari juzi Jumatano kabla ya mchezo dhidi ya Napoli katika dimba la Hard Rock mjini Miami.

"Kuna watu ambao hawakuwa na furaha kwa jinsi alivyoondoka, lakini kuna watu wengi ambao walikuwa na furaha kubwa kutokana na kiwango chake.

"Ni uhamisho ulioleta utata. Yeye ni mchezaji wa PSG na yupo kwenye kikosi ambacho kinauwezo wa kushinda kila taji.

"Kama nafasi inakuja, mnajua uhusiano wangu na yeye. Nitajisikia furaha kama atarudi, lakini ni mchezaji wa PSG.

"Anatakiwa Neymar mwenyewe ndio azungumze hilo. Bila shaka tunazungumza nae, lakini si sawa kuweka hadharani mambo binafsi tunayozungumza. Kama anataka kuzungumza au kutoa maoni yake, anatakiwa kujitokeza hadharani na kuzungumza wazi."

# *Lukaku ajifua Anderlecht, akitaka kuondoka United*

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Romelu Lukaku amefanya mazoezi na Anderlecht kwa siku ya pili wakati akiendelea kutafuta nafasi ya kuondoka hapo kwenda dimba la Old Trafford.

Lukaku alipigwa picha akiwa na klabu hiyo ya nchini Ubelgiji Jumatatu baada ya uhamisho wake kwenda Juventus kushindikana baada ya United kushindwa kufikia makubaliano na Paulo Dybala ambaye alikuwa sehemu ya kukamilisha uhamisho huo.

Awali Lukaku alitakiwa kurudi kwenye kambi ya mazoezi ya Man United pale Carrington, lakini Jumanne alipigwa picha akiwa akifanya tena mazoezi na Anderlecht, ambako rafiki yake Mbelgiji mwenzake, Vincent Kompany ni kocha.

Maofisa wa United walikataa kuzungumza lolote kuhusu Lukaku kufanya mazoezi na klabu hiyo. Lukaku alifanya mazoezi ya peke yake Jumatatu kabla ya kujiunga na kikosi cha timu ya vijana chini ya umri wa miaka 18.

Hajaichezea Man United katika mechi sita za kirafiki za maandalizi ya msimu mpya wa ligi kwa madai kwamba ana maumivu ya kifundo cha mguu.

Lukaku aliiambia United anataka kuondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto, lakini Inter Milan waliokuwa wakimtaka kwa udi na uvumba wameshindwa kufikia ada ya kumnunua ya pauni milioni 80.



# Alves ajipanga kuichezea Brazil Kombe la Dunia 2022



**SAO PAULO,** Brazil

DANI Alves amesema amejiunga na Klabu ya Sao Paulo ili kujiimarisha zaidi kwa ajili ya michuano ya Kombe la Dunia ya mwaka 2022 nchini Qatar, wakati ambapo atatimiza umri wa miaka 39.

Zaidi ya mashabiki 40,000 wa Brazil walijitokeza juzi Jumanne kumpokea beki huyo wa zamani wa Barcelona, Juventus na Paris Saint-Germain aliyeamua kurudi katika klabu yake hiyo ya utotoni.

Alves ambaye alikuwa nahodha akiiongoza Brazil kutwaa ubingwa kombe la mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, mwezi uliopita amesaini mkataba utakaomweka hapo hadi Desemba 2022.

Aliondoka PSG akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake kumalizika Julai mwaka huu wakati wa kipindi cha majira ya joto. Alves amebeba makombe 40 kwa kipindi chake chote cha uchezaji na sasa anaangalia kulitwaa jingine.

"Nina ndoto ya kucheza michuano ya Kombe la Dunia ijayo na nahitaji timu itakayoniamini, katika historia yangu ya soka," amesema Alves akiwaambia waandishi wa habari.

"Nimekuja Sao Paulo kuleta matokeo, sitaki mtu yeyote afikirie kwamba nimekuja kumaliza kipindi changu cha uchezaji. Bado nina matarajio mengi."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DYBALA SASA MUDA UNAHESABIKA SPURS

## Wavutana mshahara, ataka kumpiku Kane, awekewa pauni 200,000 mezani lakini...

**TURIN,** Italia

PAULO Dybala anahatarisha uhusiano wake usioweza kutenganishwa na Juventus ikiwa atakataa kujiunga na Tottenham kutokana na mshahara wake mkubwa anaoutaka.

Spurs imefikia makubaliano na Juventus kuhusu dau la uhamisho linaloelezwa kuwa takriban pauni milioni 69, lakini Dybala, ambaye alitarajiwa kutua Manchester United pia dili hilo likafa kutokana na kuhitaji mshahara mkubwa, anataka kulipwa pauni 300,000 kwa wiki, mshahara ambao utamfanya kumpiku mchezaji anayelipwa kiasi kikubwa Spurs, Harry Kane anayepokea pauni 250,000 kwa wiki.

Kwa mujibu wa vyanzo vya karibu na Dybala, mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina yupo tayari kutua Tottenham na amevutia wote kwa kucheza chini ya raia mwenza Mauricio Pochettino na kuishi London.

**Mpenzi wa Dybala, Oriana Sabatini, inaeleweka pia amemshauri Dybala kwamba angependa kuishi London.**

Lakini uhamisho huo bado unategemea zaidi na Tottenham kuongeza ofa ya mkataba wao, na utayari wa Dybala kukubali mshahara wa chini.

Endapo Dybala, 25, hatakubali mpango huo na kusema hapana kwa Spurs, mapema zaidi baada ya kukataa kutua United, Juventus itakasirika.

Ada yake ya uhamisho inahitajika ili kuwezesha kufanikisha uhamisho wa Romelu Lukaku kutoka United, na miamba hiyo ya Italia, kwa zote zitakuwa zikikabiliwa na kukosa wachezaji wao muhimu waliokuwa wakiwawinda na kuwaacha wachezaji wakiwa hawana thamani tena. Dybala anakabiliwa na kuwa ziada Juve kama hatapata klabu nyingine.

Tottenham bado haijazungumza dili hilo na Dybala. Mawakala wake wapo London kujaribu kukubaliana malipo binafsi, na wanataka kunufaika na fedha nyingi zilizopo Ligi Kuu England.

Ofa ya wazi kwa Spurs inaeleweka kuwa tayari kumlipa pauni milioni tisa kwa mwaka ambazo ni zaidi ya pauni 170,000 kwa wiki, na aibu katika mkataba wa Kane.

Kuna ishara kwamba Dybala anataka pauni 300,000 kwa wiki, lakini Tottenham inaweza kumwekea mezani pauni milioni 10 kwa mwaka sawa na pauni 200,000 kwa wiki.

Pointi zingine kubwa za kuambatana na dili la United zilikuwa pauni milioni 15 kwa mwaka na shida ya wakala wake ilikuwa haki ya matangazo. Dybala pia italazimika kuachana na ada ya wakala wake kugomea mpango huo.

## ZISIKUPITE

### COUTINHO ANUKIA TOTTENHAM

TOTTENHAM bado ipo tayari kuipata saini ya kiungo mshambuliaji wa Barcelona, Mbrazil Philippe Coutinho, 27, wakati Arsenal ikiwa haijawahi kuvutiwa naye. ***(ESPN)***

### CANCELO AFUZU VIPIMO CITY

MANCHESTER City jana ilitarajiwa kuthibitisha kuipata saini ya Joao Cancelo kutoka Juventus baada ya beki huyo Mreno kufaulu vipimo vya afya na mabingwa hao wa England. ***(Star)***

### ERIKSEN AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United imepiga hatua katika mpango wa kuipata huduma ya kiungo wa Tottenham, Mdenmark Christian Eriksen, 27. ***(Telegraph)***

### YAGOMEWA UPAMECANO

ARSENAL imetoa ofa ya pauni milioni 55 kwa beki wa kati Mfaransa Dayot Upamecano, 20, lakini klabu yake inayoshiriki Bundesliga, RB Leipzig ikawakatalia. ***(Bild - in German)***

### OZIL KUMRITHI ROONEY DC UTD

DC United inajiandaa kufanya mazungumzo na wawakilishi wa kiungo wa Arsenal, Mjerumani Mesut Ozil, 30, wakati ikisaka mbadala wa nahodha wa zamani wa England, Wayne Rooney, 33, anayetarajiwa kutua Derby Januari mwakani. ***(Mirror)***

### MADRID, UTD ZAITIWA NEYMAR

PARIS St-Germain imetoa ofa kwa Manchester United, Juventus na Real Madrid kumsajili Neymar, 27. Mabingwa hao wa Ufaransa hawataki kuiruhusu Barcelona kumsajili tena nyota huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(Sport)***

### LLORENTE KUSHITUKIZWA UTD

MANCHESTER United inapanga kushtukiza kwa kwenda kumsajili straika wa zamani wa Tottenham, Fernando Llorente, na Mhispania huyo akipatikana kama mchezaji huru. ***(Sky Sports Italy, via Metro)***

### YAFUNGUKA KWA FABINHO

LIVERPOOL haina lengo la kumuuza kiungo wao Mbrazil Fabinho, 25, licha ya kuwapo kwa tetesi za dakika za mwisho zinazomhusisha na Real Madrid. ***(Echo)***

### AJER KUMRITHI MAGUIRE

LEICESTER City inamtaka beki wa Celtic, Mnorway Kristoffer Ajer, 21, kama mbadala wa beki wa kati wa kimataifa wa England, Harry Maguire, 26, aliyejiunga na Man United. ***(Star)***

### LUKAKU HAJARUDI CARRINGTON

STRAIKA wa Manchester United, Mbelgiji Romelu Lukaku, 26, hajarudi kujifua Carrington kwa mara ya kwanza huku kukiwa na tetesi kuhusu mustakabali wake wa baadaye. ***(Mirror)***

### YAGOMEWA KWA DOUCOURE

WATFORD imekataa ofa ya pili ya pauni milioni 36.7 kutoka Everton kwa kiungo Mfaransa Abdoulaye Doucoure, 26. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Mabondia kuibuka na bima ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

HOMA ya mapambano ya ubingwa Afrika Mashariki na Kati imezidi kupanda baada ya Kampuni ya Bima ya Resolution kuahidi kutoa bima ya afya ya mwaka mzima kwa mabondia watakaoibuka na ushindi wa Agosti 24, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Resolution Insurance, Maryanne Mugo alisema mchezo wa ngumi ni miongoni mwa michezo ambayo wachezaji wake wana kila sababu ya kuwa na bima ya afya.

Kwa upande wake mratibu wa kiufundi wa pambano hilo, Yassin Abdalah, alisema ujio wa Resolution na kuboresha zawadi kwa washindi ni suala la kupongezwa kwani uwepo wa wadhamini katika ngumi ni jambo muhimu kwa maendeleo ya mchezo huo.

Aliwataja mabondia hao kuwa ni Nasibu Ramadhani na Issa Nampepeche pamoja na Haidary Mchanjo na Tonny Rashidi na katika mapambano ya utangulizi, Lukmani Ramadhan vs Ismail Haridi pamoja na Bakari Dunda na Kudura Tamimu.

Naye Mratibu Mkuu wa Pambano hilo, Selemani Semunyu, alisema mbali na mapambano hayo pia kutakuwapo na mabondia kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania wanaojiandaa na mashindano ya Dunia ya Majeshi nchini China.

## Mlandege kufyeka wachezaji 10

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mlandege itawatema wachezaji 10 katika kikosi chake cha mwaka huu kinachojiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Zanzibar 2019/2020, ili kusajili nyota wengine wapya, lengo likiwa ni kusaka mafanikio zaidi ya msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Mbaraka Hamidi, alisema klabu yao ilikuwa na msimu mzuri kwa mwaka uliopita na kuleta ushindani mkubwa licha ya kukosa mataji mawili la Ligi Kuu na lile la Kombe la FA Zanzibar.

Aidha, Hamidi alisema mabadiliko ya klabu yao yatakuwa kwenye ubora na kwamba watasajili wachezaji vijana baada ya baadhi ya nyota wao kutimkia klabu nyingine mbalimbali ikiwamo mlinzi wao wa kati mahiri, Abubakar Azizi aliyesajiliwa na Klabu ya Malindi.

Hata hivyo, hakuweka wazi majina ya wachezaji ambao wataachwa kwenye idadi hiyo badala yake akaeleza kuwa ni mapema sana kuzugumzia wachezaji hao kwani ripoti ya mwalimu haikuweka bayana anaotaka watemwe.

Ligi Kuu Zanzibar inatarajiwa kuanza rasmi Septemba 25, mwaka huu kwa kupigwa mchezo wa Ngao ya Jamii siku moja kabla kati ya mabingwa wa Kombe la FA, Malindi na Mabingwa wa Ligi Kuu, KMKM.

# AZAM YATUA ETHIOPIA NA MATUMAINI KIBAO

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Kombe la Shirikisho (FA Cup), Azam FC wametua salama nchini Ethiopia wakiwa na matumaini ya ushindi kuelekea mechi yao ya Kombe la Shirikisho Afrika raundi ya awali dhidi ya wenyeji, Fasil Ketema (Ethiopia 1) utakaopigwa Jumapili wiki hii.

Azam FC jana ilitua Ethiopia ikiwa tayari imetanguliza mashushu wake wa kuwaandalia mazingira mazuri kuelekea mechi hiyo, ambao waliongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin, 'Popat'.

**Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffary Iddi Maganga, msafara wa timu hiyo ulitua salama jijini Addis Ababa na walikuwa wakisubiri ndege jana mchana kwa ajili ya kuunganisha kwa safari kuelekea Gondar Kaskazini mwa Ethiopia itakapopigwa mechi hiyo.**

"Tumefika Addis Ababa salama na sasa tunasubiri ndege ya pili ya kwenda Gondar sehemu ambayo mechi itachezwa," alisema.

Kabla ya kukwea pipa usiku wa kuamkia jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Etienne Ndayiragije aliliambia Nipashe kuwa licha ya maandalizi mazuri waliyoyafanya wataivaa Fasil Ketema kwa tahadhari kubwa lakini ana uhakika ya kupata matokeo.

"Tunakwenda kucheza kwa tahadhari kwa sababu tutakuwa ugenini, lengo ni kutimiza ndoto zetu," alisema Ndayiragije.



Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa (katikati), akiwapongeza mashabiki wa Simba kwa kujaza Uwanja wa Taifa, pamoja na mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji (kulia) kwa kuamua kuwekeza katika soka. Pongezi hizo alizitoa wakati alipokuwa mgeni rasmi katika tamasha la Simba Day juzi. Kushoto ni Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# *ITV yajitosa kudhamini Mr. Tanzania*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya shindano la kumtafuta Mr. Tanzania 2018 kushindwa kufanyika mwaka jana kutokana na kukosekana kwa wadhamini, hatimaye ITV imejitosa kudhamini shindano hilo mwaka huu ambalo litakalofanyika Novemba 26, kabla ya mshindi kupatikana katika fainali itakayofanyika siku tatu baadaye kwenye Hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Tanzania Body Building Federation (TBBF), Francis Mapugulo, alisema lengo la shindano hilo ni kuhakikisha wanapata mshindi bora na kuwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi siku ya shindano hilo.

Alisema mwaka huu katika shindano hilo la kumtafuta Mr. Tanzania 2019, yameongezeka madaraja mawili ambayo ni Mr. Physique na Miss Fitness.

"Mwaka huu tumeongeza madaraja hayo ambapo katika makundi hayo kila mshindi atapewa zawadi na wote watakaokuwa wameshiriki hata wasiposhinda watapewa kitu kidogo," alisema katibu huyo.

Aidha, alisema kutakuwa na makundi matatu ya Mr. Tanzania, ambao Kundi la Kwanza linakuwa la uzito wa kilo 60-69, na lingine litakuwa la uzito wa kilo 70-79, na Kundi la Tatu litakuwa la uzito wa kilo 80-100.

"Katika makundi hayo tutatafuta mshindi ambaye atashiriki Mr. Tanzania na upande wa Miss Fitness hawatakuwa na uzito watakuwa uzito huru.

Alisema mshindi wa kwanza Mr. Tanzania atapata zawadi ya Sh. milioni tano, na kwa kundi la tatu mshindi wa kwanza atazawadiwa Sh. milioni tatu, mshindi wa pili milioni mbili na wa tatu milioni moja.

Kwa upande wa Mr Physique mshindi wa kwanza atapata Sh. milioni 3, mshindi wa pili milioni 1 na mshindi wa tatu atajinyakulia kiasi cha shilingi laki 5, hivyo hivyo na upande wa Miss Fitness zawadi zipo sawa.

Alisema mwaka jana walishindwa kufanya shindano hilo kutokana na ukosefu wa wadhamini ndio maana huwa wanafanya mara moja kila baada ya miaka miwili.

"Lengo la kufanya haya mashindano ni kuhakikisha mchezo huu unakuwa kama ilivyo michezo mingine, tunaomba wasichana wajitokeze kwa wingi ili wapate zawadi kutokana na mazoezi waliyoyafanya kuweka miili yao kuwa na mvuto," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa ITV ambao ndio wadhamini, Koigi Macharia, alisema mwaka huu shindano hilo litakuwa la kipekee, kutokana na mvuto ulioongezeka.

"Sisi kama ITV tutaendelea kuwatangaza mpaka watakapofikia tamati ya shindano hilo, naamini mwaka huu yatakuwa ya aina yake," alisema Macharia.

# Michezo

Alhamisi Agosti 8, 2019

Nipashe




Dybala muda unahesabika Spurs UKURASA 30



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, akizunguka uwanja kuwasalimia mashabiki wa timu hiyo baada ya kutambulishwa yeye na kikosi cha msimu mpya wa 2019/20 kwenye tamasha la kilele cha Wiki ya Simba, lililofanyika Uwanja wa Taifa juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# 'ASANTENI, SASA CAF'

## ●●● Simba yatangaza kuanza kazi Ligi ya Mabingwa, kuwafuata UD Songo Ijumaa huku...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuhitimisha kilele cha SportPesa Simba Wiki kwa mashabiki kujitokeza kwa wingi na kuujaza Uwanja wa Taifa, huku wakishuhudia timu yao ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Power Dynamos ya Zambia juzi, uongozi wa klabu hiyo umesema "asanteni sana" na kutangaza vita mpya kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwishoni mwa wiki.

**Katika ukurasa wa Instagram wa klabu hiyo, imeandika: "Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba Sports Club Company Limited, pamoja na Secretariat ya Simba tunawaambia Wanasimba na Watanzania wote Asanteni sana. Iga Ufe This is Next Level".**

Aidha, umeeleza kuwa hauna neno la kusema kwa sasa kwa mashabiki wake zaidi ya kuwashukuru kwa kujitokeza kwa wingi juzi Uwanja wa Taifa.

Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara alisema hakuna jambo jingine la kuwaambia mashabiki na wapenzi wa Simba zaidi ya shukrani.

"Mengi makubwa ambayo mmefanya kwa kuitikia wito hakuna cha kuwaambia zaidi ya kusema asante kwa sapoti yenu na kujitokeza kwenu Uwanja wa Taifa.

"Picha linaanza siku yenyewe ilikuwa ni katikati ya wiki sipati picha kama ingekuwa siku ya mapumziko namna ambavyo Wanasimba wangeitikia ila yote kwa yote asanteni sana."

Katika mechi hiyo mashabiki wa Simba waliweka rekodi kwa kujitokeza kwa wingi na kuujaza Uwanja wa Taifa, hivyo kulazimika kuwekewa TV kwenye Uwanja wa Uhuru ili kushuhudia kilichokuwa kikiendelea ikiwa ni pamoja na mechi hiyo, baada ya dimba hilo la shughuli kujaa.

Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Crescentius Magori, akizungumzia kikosi hicho kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Jumamosi ugenini dhidi ya UD Songo ya Msumbiji, alisema kila kitu kipo sawa na wana matumaini ya kupata matokeo chanya.

Simba itashuka dimbani Msumbiji Jumamosi kuivaa UD Songo kwenye mechi yao ya raundi ya awali kabla ya kurudiana wiki mbili zijazo Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na mshindi wa jumla atakutana na timu itakayoshinda nyumbani na ugenini kati ya FC Platinum ya Zimbabwe ama Big Bullets ya Malawi.

"Timu itaondoka Ijumaa asubuhi kuelekea Msumbiji kwa ndege ya kukodi na tutarejea baada ya mechi kumalizika kuja kujiandaa na mchezo wa marudiano pamoja na ule wa ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC.

"Tumefanya hivyo ili kukwepa usumbufu wa kuunganisha ndege mbili kwa wakati mmoja ilhali tunaweza kufanya mambo makubwa kwa ajili ya klabu yetu," alisema.

Msimu uliopita Simba ilifanikiwa kufika robo fainali ya michuano hiyo kabla ya kutolewa na TP Mazembe ya DR Congo.

# Yanga yaivutia gia Township Rollers

**Na Mwandishi Wetu**

YANGA leo itakamilisha 'kupangua gia' zake kuelekea mechi yake ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers ya Botswana kwa kuivaa Malindi kwenye mechi ya kujipima nguvu itakayopigwa usiku katika Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar.

Jana usiku Yanga ilicheza mechi ya kwanza ya kirafiki visiwani Zanzibar dhidi ya Mlandege, ikiwa ni baada ya kutoka kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya kwenye mechi ya kilele cha Wiki ya Mwananchi iliyopigwa Uwanja wa Taifa Jumapili iliyopita.

Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema mechi hizo mbili zitamsaidia kurekebisha makosa aliyoyabaini dhidi ya Kariobangi Sharks kabla ya kukutana na Township Rollers Uwanja wa Taifa Jumamosi.

Zahera yupo katika kibarua kigumu cha kuhakikisha anawaunganisha vema nyota wake kabla ya kuivaa Township Rollers, kutokana na klabu hiyo kusajili nyota wengi wapya.

Endapo Yanga itapata matokeo Jumamosi na kisha ugenini, itakutana na mshindi kati ya Green Mamba ya Eswatini na Zesco ya Zambia, na ikishinda itafuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, Caf.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002